# Nipashe

Jumatano Juni 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0579942

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

## Mahakama yatoa hati ya kukamatwa Wema Sepetu

UKURASA 3



Ukurasa 18

Trump 'aupiga tafu' mpango wa Brexit ziarani nchini Uingereza

UCHAMBUZI:

KUELEKEA UCHAGUZI S/MITAA;

Hofu ya sheria inavyobana wanahabari

Ukurasa 19

Kimataifa

Tunisia, Niger 'kidedea' uchaguzi wa Baraza la Usalama la UN

Ukurasa 17

siasa

JUMATANO JUNI 12, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukimya kutawala migogoro EAC, dalili za kushindwa kwa jumuiya?

Na Mashaka Mgeta

NI kama hakuna kinachoendelea katika kupata suluhu ya migogoro 'inayoitafuna' baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hususani kati ya Rwanda dhidi ya Burundi na Uganda.

Kwa hali ilivyo sasa, mataifa wanachama wa EAC yaliyo katika migogoro ya kidiplomasia yanaendelea 'kujitenga na maadui' zao, yakitafuta jinsi yanavyoweza kukuza uhusiano hasa unaolenga nyanja za kiuchumi.

Wakati hayo yakiendelea, EAC inaendelea na mchakato utakaoziwezesha nchi wanachama kuwa shirikisho moja.

Kushamiri kwa migogoro hiyo hakutoi taswira nzuri kwa hali ya baadaye ya EAC. Tayari nchi kama Rwanda inayoguswa kuwa 'kiini' cha migogoro hiyo, ikifungua uhusiano zaidi na mataifa mengine ya ukanda wa Kusini mwa Afrika, hususani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Migogoro inayoendelea 'kuitesa' EAC inajumuisha ule uliodumu kwa takribani miaka minne sasa ukizihusisha nchi za Burundi na Rwanda. Burundi 'ilishapa' kwamba Rwanda haina sifa za kuwa mshirika wake wa

Endelea 16

Rais John Magufuli wa Tanzania (kushoto) akiwa na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. PICHA: MTANDAO

Sudan yavuna ilichopanda Janjaweed wakitwaa hatamu Baraza la Kijeshi

Ukurasa 15

China, Russia zapanua ushirikiano kukabili uhasama wa Marekani

Ukurasa 20

UKURASA 13



# Wadaiwa sugu ardhi mtegoni

**LUKUVI** awapa siku tisa kulipa kodi ya ardhi, zimo TTCL, Tanesco, TPA, NHC, zikishindwa kufutiwa milki, mali kunadiwa...

*Endelea ukurasa wa 2*

## RIPOTI MAALUM



### VITAMBULISHO MACHINGA SOKONI MKANGANYIKO

UKURASA 4

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**WAKILI WA KISENA AHOJI UPELELEZI**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayowakabiliwa wanafamilia wawili, Mkurugenzi wa Kampuni ya Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (Udart), Robert Kisena (46), mke wake...

UKURASA WA 3

**DARASA LA SABA WAITWA JKT**

VIJANA waliomaliza elimu ya darasa la saba wenye umri wa kuanzia miaka 16 hadi 18 wenye ndoto za kupata mafunzo ya jeshi sasa wamealikwa kujiunga...

UKURASA WA 26

**ACT KUTINGA KORTINI WAKURUGENZI UCHAGUZI**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinatarajia kufungua kesi ya Kikatiba chini ya hati...


## Bei elekezi teksi yaiva

UKURASA 2


MICHEZO **BOCCO AZUA HOFU SIMBA USAJILI SAUZI** UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Waziri Lukuvi awapa siku 9 wadaiwa sugu pango la ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amezitaka taasisi, kampuni pamoja na mashirika 207, yanayodaiwa kodi na malimbikizo ya pango la ardhi kulipa kabla ya Juni 20.

Alisema wadaiwa hao ni wale wa muda mrefu wanaodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 200 na watakaoshindwa hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kufilisi na kupiga mnada mali zao.

Aidha, Lukuvi amesema idadi hiyo ya taasisi, mashirika pamoja kampuni 207 zilizoitwa hivi sasa ni awamu ya kwanza na awamu ya pili ambayo zaidi ya taasisi 600 wakiwamo vigogo, itafuata muda si mrefu.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na waziri huyo wakati alipokuwa akizungumza na wakuu wa taasisi, mashirika na kampuni zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi.

Lukuvi alisema kuwa mashirika, kampuni pamoja na taasisi hizo zinatakiwa kulipa kodi zinazodaiwa katika kipindi hicho ambacho kimetolewa na serikali na siyo vinginevyo.

Alisema serikali inawataka wadau hao wakubwa wa ardhi kuhakikisha wanalipa kodi hiyo ili kuunga mkono juhudi za serikali za kukusanya mapato ili kuboresha miundombinu mbalimbali.

"Hili siyo suala la awamu ya tano bali hii ni sheria ambayo ipo toka hata awamu hii haipo madarakani, hivyo basi kulipa kodi hakuna namna ya kukwepa wala kodi siyo jambo la hiyari ni takwa la kisheria," alisema Lukuvi.

Akijata baadhi ya mashirika yanayodaiwa kodi hiyo ya pango la ardhi, Lukuvi alisema Shirika la Mawasiliano nchini (TTCL), linaongoza kwa kudaiwa zaidi ya Sh. bilioni 40.

Mashirika mengini ni pamoja na Shirika la Umeme nchini (Tanesco) linalodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 25, Narco Sh. bilioni 23.4, NDC Sh. bilioni 17.5, Chuo cha Kilimo (SUA), Sh. bilioni 10.7, Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Sh. bilioni 9.1, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini (TAA) Sh. bilioni 8.1.

Wengine ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Sh. bilioni 1.6, Tazara, Sh. bilioni 1.8, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Sh. bilioni 2.3, TRC, Sh. bilioni 2.8, Benki Kuu (BoT), Sh. milioni 409, Mamlaka ya Bandari nchini (TPA), Sh. bilioni 1.6, TASO, Sh. bilioni 2.5, TBA, Sh. bilioni 1.5, TBL zaidi ya Sh. bilioni 1, na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Sh. bilioni 3.4.

Lukuvi alifafanua kuwa kwa mtu yeyote ambaye atashindwa kulipa kodi katika muda ambao umetengwa na serikali, hatua kali za kisheria zitachukulia ikiwa ni pamoja na kufuta umiliki wake, kunadi mali za taasisi husika ili kupata fedha pamoja na kuwafikisha mahakamani wahusika.

Aidha, alisema maeneo yote ambayo yamepatiwa leseni kwa ajili ya uchimbaji wa madini, lakini wamiliki wake wameongeza maeneo kwa kuwalipa wananchi fidia wanatakiwa kupata hatimiliki na kuanza kulipa kodi.

"Kampuni ya uchumbaji wa madini zilipatiwa leseni kwa ajili ya uchimbaji kwenda chini, lakini kutokana na kutaka kujiongezea maeneo wamelipa wananchi walio jirani nao na kumiliki, lakini hawana hatimiliki na hivyo kutolipa kodi na kuinyima serikali mapato," alisema Lukuvi.

"Kuanzia leo wanaonisikia waanze kulipa kwa hiyari yao kabla sijawaita kama tulivyo fanya leo hii kwa kuwa njia tutakayo itumia ni ya kufedheheshana," alifafanua Lukuvi.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na kumjulia hali mjane wa Baba wa Taifa, Mama Maria Nyerere, anayepatiwa matibabu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# Wakili wa Kisena ahoji upelelezi kutokamilika

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayowakabiliwa wanafamilia wawili, Mkurugenzi wa Kampuni ya Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (Udart), Robert Kisena (46), mke wake Frorencia Mshauri maarufu Frolence Membe (43) na wenzao watatu, umeiomba mahakama kuushinikiza upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi haraka. Kisena na wenzake wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 2.4 kwa kampuni hiyo.

Wakili wa utetezi, Peter Bethuel, alitoa malalamiko hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustine Rwizile katika kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa. Wakili wa Serikali, Esther Martin alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake haujakamilika.

Madai hayo yalimfanya wakili wa utetezi kusimama na kudai kuwa kesi hiyo ni ya muda mrefu na kwamba upande wa Jamhuri unachelewesha kesi makusudi.

"Mheshimiwa Hakimu, mahakama iushinikize upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi ili haki itendeke kwa pande zote mbili," alidai wakili wa utetezi.

Akijibu hoja za utetezi, wakili Martin alidai kuwa washtakiwa wanapaswa wawe wavumilivu na upelelezi utakamilika muda si mrefu. Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Hakimu alisema mahakama yake inapanga kesi hiyo kutajwa tena Juni 24, mwaka huu.

Awali, Wakili wa Serikaki, Glory Mwenda, alidai kuwa washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka manne ya utakatishaji wa fedha, manne ya kutoa nyaraka za uongo, manne ya kughushi, mawili kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kusababisha hasara.

Mbali na Kisena na mkewe, washtakiwa wengine katika hiyo ni Kulwa Kisena (33), Charles Newe (47) na Chen Shi (32).

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa kati ya oktoba 2012 mpaka Mei 31, 2018 washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo.

# Latra kupanga bei elekezi usafiri wa teksi

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Barabara Ardhini (Latra), imesema iko katika hatua za mwisho za kuandaa kanuni za bei elekezi ya usafiri wa teksi nchini.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mkurugenzi wa Udhibiti wa Latra, Johansen Kahatano, alisema kanuni hizo zimeshakamilika zinasubiri kupelekwa kwa wadau kwa ajili ya maoni.

Alisema kanuni hizo zitakamilika kabla ya Julai mwaka huu na kuanza kutumika kabla ya mwaka wa fedha.

"Nyaraka iko tayari kinachofuata ni kuipeleka kwa wadau kwa ajili ya kutoa maoni, wadau wajitokeze kwa wingi kutoa maoni yao kabla ya kusainiwa na kuanza kazi," alisema.

Kwa mujibu wa Kahatano, wamefikia uamuzi wa kuwa na kanuni hizo kutokana na usafiri huo kutokuwa na bei elekezi bali kila mtu kutoza fedha kwa kufikiria na maamuzi ya dereva mwenyewe.

"Malalamiko ya wadau wa usafiri wa teksi yalikuwa mengi sana na serikali inakosa mapato kwenye eneo hilo, tunakuja na kanuni za kusimamia kwa kuwa tumeona ni muhimu kusimamia," alisema.

Kwa mujibu wa Kahatano, ni lazima watumiaji wa magari hayo wajue nauli za maeneo mbalimbali na siyo kukadiria kwa kumwangalia abiria usoni.

Alisema pia katika makadirio hayo serikali inapoteza fedha na kuwa na utaratibu wa bei elekezi itasaidia kuweka usawa, na kwamba lilikuwa hitaji la watumiaji na wenye teksi.

## HABARI KITAIFA



Mama akijaza maji ya kunywa kwenye chupa za plastiki tayari kwa kuyauza katika eneo la Ubungo Stedi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kesi dereva teksi anayedaiwa kumteka MO yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi inayomkabili dereva teksi mkazi wa Tegeta, Mousa Twaleb (46) ya uhujumu uchumi ikiwamo kusaidia kutendeka uhalifu, kutakatisha Sh. milioni nane na kumteka Mohamed Dewji maarufu kama MO.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mahakamani hapo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Deisy Makakala, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na upande wa Jamhuri unaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Juni 25, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi alidai kuwa kati ya Mei Mosi na Oktoba 10, 2018 mahali tofauti jijini Dar es Salaam na jijini Johannesburg nchini Afrika Kusini, kwa makusudi alisaidia utendaji makosa ya jinai kwa nia ya kujipatia fedha.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Oktoba 11, 2018 katika hoteli ya Colloseum iliyopo Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam mshtakiwa akiwa pamoja na wenzake ambao hawapo mahakamani walimteka MO kwa nia ya kumuhifadhi kwa siri.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 249 cha kanuni ya adhabu cha 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2002 kilichotumika kufungua shtaka ya kumteka MO endapo mshtakiwa atakutwa na hatia atahukumiwa kwenda jela kutumika kifungo cha miaka saba.

Ilidaiwa katika shtaka la tatu kuwa, Julai 10, 2018 eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam mshtakiwa alitakatisha Sh. 8,000,000 huku akijua zimetokana na genge la uhalifu wa makosa ya kupanga.

Hakimu alisema mshtakiwa hatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa Juni 25, mwaka huu.

# Korti yatoa hati kukamatwa Wema

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imetoa hati ya kukamatwa Msanii wa Filamu nchini, Wema Sepetu (30), anayekabiliwa na mashtaka ya kuchapisha video ya ngono katika ukurasa wake kwenye mtandao wa Instagram, baada ya kushindwa kufika mahakamani kusikiliza kesi yake.

Amri hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi, Maira Kasonde, baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri, lakini mshtakiwa hakuwapo mahakamani.

Wakili wa Serikali Silvia Mitanto, alidai kuwa kwa sababu mshtakiwa ameshindwa kufika mahakamani, upande wa Jamhuri unaomba hati ya kukamatwa mshtakiwa na tarehe nyingine ya kusikilizwa ushahidi.

Hata hivyo, Wakili wa utetezi, Rubern Semwanza, alidai kuwa mshtakiwa alifika mahakamani kusikiliza kesi yake, lakini alipatwa na ugonjwa wa gafla.

Hakimu alisema mshtakiwa alipaswa kufika mahakamani kujieleza udhuru wake, lakini ameshindwa kufanya hivyo mahakama inatoa hati ya kukamatwa.

Alisema mahakama yake itasikiliza ushahidi wa Jamhuri Julai 4, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, mshtakiwa anadaiwa kuwa Oktoba 15, 2018 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alichapisha video ya ngono na kuisambaza katika mtandao wake wa kijamii wa Instagram.

# Darasa la saba waitwa kujiunga JKT

**Na Beatrice Moses**

VIJANA waliomaliza elimu ya darasa la saba wenye umri wa kuanzia miaka 16 hadi 18 wenye ndoto za kupata mafunzo ya jeshi sasa wamealikwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa kujitolea.

Miongoni mwa sifa zinawaruhusu vijana hao kujiunga na jeshi hilo ni pamoja na kutokuwa na alama ya mchoro wowote ikiwamo tatoo mwilini, asiwe amejihusisha na matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo bangi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kurugenzi ya Habari na Uhusiano Makao Makuu ya JKT mlango huo umefunguliwa na Mkuu wa Jeshi hilo na vijana hao watajiunga na waliohitimu kidato cha nne.

Mwaliko huo unawahusu pia wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali na sanaa waliomaliza darasa la saba au kidato cha nne.

Katika taarifa hiyo vijana hao wanatakiwa kuomba na hatimaye kuchaguliwa kujiunga na mafunzo hayo kupitia ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya wanazoishi.

Imeelezwa kuwa hatua ya kuchagua vijana hao inaanza Juni 2019, hivyo vijana watakaochaguliwa watatakiwa kuripoti Agosti kwenye makambi ya JKT waliyopangiwa.

"Kwa upande wa vijana wa mujibu wa sheria, JKT limetoa orodha ya awamu ya pili ya majina ya vijana waliohitimu elimu ya kidato cha sita 2019 kwa ajili ya kujiunga na mafunzo," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Mkuu huyo wa JKT amewaeleza kuwa katika mafunzo hao vijana watapata fursa ya kujifunza uzalendo, ukakamavu, stadi za kazi na maisha zitakazowasaidia kujiajiri baada ya kuhitimu mafunzo hayo.

Awali mwishoni mwa Mei JKT, ilitangaza majina ya vijana waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2019 iliyowachagua, kutoka shule zote za Tanzania Bara kuhudhuria mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria.

INAENDELEA UK. 8




## RIPOTI MAALUM

# Vitambulisho machinga sokoni mkanganyiko

**Na Romana Mallya**

UGAWAJI wa vitambulisho kwa wajasiriamali (machinga) jijini Dar es Salaam kwenye masoko, umejaa hofu nyingi, ikiwamo viongozi waliokuwa wavigawanye kuvisusia, masoko yakivihofia kuwa vitawaondolea tozo na kuyakosesha mapato.

Lakini si hivyo, kuna baadhi ya viongozi wanaodai vinawahusu wanaozunguka na bidhaa na si walioko sokoni na kuibua maswali kadhaa, kama kipi ni kipi?

Desemba mwaka jana, serikali iliagiza vitambulisho hivyo vitolewe kwa wafanyabiashara na wamachinga wenye mitaji iliyo chini ya Sh. 4,000,000.

Utafiti uliofanywa na Nipashe hivi karibuni katika masoko mbalimbali yakiwamo ya vyakula ulibaini mambo kadhaa kwa mfano, baadhi ya viongozi wanaohusika wanadai kuwa hawavigawi kwa sababu hawahusiki kwani kuna asasi yenye jukumu hilo.

Aidha, viongozi masokoni wanahisi pia kuwa kuanza kuvitoa, vitasababisha kukosa fedha za kugharamia huduma masokoni. Aidha, manispaa zinalaumiwa kuwa hazijalizungumzia suala hilo na kulitolea ufafanuzi.

Khalifan Mandamo, Mwenyekiti wa Soko la Chakula Mwenge, aliiambia gazeti hili kuwa anahofia kuchukua vitambulisho hivyo kwa sababu masoko yameunganishwa na Muungano wa Masoko Mkoa wa Dar es Salaam (Mumada), ambao ndiyo msimamizi.

"Baada ya serikali kutangaza kuhusu vitambulisho hivyo, tuliitwa serikali za mitaa kuzungumzia suala hili, lakini tuliwaeleza kuwa hatujajua kama tutavichukua kwa sababu wasemaji wakuu ni Mumada, wakisema tuchukue tutafanya hivyo," alisema Mandamo.

MKANGANYIKO

Mandamo alieleza kuwa alipofuatilia alibaini kuwa kuna mambo yamejificha kwenye utoaji wa vitambulisho hivyo kwani baadhi ya viongozi wanahisi kuwa vikitolewa wafanyabiashara hawatalipa ushuru, hivyo kutishia kukosa mapato masokoni na halmashauri.



Wafanyabiashara wadogo wakiwa katika shughuli zao katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, bila ya kuwa na vitambulisho vya biashara vilivyotolewa na Rais John Magufuli. **PICHA: JOHN BADI**

Alisema kila siku wafanyabiashara hutozwa Sh. 200 ambazo Sh. 100 hubaki sokoni na nyingine inaingia kwenye mfuko wa Manispaa.

"Tukisema tuvichukue hofu yetu ni hii manispaa itatutambua? Itachukua takataka na kusafisha soko maana huleta gari kwa sababu tunalipa ushuru. Suala hili la vitambulisho tumeshalifikisha Mumada, lakini hadi sasa hawajatupa mrejesho," alisema Mandamo.

**MANISPAA LAWAMANI**

Mwenyekiti wa Muungano wa Masoko Mkoa wa Dar es Salaam (Mumada), Mohamed Mwekya, akizungumzia suala hilo, alisema kinachoendelea kwenye vitambulisho vya wamachinga ni kukosekana ufafanuzi sahihi.

Alisema viongozi wa manispaa hawajawafafanulia viongozi wa masokoni kuhusu utekelezaji wa agizo la serikali la vitambulisho.

"Mumada tunapenda wanachama wetu wote wapate vitambulisho ili waondokane na ushuru wanaotozwa kila siku. Huu ni gharama ikilinganishwa na vitambulisho vya serikali ambavyo wanalipa Sh. 20,000 kwa mwaka mzima," alisema Mwekye.

Aidha, kwa mujibu wa maelezo yake, baadhi ya viongozi wa masoko waliowasiliana naye, aliwaelekeza wachukue vitambulisho, hivyo lakini walio wengi hawajavichukua.

"Viongozi wa masoko ya Kisiwani, Mwananyamala, Magomeni na Kawe wote walinipigia simu nikawaambia Mumada inabariki suala hilo la vitambulisho. Hata masoko mengine yafanye hivyo sisi hatuna kizuizi kwenye suala hilo linaloleta unafuu kwetu," alisisitiza.

Mwekya aliwashutuma baadhi ya viongozi wa manispaa na watendaji wa serikali za mitaa kuwa ndiyo wanaochelewa kutoa ufafanuzi unaoeleweka kuhusu vitambulisho hivyo na kuwakosesha watu wa masokoni kuvipata.

"Wito wangu kwa viongozi na wafanyabiashara masokoni, chukueni vitambulisho hii ni fursa ambayo imetolewa na mkuu wa nchi Rais John Magufuli na itatoa unafuu kwa sababu wapo wanaouza mchicha, lakini gharama ya kulipa ushuru ni kubwa kuliko wanachokiingiza," alisema Mwekye.

**UKWELI UKO WAPI?**

Meneja wa soko la ndizi Mabibo-Urafiki, James Msulya, akiwa sokoni hapo aliiambia Nipashe kwenye mahojiano kuwa, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, aliwatembelea na kuwaambia vitambulisho hivyo haviwahusu walio sokoni.

"Wale ambao hawapo ndani ya masoko, wanaofanya shughuli zao barabarani na maeneo yasiyo rasmi ndiyo wanaohusika na vitambulisho hivyo na siyo sisi," alisema.

"Ofisi yetu tulikuwa na vitambulisho zaidi ya 5,000, lakini baada ya tafsiri hii ya Polepole kuwa hatuhusiki, tumewagawia wengine," alisema Msulya.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa sharti la kutotajwa majina yao gazetini, walisema kuwa, baada ya kufuatilia suala hilo kwenye uongozi waliambiwa soko la Mabibo halihusiki na vitambulisho hivyo.

"Tumeuliza viongozi wamesema sisi wa masokoni tunaendelea na utaratibu wa utozaji wa ushuru. Tunatamani na sisi tulipe Sh. 20,000 tupate vitambulisho ili tuachane na tozo hizi ambazo kwa mwaka ni zaidi ya Sh.100,000 tunazolipia," alisema mmoja wao.

Mmoja wa wauza matunda sokoni hapo, alisema hofu iliyopo masokoni ni kwamba watakapowapa vitambulisho hivyo manispaa zitakosa mapato yao.

Mwenyekiti wa Soko la Shekilango, David Mrisho, kwa upande wake alisema alifuatilia vitambulisho kwa Ofisa Mtendaji Kata ya Ubungo, Isiaka Waziri, aliyemweleza kuwa haviwahusu wafanyabiashara wa masokoni," alisema.

Mrisho alisema mtendaji alimwambia hawahusiki na vitambulisho hivyo kwa sababu kuna utaratibu wa kulipa tozo ambazo kwa siku ni Sh. 200, kwa mwezi Sh. 6,000 na kwa mwaka 72,000.

"Kama kiongozi sikuamini. Nilichokiona hapa ni kwamba Rais Magufuli alivyoingilia suala la vitambulisho, kuna baadhi ya halmashauri zinaona kama vile wameporwa mapato, mfano mimi ni fundi cherehani ninatakiwa kuwa na leseni kwa hiyo nikipewa kitambulisho, hizo tozo sitatoa," alisema Mrisho.

Alisema sokoni Shekilango kuna wafanyabiashara wadogo wasiopungua 500, wakiwamo washonaji, wauza kuku, mboga mboga na wachinjaji.

Aidha, pamoja na majibu hayo

INAENDELEA UK.8


Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku

215227501



# Michango ujenzi vyoo yazua jambo bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Nkasi, Ally Keissy (CCM), ameliomba Bunge kurejesha fedha zilizochangwa na wabunge kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya mfano kila jimbo nchini kwa madai ya kwamba mradi huo umekwama.

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jijini Dodoma jana, mbunge huyo alisimama na kutumia Kanuni ya 47 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, akitaka chombo hicho cha kutunga sheria kiahirishe shughuli zake za jana na kujadili hoja hiyo ya dharura.

Katika kujenga hoja yake, Keissy alihoji kwa nini hakuna mrejesho uliotolewa kwa wabunge kuhusu fedha walizochanga wakishirikiana na wadau wengine kufanikisha ujenzi wa vyoo bora kwenye majimbo yote nchini.

Alisema inasikitisha kuona tangu jambo hilo lianze kutekelezwa kwa kukusanya fedha kwa wabunge na wadau wengine wa maendeleo hadi jana hakuna mrejesho uliotolewa bungeni maendeleo ya ujenzi huo.

Keissy aibainisha kuwa hata majimboni vyoo hivyo bado havijajengwa, hivyo kulitaka Bunge kurejesha fedha kwa wabunge na wadau wengine waliochanga kama suala hilo limeshindikana.

"Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu zaidi ya mwaka tangu tuanze kutoa michango kwa ajili ya kupata pesa za ujenzi wa vyoo bora vya mfano katika majimbo yetu, hatujapewa mrejesho hili suala limefikia wapi, wala kiasi kilichokusanywa, nimekuwa nikiuliza, ila sipewi majibu, sasa basi kama imeshindikana turudishiwe pesa zetu tutajenga wenyewe," Keissy alisema.

Baada ya mbunge huyo kutoa hoja, wabunge wengi walisimama kumuunga mkono, lakini Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alisema hoja hiyo haikuwa ya dharura, hivyo hakukuwa na uhalali wa kujadiliwa na Bunge kulingana na masharti ya Kanuni za 47 na 48 za Kanuni za Kununi za Bunge.

Hata hivyo, Dk. Tulia alisema suala hilo linasimamiwa na Spika na "liko mikono salama na hata

INAENDELEA UK. 8

## Kamishna akiri changamoto uhifadhi Ngorongoro

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), imesema kuna kitendawili kikubwa ndani hifadhi hiyo kati ya utalii na maendeleo ya binadamu kutokana ongezeko la magonjwa, ujangili na migogoro baina ya wanyama na binadamu.

Aidha, idadi ya watu na mifugo inayokufa kutokana na ugonjwa wa kimeta, wanyama kuzaliana kizazi hicho hicho inaongezeka, huku mapito ya wanyama yakiendelea kwisha na ifikapo mwaka 2030 hakutakuwa na mapito yanayounganisha hifadhi moja hadi nyingine.

Hayo yalibainishwa jana na Kamishana wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Freddy Manongi, alipokuwa akiwasilisha mada kwenye mkutano wa waandishi wa habari za uhifadhi wa Tanzania na Thailand, walio kwenye programu maalum iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (Jet) kwa ufadhili wa Shirika la Misaada ya Maendeleo la Merekani (Usaid).

Alisema hakuna idadi ya vifo vya binadamu lakini ni wastani wa watu

INAENDELEA UK. 8


TASAF
TANZANIA SOCIAL ACTION FUND
MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

**TAARIFA KWA UMMA** // **PUBLIC NOTICE**

**NAMBA ZA KUPIGA BILA MALIPO**

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF unapenda kuwajulisha walengwa wake, wadau na wananchi wote kwamba kitengo cha huduma kwa wateja kina namba za kupiga bila malipo yoyote

Namba hizi ni **0800 110058 na 0800 110057** ambazo ziko hewani siku za Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa **2:00 asubuhi mpaka saa 2:00 usiku.**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
**Jengo la PSPF, Ghorofa ya nne**
**Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete**
**S.L.P 2719**
**DODOMA**

**Simu : + 255 26 2963866**
**Nukushi : +255 26 2963871**
**Barua pepe : info@tasaf.go.tz**
**Tovuti : www.tasaf.go.tz**

**CALL CENTRE TOLL FREE NUMBERS**

Tanzania Social Action Fund (TASAF) wishes to inform its beneficiaries, stakeholders and the public that its call centre has toll free numbers

**0800 110058 and 0800 110057**

These numbers are reachable on weekdays (Monday to Friday) from **8:00am to 8:00pm**

**Executive Director**
**Tanzania Social Action Fund (TASAF)**
**4th Floor, PSPF building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete rd**
**P.O BOX 2719**
**DODOMA**

**Telephone : + 255 26 2963866**
**Fax : +255 26 2963871**
**Email : info@tasaf.go.tz**
**Website : www.tasaf.go.tz**

215268502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Iwe bajeti jumuishi, kuondoa umaskini

**KESHO** Watanzania wanangoja kwa hamu kusikia bajeti yao ambayo ni andiko la serikali linaloonyesha na kuainisha maamuzi ya vipaumbele vya maendeleo ya nchi kwa mwaka 2019/2020.

Ni jambo jema kuwa bajeti itazungumzia maendeleo ya nchi kwenye uchumi, jamii, miundombinu na kwa ujumla kufikia malengo na matarajio ya kuwa na Tanzania ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo 2025.

Tunapenda kusisitiza kuwa ni vyema kueleza kuwa ni muhimu bajeti isizungumzie maendeleo kiujumla kwenye uchumi na kwenye sekta za kipaumbele bali iwe jumuishi ikimfikia kila mmoja.

Bajeti ya jumla faida zake hubakia kwa maeneo kadhaa bila kugusa makundi maalumu ya wanyonge wakiwamo wanaoishi pembezoni, ambao si rahisi wakanufaika moja kwa moja na vipaumbele vinavyogusiwa.

Ndiyo maana tunahimiza kuwapo bajeti jumuishi na shirikishi inayowagusa masikini hasa wanawake vijijini, yatima, wajane, wazee na kaya maskini zisizo na msaada ambazo mara nyingi haziwezi kunufaika moja kwa moja na matokeo ya bajeti ya taifa.

Bajeti jumuishi hiyo tunayotarajia ni ile inayowapa kipaumbele mabinti wa kaya maskini ambao wazazi na walezi wao, hawana kipato cha kuwawezesha kununua huduma muhimu kama taulo za wanawake za kujisitiri kila mwezi.

Kukosekana fedha za kununua huduma muhimu kunawalazimisha wasichana kukosa masomo kila mwezi angalau kwa siku tano kwa vile hawawezi kwenda shule kwani hawana kitu cha kujisitiri wakati wa hedhi.

Bajeti hii tunatarajia haitawasahau watu maskini kama hao kwa kuondoa kodi ya pedi na kutoa ruzuku ya kununulia taulo hizo shuleni, ili kuwawezesha mabinti hao kusoma.

Pamoja na vipaumbele vya jumla tunategemea kuona bajeti ikiwakumbatia pia wenye mahitaji maalumu kama wanawake na mabinti kwa kuwekeza zaidi kwenye elimu kwa wote.

Hii itawawezesha wanyonge kusoma na kubadili maisha yao kupitia elimu.

Kadhalika ni tegemeo letu kuwa bajeti ya serikali itaelekeze nguvu kwenye elimu, itakuwa na kipaumbele kwenye kuhakikisha upatikanaji wa madarasa ya kutosha, mabweni, maji na vyoo shuleni iwe msingi au sekondari kwa ajili ya mahitaji mbalimbali.

Hayo ni pamoja na mahitaji ya wasichana na wanaoishi na ulemavu wa aina mbalimbali.

Aidha, tunatarajia bajeti itakayofikisha huduma muhimu, wataalamu na vifaa tiba hospitalini ili kupunguza vifo vya wanawake na watoto.

Ikumbukwe kuwa idadi ya wanawake wanaokufa katika matatizo yanayohusiana na uzazi sasa ni takribani 556 suala ambalo linaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi hatarishi kwa wanawake wajawazito na wazazi.

Masuala ya kufikisha huduma muhimu kwa wananchi kama maji nayo ni muhimu yakaonekana kwenye bajeti, ili kulinda afya za mamilioni ambao huathirika kutokana na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa maji safi na salama mijini na vijijini.

Bajeti hii jumuishi tunatarajia iwakumbuke watu wanaoishi na magonjwa sugu kama VVU na Ukimwi hasa wa familia maskini ambazo zinahitaji mkono wa serikali kuzisaidia kumudu maisha yao.

Mambo ni mengi, lakini bajeti inayoyakumbuka makundi ya wanyonge na kuinua maisha yake ni muhimu kwa kuwa ni vigumu kupunguza pengo la maskini na matajiri kama serikali haitakuwa na bajeti inayobadilisha maisha ya kila mwananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Jamii iamuke, kuzembea elimu ni kukumbatia kipindupindu

**UGONJWA** wa kipindupindu jijini Dar es Salaam bado umetamalaki kwa wiki kadhaa sasa na watu waliokumbwa na ugonjwa huo wameongezeka kutoka 34 mwishoni mwa Mei hadi kufikia 55 sasa, huku watu watatu wakiwa wamefariki dunia.

Hiyo ni kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu ambaye amekaririwa na vyombo vya habari hivi karibuni akiwataka watu kuacha kutiririsha majitaka mitaani.

Inaelezwa na wataalamu wa afya kuwa kipindupindu ni miongoni mwa magonjwa ambayo husababishwa na aina ya bakteria aitwaye Vibrio cholerae, na kwamba ugonjwa huo ni wa kuambukizwa.

Njia kubwa ya kuambukiza inatajwa na wataalamu kuwa ni kupitia kinyesi, kwamba viini kutoka kwa wagonjwa wenye kipindupindu huenezwa kwenda kwa watu wengine kwa njia hiyo.

Dalili za ugonjwa huo ni kuharisha kinyesi kilicho na majimaji, mwili kushindwa kutumia maji na chakula na kumfanya mgonjwa kudhoofika haraka, kwa sababu ya kukosa maji mwilini.

Dalili zingine ni mgonjwa kuhisi kiu kingi na uchovu mwingi, na kushindwa kutulia, ngozi yake ya nje na ndani kunyauka, macho kuingia ndani huku akihisi kichefuchefu na kiharusi kisicho cha kawaida.

Wataalamu wanasema njia ya kuepukana na kipindupindu ni kunawa mikono kwa sabuni, viganja, upande wa nyuma wa mkono, katikati ya vidole na kucha kwa sekunde kadhaa baada ya kutoka msalani na kabla ya kula.

Si hayo tu, wanaishauri mara kwa mara jamii kuacha kutiririsha majitaka mitaani, kutumia vyoo safi na kuchemsha maji ya kunywa, lengo likiwa ni kuepukana na ugonjwa huo. Pamoja na hayo bado baadhi ya watu hawazingatii hayo.

Kuzembea elimu hiyo ni kuendelea kuhatarisha maisha, hivyo ni muhimu jamii ikabadilika na kuzingatia kile ambacho wataalamu wa afya wanaelekeza.

Muungwana anashangazwa na hatua katika baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam ya wakazi wake kutiririsha majitaka mitaani kipindi cha mvua na hata wakati wa kiangazi.

Mtindo wa kuvizia mvua na kuelekeza uchafu wa vyooni kwenye mkondo wa maji ya mvua ni jambo linalowaweka wakazi wa jiji katika hatari kubwa ya magonjwa ya mlipuko.

Ieleweke kuwa mazoea haya yanawapoteza, hivyo ni vyema kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa afya.

Usafi ni adui mkubwa wa kipindupindu, hivyo jamii ikizingatia usafi ni wazi kwamba ugonjwa huo utakoma, lakini kuendelea kukumbatia uchafu ni sawa na kuukaribisha.

Kwa sasa kipindupindu kipo jijini Dar es Salaam na tayari serikali imeshatoa onyo la kuwataka wakazi wa jiji kuzingatia kanuni za afya ili kuepuka ugonjwa huo ambao chanzo chake ni uchafu.

Muungwana anabainisha kwamba kipindupindu ni ugonjwa unaoweza kutoweka iwapo kila mmoja atazingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

Oktoba mwaka 2017, ulifanyika mkutano wa kutokomeza ugonjwa wa kipindupindu ifikapo 2030, ambao ulijumuisha maofisa kutoka nchi mbalimbali duniani. Mkutano huo ulifanyika nchini Ufaransa.

Katika mkutano huo, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilieleza matumaini yake ya kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya ugonjwa wa kipundupindu, pamoja na idadi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 90 ifikapo 2030.

Hiyo ni kwa sababu ni aibu kuwa na ugonjwa huo katika karne hii.

Sasa wakati WHO ikifanya juhudi hizo, jamii nayo iwe tayari kumkabili adui huyo maradhi kwa kukubali elimu inayotolewa na wataalamu wa afya, vinginevyo adui huyo atakuwa anaondoka na kurudi kama, ambavyo imekuwa ikitokea nchini.

Ugonjwa huo ambao katika karne ya 21 umeelezwa kama 'aibu kubwa kwa dunia,' unaua karibu watu 100,000 kila mwaka.

# MJADALA/BARUA

## *Tuwe wastaarabu tuwapo kwenye usafiri wa umma*

*Mhariri*

*Habari za majukumu!*

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

**Deogratius Munishi- Mbagala**




# Viongozi jifunzeni kwenye darasa hili

**Na Mwandishi Wetu**

NI dhahiri kuwa watendaji wa serikali wamesikia mara kadhaa kile wanachotakiwa kufanya kupitia darasa linalotolewa na Rais John Magufuli, kila mara anapofanya uteuzi na kuapisha watendaji wapya.

Rais mara nyingi anaeleza sababu za kuwatimua wanaotumbuliwa na kutoa maagizo mapya ya matarajio yake kwa wale anaowateua kushika nyadhifa zilizofanyiwa mabadiliko.

Mathalani Jumatatu wiki hii, Rais alipowaapisha Waziri Innocent Bashungwa kuongoza Wizara ya Viwanda na Biashara na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Dk. Edwin Mhende, anayechukua nafasi ya Charles Kicheere, aliyeondolewa kwenye wadhifa huo.Nizungumzie zaidi eneo la TRA ambako Rais alisema amemuondoa Kicheere baada ya kushindwa kufanyakazi kikamilifu ya kukusanya mapato na kufuatilia majukumu na maagizo anayompatia.

Jambo linalomtofautisha Rais Magufuli na viongozi wengine ni uwazi na kila mara anawaeleza Watanzania kinachomuudhi hadi kufikia hatua ya kumtumbua mteule wake kutoka kwenye idara au eneo alilokuwa akiliongoza.

Hivyo hakuna swali linalobakia kwanini fulani kaondolewa kazini pale hatua zinapochukuliwa dhidi yake.

Ni kwa msingi huo Nipashe inapenda kuibua mjadala kuhusu mazoea ya viongozi kutowajibika kuanzia pale wanapopewa taarifa iwe kutoka kwa wakuu wao, raia au taasisi na wakati mwingine kuendelea na hali mbaya wanayoiona kwenye eneo wanaloliongoza bila kuchukua hatua.

Wanabakia na fikra mgando kwa muda mrefu licha ya kuwa wanapewa bajeti, vitendea kazi na kila wanachohitaji ili kutimiza lengo hilo la kuwajibika.

Kwa mfano Rais alieleza kuwa mara kadhaa alikuwa anamweleza Kamishna Mkuu Kicheere kuwa ameshindwa kuongeza mapato ambayo yalikuwa Sh. trilioni 1.3 kiwango kilichokusanywa na Waziri wa Fedha, Dk. Phillip Mpango, miaka minne iliyopita, ambaye alikuwa akiongoza TRA kabla ya uteuzi wa kuwa waziri.

Anaeleza kuwa kuna malalamiko mengi ya wafanyabiashara aliyoyapokea na kumtumia Kicheere wakati mwingine hata usiku wa manane lakini hakuyafanyia kazi.

Rais anachosema ni kweli kwani kuna viongozi wengi ambao licha ya kupewa jukumu, vitendea kazi, fedha na hata posho ya kazi hawawajibiki kikamilifu kuondoa kero na kuleta hali bora.

Katika hali ya kawaida watu wanapoona uongozi mpya wanatarajia mabadiliko, lakini kwa kiasi kikubwa sicho kinachoonekana

Kwa mfano, wananchi wanalalamikia ukosefu ama kutoridhishwa na huduma ambazo wanazichangia kupitia kodi kwenye maeneo ya biashara hasa masokoni, lakini hakuna kinachofanyika.

Eneo mojawapo linalowakera watu ni kulipia huduma kwenye vituo vya mabasi katika kila stendi za mikoani wanazopita.

Ndani ya vituo hivyo hakuna vyoo, maji wala huduma za msingi za kuwaridhisha wasafiri.

Mfano wa sehemu ambayo inakera ni kituo cha mabasi ya masafa marefu cha Ubungo jijini Dar es Salaam ambapo kila siku anayeingia analipia, lakini hakuna hata choo safi cha kulipia, mgahawa wa kisasa, viti vya kupumzika, wala pipa la kutupia taka.

Umma unajiuliza viongozi wanafanyakazi gani hata kushindwa kujenga choo safi ndani ya kituo hicho? Uongozi wa Jiji la Dar es Salaam, kwanini usichukue hatua kuwawajibisha wanaosimamia?

Si hivyo tu kwenye masoko ndiko hali ni mbaya zaidi. Mengi hayana vyoo safi na salama, maji ya kunywa na hata ya kunawa na kusafisha bidhaa.

Hata kama kuna vyoo ni vichafu vichafu na havifai kutumika. Swali ni lile lile mabwana afya, waganga wakuu na mamlaka zinazosimamia usalama wa chakula zinafanya nini?Katika baadhi ya maeneo wananchi wanalalamikia mambo maovu kama huduma mbovu hospitalini ikiwamo kudaiwa rushwa na kulazimishwa kulipa fedha nyingi ili kufanyiwa upasuaji.

Mfano ni hospitali ya Mkoa wa Manyara ya Babati- Mrara, ambako Mkuu wa Mkoa wa Manyara Alexander Mnyeti, alimwagiza Mganga Mkuu kuwahamishia vijijini waganga wala rushwa na wanaoongeza gharama za huduma.

Hatua hiyo inakuja baada ya wananchi kulalamikia kutozwa Sh. 250,000 kwa upasuaji unaotakiwa kufanyika kwa Sh. 100,000.

Licha ya maelekezo hayo viongozi hao watahamishwa? Kuadhibiwa baada ya kuchunguzwa?

Wananchi wanalalamika kwani wanafahamu kuwa kuna bei elekezi kwenye huduma hiyo.

Hata hivyo, waganga wakuu wa mikoa na wilaya hawachukui hatua licha ya kupewa taarifa na wananchi.

Mnangoja nini viongozi wakati mnapewa mafuta, posho, wataalamu na malipo halali ili kutimiza wajibu wenu?

Si hospitalini tu, pia yapo matatizo ya kunyimwa haki, kesi kucheleweshwa, kudhulumiwa mahakamani nayo ni changamoto ambazo wananchi wanataka zitatuliwe.

Pengine ni wakati wa kuanza utaratibu wa 'name and shame' ambao utawataja viongozi wasiowajibika na kuwaaibisha hadharani ili kuongeza uwajibikaji zaidi.

Haipendezi kusikia kila mara, viongozi wa mashirika na taasisi za umma wakiwahimiza wananchi kutoa taarifa za uhalifu ama za uhujumu maendeleo lakini zinapofikishwa hazifanyiwi kazi.

Wenye dhamana mnasubiri kuanza kutajwa na kuaibishwa? Jifunzeni kupitia somo linalotolewa na Rais kila wakati anapowawajibisha viongozi wasiotimiza wajibu.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Michango ujenzi vyoo yazua jambo bungeni

INATOKA UK. 5

fedha zilizochangwa ziko salama" na wakati utakapofika wabunge watapewa taarifa.

Alisema fedha zilizotolewa na wadau nazo ziko salama huku akiwataka wale ambao bado hawajakamilisha ahadi zao, wafanye hivyo ili kuhakikisha wanapata fedha na kujenga vyoo bora vya mfano.

Juni 22, mwaka jana, Bunge lilizindua kampeni ya ujenzi wa vyoo vya mfano shuleni, huku Spika Job Ndugai akibainisha kuwa hali ya vyoo katika shule nyingi nchini ni mbaya.

Uzinduzi huo ulifanyika kwenye Viwanja vya Bunge jijini Dodoma, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiwa mgeni rasmi.

Katika hafla ya uzinduzi huo, Spika Ndugai alisema wabunge wote walikuwa wameshachangia Sh. milioni 81 huku wabunge wa majimbo wakichanga Sh. milioni 528 (kila jimbo Sh. milioni mbili kwa majimbo yote nchini).

Alisema hali ya vyoo katika shule nyingi zinazomilikiwa na serikalini ni mbaya na inahatarisha maisha ya wanafunzi.

Spika Ndugai alibainisha kuwa kuna ongezeko kubwa la wanafunzi katika shule nyingi za umma nchini kutokana na uamuzi wa serikali ya awamu ya tano wa kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari.

Ndugai alisema idadi ya wanafunzi imeongezeka lakini miundombinu ya kujifunzia na kufundishia vikiwamo vyoo bado haijaongezwa na kuboreshwa.

Alisema ni kutokana na changamoto hiyo, Bunge limeamua kuanzisha kampeni hiyo ya kukusanya fedha kwa ajili ya kujenga vyoo vya mfano katika kila jimbo nchini ili wadau wengine watakaojitokeza wavijenge kunusuru afya za wanafunzi.

Alisema zipo shule ambazo vina vyoo hatarishi kwa afya za watumiaji na kwamba katika shule nyingi vyoo vilivyopo havikidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu na watoto wa kike.

Alisema vyoo vya mfano vitajengwa kwa kuzingatia makundi matatu ya watu wenye mahitaji maalum, watoto wa kike na vya watoto wa kiume.

"Fedha tulizopata ni za kuanzia na tunaendelea kuchangia kwa kadri tutakavyoelekezwa na kamati yetu," alisema.

Kiongozi huyo wa Bunge alisema jumla ya Sh. bilioni 3.5 zinahitajika kwa ajili ya kujenga vyoo vya mfano katika majimbo yote 264 nchini.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo siku hiyo, jumla ya Sh. bilioni 1.45 zilikusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwamo wizara, wabunge, taasisi za umma na kampuni wa watu binafsi.

# Darasa la saba waitwa kujiunga JKT

INATOKA UK. 3

Jehi hilo lilitangaza makambi watakayokwenda kupatiwa mafunzo hayo kwa muda wa miezi mitatu na wanatakiwa kuripoti makambini kuanzia tarehe 01 hadi 07 Juni 2019.

Kambi za JKT walizopangiwa vijana hao ni pamoja na Rwamkoma-Mara, JKT Msange-Tabora, JKT Ruvu-Pwani, JKT Mpwapwa na JKT Makutupora-Dodoma.

Nyingine ni JKT Mafinga-Iringa, JKT Mlale-Ruvuma, JKT Mgambo na JKT Maramba-Tanga, JKT Makuyuni-Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa, na JKT Mtabila –Kigoma, JKT Itaka-Songwe, JKT Lua na JKT Milundikwa-Rukwa, JKT Nachingwea-Lindi.

Katika toleo la jana, ukurasa wa kwanza ulikuwa na kichwa cha habari 'Darasa la saba waitwa JKT'. Hata hivyo, habari hiyo haikuonekana katika Uk.3 kama tulivyoonyesha. Tunaomba radhi kwa usumbufu - **Mhariri**



Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula (wa nne kulia) na Kamishna wa Tume ya Madini, Prof. Abdulkarim Mruma (wa tatu kushoto), wakiangalia na kukagua sampuli za miamba zilizohifadhiwa kwenye mifuko kutoka kwenye mwamba wa madini ya dhahabu kutoka mgodi wa Namungo, wilayani Ruangwa mkoani Lindi juzi. **PICHA: WM**

# Kamishna akiri changamoto uhifadhi Ngorongoro

INATOKA UK. 5

wawili hadi watatu wanafariki dunia kila mwezi kutokana na kuliwa na wanyama au ugonjwa wa kimeta na kichaa cha mbwa.

Kwa mujibu wa Manongi, hivi karibuni walifanya sensa ya watu ndani ya eneo la Ngorongoro na kubaini wameongezeka kutoka 800 hadi 95,000 toka mwaka 1959, huku mifugo ikiongezeka kila siku.

Aidha, alisema hadi Desemba, mwaka jana, zaidi ya ng'ombe 7,500 walikufa kwa kimeta na ukame, mifugo na binadamu ndani ya Ngorongoro wakiongezeka kwa kasi, ikiwamo shughuli za binadamu ambazo haziruhusiwi.

"Haikubaliki mtu kufariki dunia kutokana na magonjwa ya wanyamapori na wala si lengo la uhifadhi na halikubaliki. Lakini hiyo inatokana na ongezeko la watu na mifugo ikiwamo shughuli za binadamu, aina ya nyumba zinazojengwa na sasa ni za kudumu na shughuli za kilimo ambazo hazikubaliki," alisema.

Alisema athari za mwingiliano zinaonekana kwa binadamu kuwa na wanyama na mifugo kuuawa, chakula cha mifugo na wanyama kimepungua na sasa kuna magugu ndani ya hifadhi jambo linalowafanya wananchi wawe maskini zaidi kwa kuwa wanategemea mifugo kwa ajili ya maisha yao ya kila siku.

"Mamlaka inapata fedha nyingi sana kutokana na utalii lakini hazifanani na maisha ya watu wa eneo husika, tunapata watalii 600,000 kwa mwaka na tulipata zaidi ya Sh. bilioni 120," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanajiuliza wafanyeje na hali inakuwa ngumu kwamba wanyamapori wanaweza kuishi na binadamu, na kwamba wanapata fedha nyingi kutokana na utalii, lakini maisha ya binadamu yanazodi kuwa magumu, jambo ambalo linawafikirisha kufanya mabadiliko. Alisema uchunguzi umebaini kuwa matukio ya uhalifu NCA yana uhusiano moja kwa moja na wananchi wanaoishi ndani ya Ngorongoro, kwa kuwa kati ya waliokamatwa walikuwa ni wanajamii. Alisema mwaka jana watu nane walikamatwa na nyara za faru ambaye aliuawa kati yake watano ni wanajamii wa Ngorongoro, watatu kutoka nje ya eneo hilo, na kwamba iliuzwa Vietnam.

# Vitambulisho machinga sokoni mkanganyiko

INATOKA UK. 4

ya mtendaji huyo, wameona katika Wilaya ya Arumeru, Mkuu wa Wilaya hiyo, Jerry Muro, akipita masokoni kuuza vitambulisho.

"Nimesikia hata Wilaya ya Kinondoni, wenzetu Magomeni wanavitoa, iweje kwa Wilaya ya Ubungo?

Juliana Kitenge, anayeuza mboga aliomba utoaji wa vitambulisho uwafikie sokoni hapo kwa sababu biashara wanazofanya zipo chini ya mtaji wa milioni nne.

**VIONGOZI WANENA**

Wakati wafanyabiashara wakitoa madai yao, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, aliliambia gazeti hili kuwa wilaya yake imeshagawa vitambulisho 35,000 kwa wamachinga wakiwamo wa masokoni na bado uhitaji upo.

"Wilaya ya Kinondoni kupitia watendaji wangu tumeshagawa vitambulisho 35,000 wakiwamo wafanyabiashara masokoni. Vimefika Tegeta Nyuki tumetoa zaidi ya vitambulisho 400, Mwenge wamepewa zaidi ya vitambulisho 3,000 na maeneo mengine ya wamachinga," alisema.

Kadhalika, Chongolo alisema licha ya kugawa vitambulisho hivyo kuna uhitaji na kila anayefika ofisini anavitaka, hivyo wamekuwa na utaratibu wa kuazima kwa wenzao ambao bado wanavyo.

Ofisa Masoko Manispaa ya Ilala, Frank Kibika, alisema baadhi ya watu masokoni hawajachukua vitambulisho hivyo na kwamba wanaendelea kutozwa ushuru wa Sh. 200.

"Kuna ambao wamechukua na wengine labda kwa kuona mitaji yao ni juu ya Sh. 4,000,000 hawajachukua, hawa tunawatoza ushuru kama kawaida kwa ajili ya kuendesha masoko. Utaratibu wa vitambulisho ni kwamba mtu akiwa nacho anatakiwa akivae ili atambulike, wale wasiokuwa navyo tunawatoza," alisema Kibiki.

Alitaja changamoto ya baadhi ya watu wenye maduka kuchukua vitambulisho wakati mitaji yao ni juu ya milioni nne, hivyo wamepawa elimu ili wakate leseni.

Agizo la kutoa vitambulisho lililotolewa na Rais mwaka jana katika mkutano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa kujadili namna ya kuboresha mazingira ya ukusanyaji mapato. Aidha, aligawa vitambulisho 670,000 kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo.

Rais Magufuli alinukuliwa akisema kuwa mfanyabiashara yeyote ambaye mapato yake kwa mwaka hayazidi Sh. 4,000,000 atakayekuwa na kitambulisho hicho asibughudhiwe.

Baada ya maagizo hayo kila mkoa ulikabidhiwa vitambulisho ili kutekeleza agizo hilo.

# Halima Mdee atoka hospitali

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Kawe, Halima Mdee, aliyekuwa amelazwa katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam ameruhusiwa kutoka katika hospitali hiyo baada ya kupata nafuu. Akizungumza na gazeti hili, Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya, ambaye ni rafiki yake wa karibu, alisema mbunge huyo alilazwa kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji. "Ameruhusiwa tangu jana, ingawa bado yupo chini ya uangalizi maalum, na atatakiwa kurudi hospitalini keshokutwa," Bulaya alisema.

Mdee alikwenda katika hospitali hiyo tangu Juni 6 mwaka huu na baadaye kufanyiwa upasuaji baada ya kukutwa na uvimbe tumboni.

Mdee kwa sasa anatumikia adhabu ya kutohudhuria mikutano mitatu ya Bunge, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kuunga mkono kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kuwa Bunge ni dhaifu.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Christon iliyopo wilayani Kisarawe mkoani Pwani, August Minja (kushoto), akimpa taarifa ya maendeleo ya shule yake, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu alipotembelea shule hiyo hivi karibuni alipokwenda kuwasha umeme wa REA kwenye Kijiji cha Gumba ambacho kipo kilomita tatu kutoka ilipo shule hiyo. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# Waziri aagiza shule kuunganishiwa umeme

**Na Mwandishi Wetu,**
KISARAWE

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) mkoani Pwani kuhakikisha mapema iwezekanavyo Shule ya Sekondari ya Bweni ya Christon iliyopo wilayani Kisarawe inaunganishwa na gridi ya umeme wa taifa ili kuchochea ukuaji wa taaluma na maendeleo ya shule.

Akizungumza baada ya kuwasha umeme katika Kijiji cha Gumba ambapo nyumba 28 ziliunganishiwa umeme kisha kutembelea Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Christon, Mgalu aliiagiza Tanesco kuharakisha mchakato wa kuufikisha umeme kwenye shule hiyo ambayo ipo katika Kijiji cha Msimbu.

"Nimewasha umeme katika kijiji cha Gumba ...kilometa tatu tu kufika kijiji cha Msimbu eneo ambalo shule hii ya sekondari ipo na inafanya vizuri sana kitaaluma katika Wilaya ya Kisarawe," alisema.

Alisema huduma ya kitaaluma na miradi ya shule hiyo itahitaji kuwapo kwa umeme wa uhakika badala ya kutumia jenereta ambalo uendeshaji wake ni mgumu sana kwa taasisi hiyo.

"Wakati sasa umefika kwa Tanesco kuwa na vipaumbele kwa mfano nimeambiwa shule inatumia zaidi ya Sh. 100,000 kwa ajili ya mafuta ya kuendeshea jenereta kwa siku kutokana na matumizi yake," alisema.

Mgalu aliipongeza Shule ya Sekondari ya Christon kwa matokeo mazuri ya

kitaaluma kwa kuwa imekuwa ikiongoza katika Wilaya ya Kisarawe katika mitihani ya kitaifa. "Miradi hii ya kilimo cha mbogamboga, ufugaji wa samaki, sungura, ng'ombe na sungura ni muhimu sana kwa shule ya bweni kwani husaidia kuwapa watoto, mbali ya lishe pia ni sehemu ya mafunzo na elimu ya ziada," alisisitiza.

Akiwepo shuleni hapo, alitembelea miradi mbalimbali ikiwamo eneo lililojengwa 'Biogas', mradi wa kuku, sungura na ng'ombe.

Mkuu wa Shule, August Minja, alisema kuwapo kwa umeme wa uhakika shuleni hapo utachochea maendeleo ya kitaaluma.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutujali na kuwa karibu nasi. Umeme umekuwa kilimo chetu kikubwa sana," alisema na kuongeza kuwa ujio wa Naibu Waziri wa Nishati shuleni hapo ni habari njema.

# Dar wafagilia katazo mifuko ya plastiki

**Na Enock Charles**

SIKU kadhaa baada ya kuanza kwa utekelezaji wa katazo la utumiaji, usambazaji na utengenezaji wa mifuko ya plastiki, maisha yamerudi katika hali ya kawaida, huku mifuko mbadala ikichukua nafasi.

Wakazi kadhaa wa Jiji la Dar es Salaam wamefunguka kuelekeza kwao kufurahishwa na utekelezaji wa katazo hilo.

Katika mahojiano na wadau mbalimbali katika jiji hilo wakiwamo wasambazaji na watumiaji wa mifuko mbadala wameeleza kufurahishwa na utekelezaji huo uliofanyika bila matumizi ya nguvu.

Mfanyabiashara wa mifuko mbadala awali alikuwa muuzaji wa mifuko ya plastiki eneo la Yombo Vituka, Yunus Mwakikuti, alipongeza hatua iliyochukuliwa na serikali na kuwa hali imerejea vizuri na uhitaji wa mifuko hiyo katika kubebea bidhaa ni wa uhakika. "Naipongeza serikali kwa uamuzi huo mzuri kwa kulinda mazingira na afya za watu wake. Napongeza pia mamlaka zilizoshiriki kuhakikisha katazo hili linatekelezeka pasipo kutumia nguvu zaidi ya kuelimisha watu juu ya athari za moja kwa moja zinazoonekana katika jamii kutokana na matumizi ya mifuko ya plastiki," alisema Mwakikuti.

Zakia Abdalah, mfanyabiashara soko la Mbagala Rangi Tatu, alisema katazo la serikali limekuwa na maana kubwa kimazingira kwani mifuko ya plastiki ingeachwa kutumika ingeleta madhara makubwa kwa mazingira na afya.

"Siku ya kwanza ilikuwa na usumbufu mkubwa kutokana na mazoea ya watu kutumia mifuko ya plastiki, lakini kwa sasa mambo yanakwenda vizuri tumeshazoea kutumia mifuko mbadala kutokana na uimara wake na unaweza kuitumia kwa muda mrefu kulingana na matumizi yako tofauti na mifuko ya plastiki," alisema Abdalah.

Alisema mamlaka husika ziendelee kutoa elimu kuhakikisha wanawajengea uwezo wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faida zake kwa jamii iliyopo sasa na vizazi vijavyo kuhusu faida ya utunzaji wa mazingira.

Akizungumza hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifidhi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema baraza lake litaendelea kutoa elimu na kuhakikisha ufuatiliaji na usimamizi wa sheria za mazingira unafuatwa kama inavyoelekezwa.

"Hakuna nguvu iliyotumika zaidi ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya mifuko ya plastiki katika mazingira, hivyo tutaendelea kuhakikisha sheria na kanuni za usimamizi wa mazingira zinafuatwa kikamilifu ili kulinda mazingira ya nchi yetu," alisema Dk. Gwamaka.

Dk. Gwamaka alisema NEMC imewataka wataalamu katika mikoa yote hapa nchini kuhakikisha elimu inatolewa kwa wananchi na utekelezaji wa katazo linaendelea kutekelezwa ili kunusuru taifa kuingia katika athari za kimazingira kutokana na matumizi makubwa ya mifuko ya plastiki.

# Sera ugatuzi madaraka yaandaliwa

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Sera ya Taifa ya Ugatuzi wa Madaraka.

Sera hiyo inatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha wa 2019/20.

Hayo yalielezwa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Mwita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mchinga (CUF), Hamidu Bobali.

Katika swali lake, Bobali alisema Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwamba serikali ni pamoja na serikali za mitaa na mtu yeyote anatekeleza madaraka au mamlaka kwa niaba ya serikali au halmashauri.

"Je, ni kwa nini katika kipindi chote cha uwepo wa katiba hiyo, serikali haijatunga sera ya ugatuaji madaraka ambayo ingewezesha kuweka mfumo wa kisheria unaoelekeza mipaka, majukumu na utaratibu wa utekelezaji wa matakwa hayo ya kikatiba?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema sera hiyo itaweka mfumo wa kisheria unaoelekeza majukumu na mipaka ya wadau mbalimbali kwenye utekelezaji wa majukumu ya serikali katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Awali, alifafanua kuwa serikali za mitaa zipo kwa mujibu wa Ibara za 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

"Mwaka 1998 serikali iliandaa andiko la kisera la kuboresha serikali za mitaa ambalo ndio mwongozo wa utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka nchini," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara (katikati), akiwa kwenye picha ya pamoja na wanafunzi wa Shule ya St Anne Marie Academy waliopata daraja la kwanza na la pili kwenye matokeo ya kidato cha nne mwaka jana, waliotembelea bungeni juzi. Kushoto ni Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Jasson Rweikiza ambaye ndiye mkurugenzi wa shule hiyo na Mbunge wa Mikumi (Chadema), Joseph Haule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Barabara ya Gairo hadi Kilindi yatengewa fungu

SERIKALI kupitia Wakala wa Barabara (Tanroads) mikoa ya Morogoro na Tanga, itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara ya Gairo hadi Kilindi, ili kuiwezesha kupitika majira yote ya mwaka.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christine Ishengoma.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni lini madaraja ya Gairo - Chakwale - Idilo – Kilindi yatajengwa au karabatiwa ili barabara hiyo ipitike wakati wote wa kiangazi na masika bila matatizo.

Akijibu swali hilo, Kwandikwa alisema barabara hiyo inaunganisha wilaya za Gairo na Kilindi na sehemu ya barabara hiyo kwa upande wa mkoa wa Morogoro inaitwa Iyogwe – Chakwale – Ngilori kilomita 42 na sehemu iliyobaki ya kutoka Iyogwe – Kilindi iko mkoa wa Tanga.

Alisema kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi na kijamii, hususan katika wakati wa kusafarisha mazao ya kilimo na chakula kwa wilaya hizo katika mwaka wa fedha 2019/20.

Kwa mujibu wa Kwandikwa, serikali kupitia Tanroads imetenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa 'vented drift' moja na 'box culverts' mbili kwenye mito mikubwa ya Chakwale, Nguyani na Matale iliyopo kwenye barabara hiyo.

# Wakimbizi 66,100 warejeshwa kwao

BUNGE limeelezwa kuwa hadi sasa wakimbizi 66,148 wamerejeshwa kwao katika nchi mbalimbali ikiwamo Burundi tangu mwaka 2017.

Utaratibu huo wa kuwarudisha wakimbizi hao ambao ulianza mwaka 2017 umeelezwa kuwa ni endelevu.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rukia Kassim Ahmed.

Katika swali lake, alisema baadhi ya magereza nchini yamejaa wafungwa na mahabusi ambao ni wakimbizi.

"Je, ni lini serikali itawarejesha wakimbizi hao kwao ili kupunguza msongamano ndani ya magereza yetu?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema utaratibu huo wa kuwarejesha wakimbizi kwao kwa hiari ni endelevu na ulianza tangu mwaka 2017 hadi Aprili mwaka huu, wamerejeshwa 66,148.

Alikiri kuwa miongoni mwa wafungwa na mahabusi walioko katika magereza nchini ni raia wa kigeni wakiwamo wakimbizi kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Alisema magereza yenye idadi kubwa ya raia wakigeni yako mkoani Kigoma ambako kuna wakimbizi 91 wakiwamo wafungwa 38 na mahabusi 53.

Kwa mujibu wa Masauni, katika Gereza la Kibondo kuna wafungwa 22 na mahabusi 31, Gereza la Kasulu lina wafungwa wawili na mahabusi 19, Bangwe mfungwa mmoja na mahabusi watatu, Ilagala mfungwa mmoja na Kwitengo wafungwa 12.

Alisema wakimbizi ambao wamefungwa gerezani wanarejeshwa katika nchi zao za asili baada ya kumaliza kutumikia vifungo vyao.

Kadhalika, alisema serikali inaendelea kuwarejesha wakimbizi nchini kwao kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wahamiaji (IOM) na Burundi.


"Kuanzia Julai, 2018 hadi Aprili, mwaka huu, wakimbizi 31,643 kutoka Burundi walirejeshwa nchini kwao kwa hiari," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema wakimbizi kutoka Somalia na Ethiopia hawawezi kuingia nchini hadi wapitie nchini Kenya.

"Je, serikali haioni iko haja ya kushirikiana na Kenya kuwazuia wakimbizi hawa kuingia nchini? Pia kuna wakimbizi wako kambi za wakimbizi, lakini wana tabia ya kuzaliana sana sasa hivi wako mara mbili zaidi. Serikali ina mkakati gani wa kuwarejesha kwao wasiendelee kuzaliana hapa?," Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Masauni alisema hivi karibuni walikuwa na kikao cha kushirikisha mawaziri wa Kenya na Ethiopia ili kuzuia wahamiaji wanaoingia kwa wingi kutoka nchini Ethiopia kupitia Kenya na jambo hilo lina mafanikio makubwa.

Aliwahakikishia wabunge kuwa hali ya amani katika nchi hizo imetulia, hivyo hakuna sababu ya kuendelea kuwa na wakimbizi nchini na kwamba wataendelea kurejeshwa kwa hiari.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

HABARI ARUSHA

# TIC yasajili miradi ya uwekezaji 87 ya bil. 40/-

**Novatus Makunga,** ARUSHA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesema kwamba kilisajili miradi ipatayo 87 ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,482.23 (sawa na Sh. bilioni 40) kati ya Julai na Desemba mwaka 2018.

Miradi hyo ilitarajia kutoa ajira mpya kwa zaidi ya Watanzania 11,191 katika sekta mbalimbali.

Aliyebainisha hayo ni Meneja wa TIC Kanda ya Kaskazini, Daud Riganda, wakati wa maonyesho ya pili ya Karibu Kili-Fair yaliyomalizika jijini Arusha hivi karibuni.

Kati ya miradi 87 iliyosajiliwa ama kuandikishwa na TIC kwa upande wa sekta ya utalii hususan ujenzi wa mahoteli na kampuni za uwakala wa utalii, Riganda alisema kuwa kituo hicho kilisajili miradi takribani kumi.

Alitaja miradi ya mingine ni minne katika sekta ya kilimo, majengo ya biashara ni miradi 11 na miradi ya nishati iliandikishwa miwili. Alisema mbali na miradi hiyo, TIC pia ilisajili na kuandikisha mradi mmoja wa taasisi ya fedha, shule na afya.

Aidha, Riganda alisema kwamba kulikuwa na miradi ya huduma ipatayo saba, utangazaji mradi mmoja, masuala ya maliasili mmoja na miradi ya usafirishaji takribani saba.

Riganda alieleza kwamba kati ya miradi yote hiyo 87 iliyosajiliwa na kituo hicho nchini katika kipindi hicho, miradi 52 sawa na asilimia 60 inamilikiwa na Watanzania.

Kwa mujibu wa Riganda, miradi 33 sawa na asilimia 38 inamilikiwa na wageni na asilimia mbili ambapo ni mradi mmoja unaendeshwa kwa ubia kati ya Watanzania na wageni.

Alieleza kwamba kutokana na takwimu hizi, inaonyesha kwamba hivi sasa Watanzania wameamka na wameanza kuchangamikia fursa za uwekezaji.

Alizitaja nchi nyingine nne zinazoongoza kwa uwekezaji nchini kuwa ni China, Uingereza, Marekani na India.

Aidha, kwa upande wa nchi za Afrika zinazoongoza kwa uwekezaji nchini Mauritius, Afrika Kusini na Kenya.

Akifafanua kuhusiana na kituo hicho kinavyorahisisha mazingira ya uwekezaji nchini, Riganda alieleza kuwa katika kipindi hicho walishughulikia maombi ya huduma za ukaazi daraja la A za uwekezaji 258 na maombi ya daraja B 1,119.

Alisema kwamba katika kipindi hicho TIC ilitoa vibali vya kufanya kazi nchini takribani 1,248.

Alisema TIC ilishughulikia maombi yanayohusu masuala ya kodi kwa wawekezaji takribani 146 na kutoa leseni za biashara 40 katika kipindi hicho cha miezi sita.

Meneja huyo wa TIC Kanda ya Kaskazini, alieleza kwamba katika masuala yanayohusu mazingira, TIC walishughulikia na kusajili maombi 11 na maombi ya masuala ya ardhi kwa wawekezaji 248.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla (kushoto), akisalimiana na wananchi wa Kata ya Alaitole ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, alipofika kutatua mgogoro wa wananchi hao kuzuiwa kujenga shule ya wasichana ya bweni na mamlaka hiyo, katika eneo la Esere, wilayani Ngorongoro, juzi. **PICHA: WMU**

# Watakiwa kufanya kazi bidii, kuunga mkono juhudi serikali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI wa Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, wametakiwa kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi na kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli, katika kupambana na rushwa na dawa za kulevya.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2019, Mzee Mkongea Alli, wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwenye halmashauri hiyo.

Alisema kuwa serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za kijamii ikiwamo huduma za afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara, hivyo wananchi wanapaswa kuunga mkono juhudi hizo kwa kufanyakazi kwa bidii.

Alisema endapo wananchi watafanya kazi kwa bidii watakuwa wameiunga mkono serikali kupiga vita rushwa na adui ujinga kuelekea uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda kufikia mwaka 2020. Aliwataka wananchi kuhakikisha wanatunza mazingira na vyanzo vya maji, ili waendelee kupata majisafi na salama, kwani kupata huduma hiyo ni haki ya kila mtu, hivyo alisema ni wajibu wa kila mwananchi kutunza vyanzo vya maji.

"Suala hili la kutunza vyanzo vya maji ni letu sote, niwasihi wananchi wenzangu kuacha, kuchunga mifugo yetu katika hifadhi za misitu yenye vyanzo vya maji, pamoja na kuacha tabia ya kufanya shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji," alisema Ali.

Aidha, aliwataka wananchi kuwa tayari kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, huku akiwasisitiza muda utakapofika waende kujiorodhesha katika daftari la wapigakura.

Alisema jamii inapaswa kuwahamasisha wanawake na vijana kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Pia aliwataka wananchi kujitokeza wakati wa kampeni kusikiliza sera za wagombea na kufanya maamuzi sahihi ya kuchagua kiongozi, ambaye ataweza kuwaongoza vyema na kuwaletea maendeleo.

Katika Halmashauri ya Arusha, Mwenge wa Uhuru mwaka huu umetembelea na kukagua miradi nane yenye thamani ya Sh. bilioni 15.9 kwenye sekta za elimu, afya, maji, mifugo na uwekezaji, huku miradi mitatu imewekwa jiwe la msingi, miradi miwili imezinduliwa na kukagua miradi mitatu.

## Nguvu kuongezwa utalii wa fukwe

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

TANZANIA inatarajia kuongeza nguvu katika utalii wa fukwe kwa kuanzisha safari za meli za kisasa katika bahari pamoja na kuanzisha utalii wa mikutano.

Mkakati huo ulibainishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, alipotembelea maonyesho ya pili ya utalii ya Karibu Kili-Fair yaliyomalizika jijini hapa hivi karibuni.

Alisema hali halisi inaonyesha kwamba utalii wa fukwe una nafasi kubwa ya kuinua uchumi kwa kuwa mara nyingi wageni wanaotembelea huwa na mazoea ya kurudi mara kwa mara tofauti na utalii mwingine wa kutembelea mbuga za wanyamapori.

Alisema baadhi ya nchi zimeanza kutumia utalii wa meli kwa ajili ya vivutio ambavyo vipo katika fukwe, hivyo kuongeza idadi ya watalii na pia kukuza mapato.

Alisema licha ya kuongeza nguvu katika utalii wa fukwe, pia serikali itaongeza aina nyingine ya utalii wa mikutano ya kimataifa.

"Ni asilimia 20 tu ya fursa za utalii zilizopo Tanzania ndizo zinatumika licha ya kuwa na fursa kibao katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu," alisema.

Prof. Mkenda alisema maonyesha ya kimataifa ya utalii ya Karibu-Kili Fair ni moja ya mkakati ya ubunifu wa kusaidia kuchochea na kutangaza vivutio vilivyoko Tanzania.

Alisema vipo vivutio vingi vya malikale katika kanda mbalimbali za utalii kuwa ni pamoja na Iringa, Rukwa, Songwe, Mwanza, Mtwara, Lindi, Kigoma na Kagera ambavyo havijatangazwa vya kutosha.

Alisema lengo la serikali ni kuongeza idadi ya watalii watakaokuja Tanzania kutoka milioni 1.3 hadi milioni 1.5

Prof. Mkenda alisema mikakati hiyo inafanyika pamoja na uboreshaji wa huduma mbalimbali za utalii kwa kuimarisha mafunzo katika vyuo vya utalii.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya (CCM), akielezea kwa hisia maendeleo yaliyofanywa na Rais John Magufuli hadi kusababisha ahame Chadema kwenye Kijiji cha Nadonjukin, Kata ya Komolo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ripoti yabaini makubwa ukatili kwa wanawake

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MFUKO wa fedha unaotoa ruzuku kwa asasi za kiraia na taasisi binafsi zinazojishughulisha na utoaji wa msaada wa kisheria (LSF), umedai kuwa ripoti kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia inaonyesha kuwa nusu ya wanawake nchini wamefanyiwa ukatili wa kijinsia katika maisha yao.

Meneja Uhusiano na Biashara wa LSF, Jane Matinde, alisema utafiti wa mwaka 2010 juu ya mabadiliko ya idadi ya vizazi, vifo, maradhi na afya Tanzania (THDS) unaonyesha kwamba asilimia 39 ya wanawake wamefanyiwa shambulio la mwili.

Wakati asilimia 20 walifanyiwa unyanyasaji wa kijinsia katika maisha yao wakiwa watu wazima.

Matinde alikuwa akizungumza na waandishi wa habari wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Manyara katika Manispaa ya Moshi jana.

"Kwa wanandoa, kupigwa kofi kuliripotiwa kwa asilimia 36 na wanawake walioolewa, ikifuatiwa na asilimia 18 waliopigwa ngumi na wale waliosukumwa, tikiswa au kitu au vitu kutupwa kwao ni asilimia 16," ameeleza meneja huyo.

Matinde ameeleza kuwa tayari mfuko huo umeshatoa elimu kuhusu huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi milioni tatu nchini kote, lakini changamoto ni kuwapo kwa idadi ndogo ya kesi zinazoripotiwa.

Mpaka sasa kwa mujibu wa LSF, kesi zilizofikishwa mahakamani baada ya elimu hiyo ni 73 pekee katika mwaka 2018.

Aidha, kati ya mashauri ya mirathi 6,085 ambayo ni sawa na asilimia 58 yaliyoripotiwa na wanawake, asilimia 27 wamepata haki zao.

# Brela yafunguka mwamko mzuri wa biashara kaskazini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umesema mwamko wa urasimishaji wa biashara kwa mikoa minne ya kanda ya kaskazini umepata mjongeo chanya ikilinganishwa na kanda nyingine nchini.

Kasi ya usajili wa kampuni kwa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga inaongeza hamasa kitaifa, licha ya kuwa wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa elimu ya namna bora ya kujisajili kupitia njia ya mtandao.

Mkurugenzi wa Utawala na Fedha wa Brela, Bakari Mketo, aliyasema hayo jana, wakati wa utoaji elimu ya mafunzo ya namna bora ya kutumia mtandao katika zoezi la urasimishaji wa biashara kwa wamiliki wa kampuni mbalimbali.

Mketo alisema licha ya kuwapo kwa ofisi zao katika kanda mbalimbali hapa nchini, lakini tumekuwa tukipokea simu nyingi kutoka kanda ya Kaskazini hasa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha wanaotaka kurasimisha biashara zao ili kuweza kutambulika kisheria.

"Tulipotoa maoni kutoka kwa wananchi ya kutaka kuweka ofisi kila mkoa, lakini tumeona bado haitasaidia kuwafikia wananchi wengi hasa wa maeneo ya vijijini na badala yake tukaamua kuongeza nguvu kwenye namna ya kutumia mtandao kurasimisha biashara, ili wananchi waweze kuendana na wakati na kuongeza ushindani wa kimataifa," alisema.

"Tunachotoa hasa mbali na elimu ya namna bora ya kutumia mtandao kujisajili pia tunawaeleza umuhimu wa urasimishaji wa biashara zao, ili waweze kutambulika maeneo mbalimbali ikiwamo taasisi za kifedha, ushindani wa zabuni serikalini pamoja na kulalamika ikiwa mtu ametumia jina la kampuni/biashara yako," alisema.

Alisema gharama za usajili zinatofautiana kulingana na aina ya usajili husika kwa kampuni ambazo ni kati ya Sh. 175,000 hadi 512,200 kwa kiwango cha juu kwa kampuni, ingawa usajili huo unategemea na mtaji uliopo kwenye mkataba wa makubaliano (MoU).

Pamoja na mambo mengine, Ofisa wa Brela kutoka Kitengo cha Miliki Bunifu, Suzana Senso, alisema kwa kasi ya nchi yetu na dunia kwa ujumla ni kwamba urasimishaji wa biashara haukwepeki, hivyo wajasiriamali wote wanapaswa kusajili biashara zao kabla ya kuanza kijitangaza kwa kiwango kikubwa na baadaye kupata hasara kwani wapo wanaowahi kufanya usajili kwa majina hayo.

"Tunawaomba wafanyabiashara kabla ya kuanza kuzitangaza biashara zao wafike ofisini kwetu kwa ajili ya urasimishaji kwani wengi wamekuwa wakipata hasara baada ya kutumia jina kuzitangaza biashara zao na wanapofika kwetu wanakuta jina hilo tayari linatumika na mtu mwengine," alisema.

"Tupo hapa mkoani Kilimanjaro kwa siku tatu ambapo tutoa elimu kwa wadau mbalimbali juu ya namna bora kutumia mtandao pia tutafanya ukaguzi, na kufanyia kazi changamoto tulizozionа, ambapo panamkanganyiko wa nani ni mrasimishaji wa biashara kwani wapo ambao wanakwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)."

# Mawenzi yaomba madaktari bingwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BAADHI ya wananchi wa Manispaa ya Moshi, wamemuomba Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kuangalia uwezekano wa kupeleka madaktari bingwa walao wawili wa magonjwa ya akili katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), ili kupunguza changamoto ya uhitaji wa huduma za kibingwa.

Hospitali hiyo kwa muda mrefu imekuwa ikitumika kama hospitali ya rufani ya kupokea wagonjwa wa akili kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Manyara.

Miongoni mwa watu waliozungumza na Nipashe kuhusu uhitaji wa daktari bingwa wa magonjwa ya akili, Lucas William, Yohana Peter na Agness Emanuel, kwa nyakati tofauti wameeleza kuwa kukosekana kwa wataalamu hao kunasababisha huduma za kibingwa kuwa ngumu kupatikana.

Kwa siku moja, hospitali hiyo inapokea wagonjwa wa akili kati ya 45 hadi 60 kutoka mikoa hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Japhet Boniface, alisema wanakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa daktari bingwa wa magonjwa ya akili, licha ya ukweli kwamba Mawenzi sasa inatumika kama Hospitali ya Kanda ya magonjwa haya.

Pia, alisema changamoto nyingine inayoikabili hospitali hiyo ya kanda ni uhaba wa dawa za magonjwa ya akili.

Kutokana na changamoto hiyo na yeye amemwomba Waziri Mwalimu kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya dawa hizo katika hospitali hiyo.

Pamoja na kujitokeza kwa tatizo hilo, Kafwila ameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la mama na mtoto katika hospitali hiyo ili kuondoa msongamano uliopo sasa katika jengo wanalolitumia ambalo ni dogo.

Ukurasa 18



Trump 'aupiga tafu' mpango wa Brexit ziarani nchini Uingereza


## UCHAMBUZI:

**KUELEKEA UCHAGUZI S/MITAA;**
Hofu ya sheria inavyobana wanahabari



Ukurasa 19

## Kimataifa



### Tunisia, Niger 'kidedea' uchaguzi wa Baraza la Usalama la UN

Ukurasa 17


# siasa

JUMATANO JUNI 12, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




### Sudan yavuna ilichopanda Janjaweed wakitwaa hatamu Baraza la Kijeshi

Ukurasa 15

# Ukimya kutawala migogoro EAC, dalili za kushindwa kwa jumuiya?

**Na Mashaka Mgeta**

NI kama hakuna kinachoendelea katika kupata suluhu ya migogoro 'inayozitafuna' baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hususani kati ya Rwanda dhidi ya Burundi na Uganda.


Kwa hali ilivyo sasa, mataifa wanachama wa EAC yaliyo katika migogoro ya kidiplomasia yanaendelea 'kujitenga na maadui' zao, yakitafuta jinsi yanavyoweza kukuza uhusiano hasa unaolenga nyanja za kiuchumi.

Wakati hayo yakiendelea, EAC inaendelea na mchakato utakaozifikisha nchi wanachama kuwa shirikisho moja.

Kushamiri kwa migogoro hiyo hakutoi taswira nzuri kwa hali ya baadaye ya EAC. Tayari nchi kama Rwanda inayoguswa kuwa 'kiini' cha migogoro hiyo, ikifungua uhusiano zaidi na mataifa mengine ya ukanda wa Kusini mwa Afrika, hususani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Migogoro inayoendelea 'kuitesa' EAC inajumuisha ule uliodumu kwa takribani miaka minne sasa ukizihusisha nchi za Burundi na Rwanda. Burundi 'ilishaapa' kwamba Rwanda haina sifa za kuwa mshirika wake wa

Endelea 16




Rais John Magufuli wa Tanzania (kushoto) akiwa na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. **PICHA: MTANDAO**

### China, Russia zapanua ushirikiano kukabili uhasama wa Marekani

Ukurasa 20

# Mbio za Mwenge ziendelee kuumbua wanaofisadi miradi ya maendeleo

Na Sabato Kasika

MWENGE wa Uhuru kwa sasa unaendelea kukimbizwa mikoa mbalimbali nchini ukiwa na kaulimbiu isemayo; "Maji ni haki ya kila mtu, tutunze vyanzo vyake na tukumbuke kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa."

Uzinduzi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ulifanywa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan Aprili 2 mwaka huu, kwenye uwanja wa Mlowo mkoani Songwe na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Katika uzinduzi huo, Makamu wa Rais alitoa rai kwa Watanzania kutumia mbio hizo kwa mwaka huu kumkumbuka Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kwa kupinga vitendo vyote vya dhuluma.

Lakini pia ufisadi, rushwa, maradhi, chuki, dharau huku akiwataka kuenzi umoja na mshikamano na kuchapa kazi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

"Nimependezwa na kaulimbiu hii ambayo ina uwiano wa moja kwa moja na jukumu langu la kila siku la kusimamia na kutunza mazingira nchini... sote tunafahamu kwamba bila utunzaji thabiti wa mazingira basi vyanzo vya maji hupotea," akasema.

Yapo mengi aliyoyasema Makamu wa Rais katika uzinduzi huo, lakini hapa ninataka kujikita zaidi katika kile ambacho kimekuwa kikiibuliwa na mbio hizo.

Mwenge unaendelea kuzunguka mikoa mbalimbali nchini huku kukiwa na kumbukumbu ya miradi hewa ambayo ilibainika katika mbio za mwaka 2018.

WAZIRI MHAGAMA

Wakati akitoa taarifa za mbio za Mwenge wa Uhuru Oktoba 2018 jijini Tanga, Waziri wa Nchi, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliweka wazi miradi hewa iliyoibuliwa na mbio hizo.

Kwamba Mwenge wa Uhuru kwa mwaka jana ulizindua miradi 1,432 ya thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 664 kwenye mikoa 31 na halmashauri 195, lakini kati ya miradi hiyo 64 iligundulika kuwa na ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni 27. Mhagama akasema mwenge huo umekuwa ukifanya kazi ya kupambana na kufichua rushwa katika miradi yote iliyozinduliwa na kuwekewa jiwe la msingi nchini kote huku mingine ikiachwa kutokana na kuwa na kasoro.

"Mbio za Mwenge wa Uhuru zimetumika kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo, kumulika na kuchoma uzembe ambapo kwa mwaka huu wa 2018 zimebaini kuwapo kwa kasoro katika kutekeleza miradi ya maendeleo," akasema na kuongeza:

"Miradi 80 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 27 za halmashauri 64 ilionekana kuwa na kasoro hivyo haikuzinduliwa wala kuwekewa jiwe la msingi."

Kaulimbiu ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka jana ilikuwa ni; 'Elimu ni ufunguo wa maisha, wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu'

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alibainisha dhamira ya serikali kupitia kaulimbiu hiyo ni ya kuwashirikisha wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo kuwekeza katika elimu ili kuzalisha rasilimali watu yenye ujuzi na stadi zitakazowezesha kuchochea mapinduzi ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025.

"Ukitaka kuleta maendeleo ya uchumi ulio imara, ukitaka kujenga jamii inayoheshimu na kufuata misingi ya uwajibikaji na ubunifu, ukitaka kujenga taifa lenye amani na utulivu, lazima uwekeze zaidi katika elimu," anasema.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan (aliyeshikilia mwenge mwenye miwani), akimkabidhi Mwenge kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa kwa mwaka 2019, Mzee Mkongea Ali kuashiria kuanza kwa mbio za Mwenge wa Uhuru 2019. Kulia ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. **(PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**MBIO ZA MWENGE 2019**

Siku chache baada ya uzinduzi huo, kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa kwa mwaka huu alianza kukumbana na madudu katika miradi ya maendeleo.

Kiongozi huyo, Mkonge Ally, aligoma kuzindua mradi wa kwanza wa ujenzi wa Zahanati ya kijiji cha Igunda kutokana na mgongano wa taarifa.

Mradi huo uko wilayani Mbozi, ambapo taarifa aliyosomewa na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Igunda, Mwanyukwa Myuki ilionyesha kwamba Sh. 537,000 za ujenzi wa zahanati hiyo, zilitokana na michango ya Mwenge wa Uhuru zilizochangishwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Mtendaji huyo alisema jengo hilo limegharimu Sh. 32,726,400 zilizotolewa na wadau ambapo wananchi wametoa Sh. 13,721,300, halmashauri Sh 10, 355,011, Mfuko wa Jimbo Sh. 1, 278, 000 na Sh. 6, 835, 000 zimetoka kwa wadau wa maendeleo.

Wakati akiendelea na mbio za Mwenge mikoa mbalimbali nchini, kiongozi huyo ameendelea kubaini kuwapo kwa madudu kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo, hali ambayo imesababisha miradi hiyo isizinduliwe.

Kwa mfano mwezi huu wa Juni kuna miradi kadhaa ambayo amekataa kuizindua ukiwamo wa maji uliopo Halmashauri ya Geita, ambao taarifa zimepishana.

Kwamba hawezi kufungua mradi huo kutokana na taarifa za utekelezaji wake kupishana kwa gharama ya Sh. milioni 9, ambapo ameagiza Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru) kuchunguza taarifa za mradi huo na kukabidhi taarifa kwa wakimbiza mwenge ndani ya siku 10.

Siyo hapo tu bali mwezi huu pia amekataa kupokea mradi wa sekta ya maji na barabara wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 484.9 kwa sababu nondo zilizotumika katika ujenzi huo hazikupimwa.

Mradi upo wilaya ya Tarime mkoani Mara na kuagiza mkuu wa wilaya hiyo, Charles Kabeho kutoa taarifa ndani ya wiki mbili.

Vilevile kiongozi huyo amekataa kutoa hundi ya Sh. milioni 100 kwenye Saccos ya Tuimarike, kwenye Halmashauri ya Mji wa Kahama, kutokana na kile alichodai kwamba mkurugenzi amekiuka sheria ya vikundi iliyopo.

Safari ya mbio za Mwenge wa Uhuru inaendelea hadi Oktoba mwaka huu, sasa ni mwezi Juni, na tayari baadhi ya miradi ya maendeleo imekataliwa. Je, kama hali itaendelea kuwa kama hivi, kufikia Oktoba itakuajе?

MASLAHI YA UMMA MBELE

Moja ya mambo ambayo Rais John Magufuli anahimiza viongozi, ni kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, sambamba na kuhakikisha wanasimamia matumizi ya rasilimali za umma kwa maslahi ya wananchi.

> "Mbio za Mwenge wa Uhuru zimetumika kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo, kumulika na kuchoma uzembe ambapo kwa mwaka huu wa 2018 zimebaini kuwapo kwa kasoro katika kutekeleza miradi ya maendeleo,"

Rais anaamini kwamba utekelezaji wa majukumu kwa kuzingatia sheria, ni njia ambayo inasaidia kuepusha uchakachuaji kwenye miradi ya maendeleo, lakini inaonekana bado wapo ambao hawajazingatia hilo.

Mfano hai ni taarifa hizi za kuwapo kwa miradi ya maendeleo ambayo haikuzinduliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka jana na za mwaka huu ambapo pia ipo baadhi ya miradi imekataliwa wakati mbio hizo zikiendelea.

Ninaamini kwamba kama wahusika wangezingatia wito ambao umekuwa ukitolewa mara kwa mara na Rais, basi wangetimiza wajibu wao kwa kuzingatia kwamba katika maendeleo yoyote yale kuna haja ya kuzingatia ushirikishwaji wa wananchi ili kuepuka uchakachuaji.

Ikumbukwe kwamba ushirikishwaji wa wananchi katika miradi ya maendeleo ni hatua ambayo wale waliokusudia kuanzisha mradi kwenye eneo fulani hushirikisha wananchi husika, ambao kimsingi ndio mradi unaowalenga.

Pamoja na hayo, wale ambao bado hawajafikiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru na wamefanya vitu ambavyo ni kinyume na utaratibu, basi wajue kuwa watajikuta katika mnyororo huo wa miradi yao kukataliwa.

Taarifa ya baadhi ya miradi ya maendeleo kutozinduliwa katika mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka jana zilitosha kuwa fundisho, lakini hali hiyo inapoanza kujitokeza tena mwaka huu, ni wazi bado kuna tatizo.

UCHAMBUZI

# Sudan yavuna ilichopanda Janjaweed wakitwaa hatamu Baraza la Kijeshi

**Na Ani Jozeni**

UMMA wa Sudan umeanza kujitafakari nini hasa kinatokea nchini humo baada ya kukwama kwa juhudi za kuunda serikali ya mpito inayoongozwa na raia, licha ya kuwa na wajumbe wengi wa Baraza la Kijeshi linalosema ni la mpito hadi ufanyike uchaguzi mkuu.

Baada ya pande hizo mbili kukwama katika kuamua nani ataongoza chombo maalum cha utawala (hasa ni baraza mchanganyiko), inaelekea kuwa watendaji katika Baraza la Kijeshi wamefikia uamuzi kuwa kutumia nguvu ndiyo njia ya kumaliza mvutano huo.

Viongozi wa maandamano walisakwa na zaidi ya waandamanaji 100 kuuawa, huku ikijitokeza kuwa kundi la Janjaweed linatenda hayo.

Kundi hilo linajulikana nchini humo kwa jina la kijeshi (kitaaluma) la Rapid Support Forces, yaani vikosi vyenye uwezo wa kuwekwa katika medani ya vita kwa haraka, na wachambuzi wa habari wanasema ni kundi lile lile lililosikika dunia nzima kwa jina la Janjaweed.

Lilishutumiwa miaka zaidi ya 10 iliyopita kwa kuzingira makazi na kunyang'anya mali, kuua watu wengi katika eneo la Darfur, wakilizingira kwa kutumia askari wanaopanda farasi na kusomba watu bila kufuata utaratibu wowote wa kisheria.

Mkuu wa kundi hilo sasa ndiye naibu mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi linalotawala sasa, na amekuwa msemaji wake, kuainisha umuhimu wa vikosi vyake katika mazingira ya Sudan hivi sasa, ambako sehemu ya jeshi la kawaida inawajali watu.

Mashambulio yaliyofanywa na vikosi vya jeshi na vikosi maalum vya medani ya vita (nusu mgambo na kwa upande fulani kuna makomandoo miongoni mwao) ilishtua dunia wakati ilipoonekana kuwa watu wako waliouawa kwa risasi wakati wa maandamano, na wengine kuonekana tu wakielea katika mto wa Nile.

Ni watu waliotafutwa maeneo tofauti, hata majumbani kwao wakati wa usiku, wakateswa kwa muda kupata habari za usimamizi wa maandamano, wakapigwa risasi na kutupwa katika mto, hali iliyoishtua dunia kuwa jeshi la Sudan linaandaa umwagaji damu wa kina ili maandamano yaishe. Bado mwanya haujaonekana katika hali hiyo.

Dhamira ya utawala wa kijeshi kufuata mwelekeo wake huo ilidhihirika bila kificho wakati watawala walipomruhusu Abiy Ahmed, Waziri Mkuu wa Ethiopia kufika nchini humo kujaribu kupata usuluhishi akaongea na viongozi wa upinzani, halafu wajumbe wa Baraza la Kijeshi.

Punde, viongozi wa waandamanaji walioshiriki walikamatwa, angalau baadhi yao, ingawa haikutajwa kama kuna aliyeuawa hadi sasa, baada ya kushiriki majadiliano hayo.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje alisema labda juhudi za kutafuta muafaka zitafanikiwa; labda, labda.

Miili iliyoopolewa kutoka Mto Nile ilifikia 40 kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Madaktari wa Sudan (moja ya asasi muhimu za kuratibu maandamano hayo), ambako taarifa zilisema kuwa baadhi ya walioopolewa walikuwa wamejeruhiwa, wakatupwa mtoni na kufa.

Kuna hofu kuwa idadi ya waliouawa na hata kutupwa mtoni inaweza kuongezeka siku zinavyopita, kwani kuna mkanganyiko mkubwa kuhusu watu kadhaa waliopo, na si rahisi kuthibitisha kila taarifa kuhusu mtu kuwa salama au kuuawa, kama mwili haujapatikana.

Lawama zote zinaelekezwa kwa kundi hilo la Janjaweed, linalofahamika kwa utamaduni wake wa ukatili na kutojali haki za binadamu katika kuendeleza malengo ya utawala wa kijeshi dhidi ya makundi yenye mwelekeo tofauti.

Pamoja na kuwa sehemu kubwa ya viongozi wa maandamano na sehemu kubwa zaidi ya waandamanaji wenyewe ambao wengi zaidi ni vijana, bado kuna tatizo la kitaasisi na kitamaduni kwani upande wa Kaskazini wa iliyokuwa Sudan kubwa ilikuwa upande wa aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo, Jenerali Omar al-Bashir.

Ni kama vile wananchi wa rika la kati na vijana wanavuna walichopanda wazazi wao, kwa kujitofautisha na wakazi wa Kusini ya nchi, hasa kwa kuutukuza 'Uarabu' na kuubeza Uafrika, wakati lugha yenyewe ya Kiarabu imegawanyika vipande vipande, na si rahisi kusema kuwa kule Misri au Jordan wanawatambua kina Al Bashir kama ni Waarabu.

Viongozi wa waandamanaji wamebakiwa na silaha moja tu, yaani kuendelea na maandamano, kufunga barabara za jiji la Khartoum (na labda kwingineko nchini) na kutazamia kuwa nchi za nje zitaongeza msukumo kwa utawala wa kijeshi kuonyesha nia dhahiri ya kutoa madaraka kwa raia, ili kipindi cha mpito kisiwe cha kuimarisha udikteta.

Hasa ni kufufua ngome za u-Bashir na kusheheni Janjaweed katika ngazi tofauti za utawala nchini humo.



Jenerali Mohamed Hamdan "Hemeti" Dagalo, Naibu Mkuu wa Baraza la Kijeshi linaloongoza Sudan kwa hivi sasa. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo si rahisi kuona kinachoweza kutokea kwani nchi za nje zimegawanyika, kwa mfano jirani Eritrea ni mtetezi wa mstari wa mbele wa Baraza la Kijeshi na kutoangalia vitendo vyake, ila kutoingiliwa kutoka nje.

Mkutano wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ulifanyika New York baada ya kuona hatua za kwanza za mazungumzo zinakwama, na kabla ya kupigwa risasi kwa waandamanaji na miili kuopolewa katika mto wa Nile.

Hapakuwa na muafaka wowote na hata taarifa ya kina ya mjadala haikutolewa, hali inayoashiria kuwa hapakuwa na pendekezo lolote lililoungwa mkono na wajumbe wengi, hata kama baadhi ya wanachama hasa wa kudumu wenye 'kura ya turufu' wasingekubaliana.

Ina maana juhudi za kuingiza Umoja wa Mataifa zinaelekea kukwama bado.

Yako maeneo mengine ambako juhudi tofauti za kimataifa zinawezekana, tena si kwa diplomasia ila kwa mashtaka ya jinai, kwani baadhi ya watendaji na hasa msemaji wa Baraza la Kijeshi ni mmoja wa vinara wa kuendeleza vitendo vya kukiuka haki za binadamu hasa jimbo la Darfur wakati uliopita.

Ikiwa naibu mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi ataendeleza mbinu za kuua wale wanaoandamana na kutupa mtoni baadhi kuwa funzo kuwa utawala wa kijeshi uko 'ngangari kinoma,' si vigumu kuona Mahakama ya Jinai ya Kimataifa (ICC) huko The Hague ikitaka afikishwe huko, pamoja na baadhi ya watu wake wa karibu.

Si ajabu vilevile vikwazo vya kina vikawekwa pamoja na kuwa yapo mataifa makubwa yasiyoweza kuafikiana kuchukua hatua hizo, zichelewe.

Kina cha umahiri na nafasi ya Janjaweed katika Baraza la Kijeshi la mpito inaonekana wazi katika itifaki ya kutoa matangazo ambako naibu mwenyekiti kimsingi ndiye msemaji, na pia rejea zote kuhusu baraza hilo linaainishwa kuwa mwenyekiti wake ni Jenerali Abdel-Fattah al-Bourhani na naibu mwenyekiti ni Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, wanayemwita 'Hemeti' ambaye pia ni kamanda wa RSF, vikosi maalum vya kupeleka mstari wa mbele.

Mstari huo wa mbele wa vita nchini humo sasa ni kupambana na waandamanaji, na hawatokani na wale ambao Janjaweed ilikuwa inawasaka maeneo ya Kusini hasa Darfur, ila wale ambao - katika kizazi kilichopita – walisimama pembeni wakiwasikiliza wapambe wa Rais Al Bashir wakijitetea.

Jambo la msingi katika msuguano huo ni kuwa Sudan tangu mwaka 1989 imeongozwa na utawala wa kijeshi ambao ndani yake wakuu wa makabila na koo nchini humo wanafanya maamuzi kuhusu bajeti na usimamizi wa sheria kwa jumla.

Ni baada ya kuanguka kwa utawala wa kijamaa wa Jenerali Jafaar el Nimeiri na kuingia kwa uzalendo wa siasa kali, kusafisha makundi yasiyotaka utawala huo. Sasa wazawa wenyewe wa Kaskazini wanataka demokrasia.

UCHAMBUZI

Inatoka Uk. 13

maendeleo.

Unapoisoma dira ya EAC inaeleza kwamba ni kutanua wigo wa ushirikiano kati ya nchi wanachama pamoja na mambo mengine, masuala ya siasa, uchumi na kijamii kwa maslahi ya pande zote.

Hivyo migogoro ya kidiplomasia kama huo wa Rwanda na Burundi inazidi kuongeza changamoto katika kufikia azma hiyo.

Jamal Juma ni mwanataaluma wa ushirikiano wa kimataifa, anasema nchi zilizo wanachama katika ushirikiano wa kikanda zinapoibua na kuweka bayana mgogoro kati yao, zinafifisha (kimantiki) malengo, mipango na mikakati inayokusudiwa, ili ziweze kuwa na nguvu kubwa za kiuchumi, kiulinzi na kijamii.

"Huwezi kuwa na jumuiya imara katika ukanda husika wakati wanachama wake hawazungumzi lugha moja, hawapo pamoja bali wanatengana kwa migogoro hasa ya kidiplomasia," anasema Juma anapohojiwa juu ya mtazamo wake kuhusu kudorora kwa ushirikiano wa baadhi ya nchi wanachama wa EAC.

Ikumbukwe kwamba katika mgogoro wa kidiplomasia uliowekwa wazi kati ya mataifa hayo, Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza, amekuwa akimshutumu Rais Paul Kagame wa Rwanda na utawala wake kwa kuihujumu Burundi.

Rais Nkurunziza akasema kujiingiza kwa Rwanda katika masuala ya ndani ya Burundi kulisababisha athari tofauti ikiwamo kukosekana kwa amani na utulivu nchini humo.

Lakini serikali ya Rwanda imekuwa ikikanusha madai hayo mara kwa mara na kwa upande mwingine, ikieleza pia shutuma zake dhidi ya Burundi, kama ambavyo imekuwa ikifanya kwa mataifa mengine yaliyo kwenye mgogoro kama huo.

Yapo matukio kadhaa ambayo Burundi imekuwa 'ikiinyooshea kidole' Rwanda kwamba inahusika ama kuwa karibu na uratibu na utekelezaji wake.

Kwa mfano ni kuhusiana na uhasama uliopo kati ya utawala wa Rais Kagame wenye Makao Makuu yake jijini Kigali na ule wa Rais Nkurunziza wenye Makao Makuu aliyoyahamisha kutoka Bujumbura kwenda Gitega, ulikolea zaidi mwaka 2015.

Wakati huo, Rais Nkurunziza alikuwa katika mchakato wa kuingia katika awamu ya tatu ya utawala, hivyo kuzua utata kiasi cha kusababisha maandamano nchini mwake, na baadaye kunusurika katika mapinduzi ya kijeshi yaliyozimwa.

Mapinduzi hayo yalifanyika Mei, 2015 wakati Rais Nkurunziza akiwa jijini Dar es Salaam kushiriki kikao cha usuluhishi wa mzozo wa kisiasa uliohusu kutaka kuongeza muda wa kuiongoza Burundi.



Rais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto), akiwa na Rais Paul Kagame wa Rwanda.

# Ukimya kutawala migogoro EAC, dalili za kushindwa kwa jumuiya?

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Usalama wa Burundi 'aliyetumbuliwa' na Rais Nkurunziza Februari, 2015, Meja Jenerali Godefroid Niyombare, alitangaza mapinduzi hayo kupitia kituo binafsi cha redio cha Bonesha FM.

Ikulu ya Rais Nkurunziza ilijibu baadaye kwamba mapinduzi hayakufanikiwa na mhusika alikuwa akisakwa kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Pia, kumewahi kutokea mapigano ya kutumia silaha za moto kufuatia mauaji ya raia na wapiganaji kwenye maeneo ya mpakani mwa nchi hizo.

Hayo ni miongoni mwa matukio ambayo Burundi inaihusisha Rwanda kiasi cha kuifanya serikali ya Rais Nkurunziza, kutamka wazi kwamba Rwanda imekosa sifa za kuendelea kuwa mshirika wake.

Na kwa hali hiyo, Burundi ikaiomba EAC kuitisha kikao cha dharura kwa lengo la kupata suluhu ya mzozo huo ambao hata hivyo hakikufanyika.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa Burundi, Uganda na Rwanda zipo katika historia inayozipitisha kutoka kwenye uhusiano mwema na ule unaowakaribisha kuingia katika vita.

Ni 'urafiki wa mashaka' ukijikita katika historia inayoonyesha kuwa Rais Kagame amewahi kuwa mmoja wa 'nguzo' zilizofanikisha kilichokuwa kikundi cha uasi kumuingiza madarakani Rais Yoweri Museveni mwaka 1986.

Kwa upande wake, Rais Museveni pia anatajwa kuwa mshirika wa karibu aliyeibuka baadaye na kukisaidia kilichokuwa kikosi cha uasi cha Kagame (kabla ya kuwa Rais) kuingia madarakani.

Kwa maana nyingine, viongozi hao wawili wenye historia ya kutokea jeshini na kupigana vita vya msituni, wanajuana kwa muda mrefu na pia kusaidiana katika harakati za kisiasa na uongozi kwa mataifa yao.

Lakini wawili hao wamejikuta katika mgogoro unaokuwa kufikia hatua ya kuhatarisha uhusiano wa wananchi wao, umoja na mshikamano ndani ya EAC.

Hivi karibuni, Uganda iliishutumu serikali ya Rais Kagame kwa kuzuia malori ya mizigo na magari mengine kutoka nchini mwake kuingia Rwanda.

Pia Uganda ikasema serikali hiyo iliwazuia raia wake wasivuke mpaka kuingia nchini humo (Uganda), wakati ambapo mataifa hayo jirani yanaingia kwenye mgogoro.

Utawala wa Rwanda uliyazuia maroli na magari mengine kutoka Uganda kuingia nchini humo, Msemaji wa Serikali ya Rais Museveni, Ofwono Opondo, aliwaambia waandishi wa habari.



Rais Pierre Nkurunziza wa Burundi. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, serikali ya Rais Kagame kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Richard Sezibera, ilikanusha shutuma hizo na kufafanua kwamba magari hayo yalielekezwa kupitia mpaka wa Kagitumba uliopo Kaskazini mwa nchi hiyo ili kupisha ujenzi wa barabara yenye shughuli nyingi katika mpaka wa Gatuna.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kwa takribani muongo mmoja tangu vikosi vya majeshi kupigana hadi kumwaga damu kwenye jiji la Kisangani, Mashariki mwa DRC, Uganda na Rwanda wamekuwa katika 'urafiki wa mashaka'.

Hata hivyo, mzozo huo ulichukua sura tofauti hadi Julai 2011 ambapo Rais Museveni alifanya ziara iliyowashangaza wengi kwenda Rwanda na kutumia siku kadhaa, akiwa na timu ya wataalamu wake waliongia mikataba kadhaa ya ushirikiano kati ya nchi mbili hizo.

**UENYEKITI WA KAGAME EAC**

Devotha Masha, anayejitambulisha kuwa mfuatiliaji wa masuala ya EAC, anasema kwa hali ilivyo sasa ni vigumu kufikiria kupatikana kwa suluhu ya migogoro ndani ya jumuiya hiyo, hasa inayozihusu Rwanda dhidi ya Burundi na Uganda.

Masha anasema kiwango cha mgogoro kati ya mataifa kinapodhihirika kupitia kwa marais wa nchi husika kinahitaji zaidi utashi wa kisiasa na kujitenga na 'upande' ili kupata suluhu ya kudumu.

Anasema hali hiyo haionekani kwa EAC kutokana na namna uongozi ulivyo, Rais Kagame akiwa Mwenyekiti wakati huo huo mhusika muhimu katikati ya migogoro kidiplomasia inayoitikisa jumuiya hiyo.

Rais Kagame 'alichukua' nafasi hiyo kutoka kwa mtangulizi wake, Rais Museveni wa Uganda ambao pia mataifa yao yapo katika mgogoro.

Ingawa ni hivyo, taarifa zinazodaiwa kutoka ndani ya sekretarieti ya EAC zikaripotiwa na gazeti la East African kuwa jumuiya hiyo ilitambua ugumu uliopo kwa Rais Kagame kuchukua nafasi hiyo hasa baada ya kuwekewa pingamizi na Burundi, lakini hatimaye uteuzi wake ukapitishwa 'kwa mbinde'.

Francis Chota, mhitimu wa shahada ya uhusiano wa kimataifa anasema isingefaa kwa Rais Kagame kuchukua nafasi hiyo kwa vile kunaweka mazingira ya kupunguza tija katika kupata suluhu ya migogoro iliyopo.

Mwanaharakati wa masuala ya migogoro ya kijamii, Silvanus Isdory anasema ni vigumu kupata suluhu ya mzozo unaohusisha mmoja wa upande kuwa na nguvu za kiutawala na uongozi.

"Katika utatuzi wa mgogoro wowote, ili upate suluhu nzuri ya kudumu, pande zinazopingana zisiwe katika mamlaka ya utawala ama uongozi, na ndio maana hata kiongozi anaposhutumiwa, ni vema akajiuzulu kupisha uchunguzi, ndivyo ilivyo katika migogoro pia," anasema.

Anasema ingawa EAC inaweza kuwa na mifumo ya kitaasisi inayoweza kukabiliana na kuwapo katika uongozi kwa Rais Kagame na kushughulikia mzozo ambao serikali yake inashutumiwa, lakini mazingira ya kupata suluhu ya kudumu hayatakuwa na wigo mpana kufikia lengo.

Vyanzo vingine vimewakaririwa na vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano vikieleza kuwa kutokana na mzozo unaoendelea kati ya Burundi na Rwanda, kuna uwezekano kuvunjika kwa EAC kama ilivyotokea mwaka 1977.

Lakini Katibu Mkuu wa EAC, Libérat Mfumukeko, anasema kuvunjika kwa jumuiya hakuwezi kutokea tena na kufafanua kuwa awali (1977) ilikuwa 'nyakati za giza' tofauti na sasa ambapo jumuiya imepiga hatua kubwa katika kujiimarisha kwake.

Lakini swali bado linabaki kuwa, je ukimya unaojitokeza kwa migogoro inayozikabili nchi wanachama wa EAC, utarajiwe kuibuka na mafanikio katika kuidhibiti ama itakuwa mwanya wa mpasuko zaidi katika jumuiya hiyo?

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540.**

## Tunisia, Niger 'kidedea' uchaguzi wa Baraza la Usalama la UN

BARAZA Kuu la Umoja wa Mataifa, limechagua nchi tano wanachama wa umoja huo ambao watachukua ujumbe usio wa kudumu kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC), kuanzia mwezi Januari mwakani.

Uchaguzi huo umefanyika kwa mujibu wa Ibara ya 23 ya Katiba ya Umoja wa Mataifa (UN) na kanuni namba 142 ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kuhusu chaguzi za kila mwaka za wajumbe wasio wa kudumu wa Baraza la Usalama ambao watahudumu kwa kipindi cha miaka miwili.

Kanuni zinataka mshindi apate theluthi mbili za kura ambapo kwa upande wa bara la Afrika, nchi zilizochaguliwa ni Niger na Tunisia ambazo zitachukua nafasi ya Cote d'Ivoire na Equatorial Guinea, zinazomaliza muda wao mwishoni mwa mwaka huu.

Kutoka kundi la Asia-Pasifiki, kiti kilichokuwa kinashindaniwa ni kimoja ambapo Vietnam imeshinda na itachukua nafasi ya Kuwait.

Kwa upande wa kundi la nchi za Amerika ya Kusini na Karibea, Saint Vincent na Grenadines imeibuka kidedea kwa kupata kura 185 dhidi ya El Salvador iliyopata kura 6 na hivyo kuchukua nafasi ya Peru inayomaliza muda wake.


Nafasi ya bara la Ulaya imechukuliwa na Estonia iliyopata kura 132 ambayo imeshinda nchi nyingine tatu ambazo ni Romania, Georgia na Latvia na sasa Estonia itachukua nafasi ya Poland inayomaliza muda wake.

Baraza la Usalama lina jumla ya wanachama 15 ambapo 10 wasio wa kudumu hivi sasa ni Ubelgiji, Cote d'Ivoire, Equatorial Guinea, Jamhuri ya Dominika, Ujerumani, Indonesia, Kuwait, Peru, Poland na Afrika ya Kusini.

Wajumbe wa kudumu ni Uingereza, Ufaransa, China, Urusi na Marekani.

Mgawanyo wa idadi ya uwakilishi wa wajumbe wasio wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa maeneo ni nchi 5 kutoka Afrika na Asia, 1 kutoka Ulaya, 2 kutoka Amerika ya Kusini na Karibea na 2 kutoka nchi za Ulaya Magharibi na kwingineko.

**HABARI ZA UN**



Kikao cha Baraza la Umoja wa Mataifa. **PICHA: MTANDAO**

# Trump 'aupiga tafu' mpango wa Brexit ziarani nchini Uingereza

Na Nimi Mweta

RAIS Donald Trump wa Marekani, ametumia fursa ya kuitembelea Uingereza katika ziara rasmi kwa kumbukumbu ya miaka 75 ya kumalizika Vita Vikuu vya Pili duniani mwaka 1945, kwa kuipa nguvu hoja ya Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya (EU) hata kama haitaweza kufikia mkataba rasmi wa kuchukua hatua hiyo.

Ni mazingira ambayo wachambuzi wa habari nchini Uingereza bila kujali ni wa mrengo wa kulia au kushoto (waunga mkono Brexit bila mkataba na wanaopinga) wanakiri uingiliaji huo wa Rais Trump katika siasa nchini Uingereza umekuwa na athari kubwa kwa mjadala wenyewe.

Umeipa nguvu ajenda hiyo ambayo hata hivyo ilidhihirika kukubalika katika kupiga kura kuchagua wajumbe wa Bunge la Ulaya hivi karibuni, 'wakujitoa' wakishinda.

Jarida moja nchini Uingereza lilisema ziara hiyo (waliyoiona kama matembezi ya starehe kwa upande wa Trump na mkewe Melania) imefichua ukweli uliojificha, kuwa wapende wasipende, Uingereza ilikuwa inahitaji kutembelewa na kupewa somo na Rais Trump hivi sasa.

Jarida hilo lilimwelezea Trump kama kielelezo cha siasa za mrengo wa kulia zilizoipeleka Uingereza katika ajenda ya Brexit ambayo licha ya kutopatikana kwa mkataba unaokubalika kwa vyama vya siasa nchini Uingereza kwa pamoja (kujadili mapendekezo ya mwisho ya EU) bado imebaki wima. xxx

Kilichobaki sasa ni uchaguzi wa kiongozi wa chama tawala kuipitisha ajenda ya Uingereza kujitoa Oktoba 31 kama ilivyoamuliwa na EU kuwa tarehe ya mwisho, bila mkataba.

Katika mashindano ya nani atakuwa kiongozi wa chama tawala cha Conservative, ziara ya Rais Trump ilisaidia kumjenga Boris Johnson, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje akajiuzulu kutokana na kutoridhika na Uingereza kukubali masharti hasi kufikia mkataba wa kujitoa EU.

Mwingine ambaye alipata faraja kwa ziara hiyo ni Nigel Farage, ambaye tayari alishinda viti vingi Bunge la Ulaya akiwa na chama cha Brexit, ambacho hadi hivi karibuni kilikuwa kinaitwa 'National Front,' ambayo kimsingi ni nembo ya vyama vya mrengo wa kulia na mara nyingi ni vya kibaguzi au kifashisti.

Sera za Rais Trump nchini Marekani zinaonekana kama mfano wa kile vyama vya mrengo wa kulia barani Ulaya vinachotaka kufanya, kila mahali.

Waziri Mkuu Theresa May ambaye tayari amejiuzulu uongozi wa chama cha Conservative na amebaki madarakani kwa muda hadi kiongozi mpya achaguliwe alikuwa njia panda kuhusu maudhui ya ziara hiyo.

Kwa upande mmoja alipewa pongezi kwa jitihada za kufikia mkataba, lakini mkazo wa Trump katika kujitoa, na siyo katika kufikia mkataba au makubaliano ya kitaifa kwa suala hilo, kiasi fulani ulimwangusha.

Lakini katika kauli ya mwisho waziri mkuu huyo ni muumini madhubuti wa Brexit, na hakuwahi katu kukubali kuwa inafaa kuitisha kura nyingine ya maoni kuhusu suala hilo, baada ya kukosekana kwa mkataba wa kujitoa unaokubalika kitaifa.

Baadhi ya wachambuzi wa habari walianza kueleza wasiwasi kuwa ziara ya Trump itawapa ari wabunge wa Conservative 'kuchanja mbele'na kujitoa bila mkataba, hali ambayo wanadhani itampa nguvu kiongozi wa upinzani Jeremy Corbyn wa chama cha Leba.

Hata hivyo wasiwasi huo ulikuwa unagwaya kwa baadhi ya wachunguzi, kwani uchaguzi wa wajumbe Bunge la Ulaya uliashiria kujitoa kwa hali yoyote ile 'ndiyo habari ya mjini.' Si kura ya pili anayoitaka Corbyn.

Wapo wachunguzi waliokata tamaa wakimsikitikia waziri mkuu anayeondoka madarakani kuwa kwa miaka mitatu amekuwa ofisa mtendaji mkuu wa kutekeleza mpango usiofaa kitu wa Uingereza kujitoa EU.

Rais Trump alionekana kufanyia mzaha suala la May kuondoka madarakani kwa mkataba wake wa kujitoa EU kukwama bungeni, akisema anatumaini May 'atabakia kwa muda' wa kutosha kufikia mkataba mkubwa wa kibiashara na Marekani, ikabidi May acheke kwa hilo.

Hisia za kuchukizwa na siasa za Trump na uingiliaji wake katika suala hilo nyeti kote Uingereza zilizidisha mkwamo kisiasa nchini humo, kushindwa kuongoza.

Wachambuzi wa habari walishangazwa na jinsi Trump alivyopuuzia makundi ya waandamanaji kupinga ziara yake, huku akitupiana maneno makali na meya wa jiji la London, Sadiq Khan akisema ameshindwa kazi.

Alimshauri katika ukurasa wake wa twitter kuwa ingefaa aweke mkazo katika kupambana na uhalifu jijini London na siyo kuparurana na yeye, akimaanisha kuwa meya huyo siyo saizi yake anajihangaisha bure.

Baadhi ya waandamanaji waliweka mabango ya kuonyesha Trump asivyopendwa nchini Uingereza, wengine wakavaa kofia zenye picha ya meli ya kivita ya John S. McCain, shujaa wa vita vya Vietnam, Seneta wa Republican ambaye alipokufa Trump hakukaribishwa kufika kwenye mazishi yake, kielelezo cha chuki inayomhusu.

Kwa upande mwingine wachunguzi wa habari wanakiri kuwa tatizo la ziara ya Trump siyo nia ya kuingilia siasa za nchi hiyo ila ukweli kwamba Uingereza haijui ifanye nini kuhusu kujitoa Umoja wa Ulaya kwani hawakubaliani na chochote kile.

Kinachoonekana ni kuwa wanaotaka kujitoa ndio wengi, na hilo linajieleza katika ngazi ya hisia, siyo kufikia matarakimu ya uchumi yanayoridhisha pande tofauti, kwa mfano hata chama cha wenye viwanda nchini humo kimeeleza wasiwasi mkubwa kuhusu kujitoa bila mkataba.

Chama cha upinzani cha Labour kimeeleza kuwa kujitoa bila mkataba na kutokuwepo kwa makubaliano ya muungano wa forodha itakuwa 'balaa' kwa ajira nchini humo, lakini makundi ya waandamanaji na wapigakura hawasikii anachosema.

> Waziri Mkuu Theresa May ambaye tayari amejiuzulu uongozi wa chama cha Conservative na amebaki madarakani kwa muda hadi kiongozi mpya achaguliwe alikuwa njia panda kuhusu maudhui ya ziara hiyo.

Kingine kilichojitokeza katika ziara ya Rais Trump ni uhusiano maalum uliopo kati ya Uingereza na Marekani kuendelea na kuvuka mawimbi ya hivi sasa ya siasa nchini Uingereza na mtafaruku wa kujitoa EU.

Mapokezi na hotuba katika dhifa ya kitaifa Buckingham Palace, maskani ya Malkia Elisabeth II na kimsingi ndiyo Ikulu ya nchi hiyo, yalionyeshwa kwamba jiwe hilo la undugu katika vita ya pili vya dunia (na kwa kurudi nyuma, hata vita vya kwanza vya dunia) ni mkataba wa damu usioweza kuvunjika.

Pia kuna uwiano wa kitamaduni kwa raia wengi wa Marekani wanajiotambua nchi wanazotoka, na Rais Trump kwa mfano anatokea familia ya wahamiaji kutoka Scotland na kichekesho ni kuwa Scotland inapigania Uingereza ibaki EU.

Akiwa nchini Uingereza, Trump alikataa kukutana na Corbyn akisema kuwa anawakilisha siasa hasi kwa kiwango fulani, akamkaribisha mmoja wa watangaza nia ya kuwania nafasi ya uwaziri mkuu, Michael Gove na Farage, akitoa pendekezo kuwa Farage aongezwe katika timu ya wajadilianaji mkataba na EU.

Hapo pia kulikuwa na kichekesho kwani majadiliano hayo yalishaisha na ni Uingereza kujipanga kupitisha azimio lolote la kisiasa la kujitoa au kubaki katika umoja huo.

Isitoshe, endapo imeshindikana kupata mkataba unaokubalika pande zote Uingereza kwa timu iliyopo ya Theresa May, kuongezeka kwa wapambanaji wa mrengo wa kulia ni kuleta kichefuchefu EU kwa mapendekezo ambayo angeishauri Uingereza ipeleke hivyo kuhakikisha kuwa hakuna mkataba ungefikiwa.

Kilicho wazi ni kuwa marafiki hao wa Trump watakuwa na nafasi nzuri ya kutoa ushauri Uingereza ifanye nini kisera ikiondoka rasmi Oktoba 31, kwani EU haitaongeza siku katika suala hilo. Ni suala la kujipanga kisera, kujihami.



Maandamano nchini Uingereza dhidi ya ziara ya hivi karibuni ya Rais Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

UCHAMBUZI

## KUELEKEA UCHAGUZI S/MITAA;

# Hofu ya sheria inavyobana wanahabari

**Na Mwandishi Wetu**



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage. **PICHA: MTANDAO**

MWEZI wa Oktoba mwaka huu ni uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji unaofanyika miezi 12 kabla ya uchaguzi mkuu wa Rais na wabunge hapo mwakani (2020), kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Uchaguzi wa viongozi kwa mujibu wa Katiba ni moja ya nguzo za kidemokrasia na ni wajibu wa wananchi katika kudumisha na kuendeleza utawala wa kidemokrasia, haki za binadamu na usimamizi wa sheria.

Ni dhahiri kuwa uchaguzi hauwezi kufanikishwa bila nguvu ya vyombo vya habari kuanzia televisheni, redio, magazeti, blogi, TV na redio mtandaoni pamoja na ujumbe unaotumwa kwa njia za wasap, telegram, twita na instagram.

Wakati uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji umebakiza miezi minne, vyombo vya habari nchini vinalazimika kuingia kwenye kuripoti jukumu hilo vikiwa na macho manne.

Ninasema hivyo kwa sababu ya sheria na kanuni zinazosimamia sekta hiyo kuwa mwiba mchungu, ambao unaweza kivitumbukiza kwenye malumbano na vyombo vya dola.

Wakati huu vyombo vya habari vinapojipanga kuingia kuripoti taarifa za uchaguzi mkuu, masuala ya kufungiwa, kufutiwa leseni za usajili, kupewa adhabu na mamlaka za usajili kama Wizara ya Habari, Idara ya Habari –Maelezo na Mamlaka ya Mawasiliano ni mambo yanayotakiwa kuwa kwenye ncha za vidole vya wanahabari.

Wanahabari wanapoingia Oktoba kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji wanatakiwa kujichunga sana, kwani wanakabiliwa na sheria kama Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ('Media Services Act 2016) ambayo mwezi Februari ilipingwa na Mahakama ya Afrika Mashariki iliyotaka ifanyiwe marekebisho.

Sheria hii ina vipengele vyenye adhabu kali kwa wanahabari ikiangalia eneo la kashfa, uchochoezi na habari za upotoshaji.

Sheria hiyo inawaweka waandishi kwenye mazingira magumu hasa wakati huu wa kuandika taarifa za uchaguzi mkuu na hata ule wa serikali za mitaa na vijiji.

Sheria hii ya huduma za habari (Media Services Act) inawabana wanahabari na inawalazimisha kuwa makini zaidi kwa vile inampa rungu Msajili wa Magazeti ambaye pia ni Msemaji wa Serikali na ni Mkurugenzi Mtendaji wa Maelezo kwa kila mwaka kusajili upya magazeti kwa utashi wake.

Utashi huo unaweza wakati mwingine, pengine huu wa uchaguzi kukiweka chombo cha habari au gazeti kwenye wakati mgumu kwa hofu kuwa kinaweza kisisajiliwe iwapo kitachapisha taarifa ambazo Msajili hakuridhika nazo.

Hivyo magazeti yanaporipoti taarifa za uchaguzi mwezi Oktoba licha ya kujichunga yawe makini kutokana na ukweli kuwa sheria hiyo si rafiki na hasa yatakapoonekana yanajiingiza kwenye uchochezi, kashfa na kutoa taarifa zisizoaminika kwa upande wa serikali.

Katika sheria hiyo suala la maslahi ya taifa linatajwa na kupewa kipaumbele, ndiyo maana sheria inaelekeza kwamba Waziri wa Habari, anaweza kuzuia uchapishaji wa gazeti iwapo litaandika taarifa zinazokinzana na maslahi ya taifa.

Maslahi ya taifa ni jambo ambalo wanahabari mara kadhaa wametaka litolewe ufafanuzi ili kuwe na tafsiri inayoeleweka kwa wadau, kuepusha mikwaruzano na kutoelewana baina ya wana habari na sheria pamoja na kanuni zinazosimamia masuala ya habari.

Kuna sheria ya takwimu ya mwaka 2016 ambayo nayo inaelekeza mkuki kwa wanahabari.

Umakini unahitajika kwenye kutoa taarifa zinazohusu idadi ya wapigakura, mchakato wa upigajikura, kujumlisha kura, kuzihesabu na kupata idadi ya mwisho na kutangaza matokeo na washindi.

Umakini unahitaji kwenye hisabati kwa sababu sheria hii, haina huruma kwa masuala ya utoaji wa takwimu zisizoidhinishwa na serikali.

Kuona kinachoendelea kwenye uchaguzi au vituo vya upigaji kura hakutoshi bali ni lazima wanabari waripoti taarifa zilizothibitishwa na Wasimamizi wa Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) au mamlaka za kiserikali.

Pamoja na kwamba Watanzania wanalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 kwenye Ibara ya 18 inayotoa uhuru wa mawazo, kupata na kutoa habari, changamoto za kisheria na kanuni zinawafanya wanahabari kuwa na macho makali ili kujihakikishia kuendelea kuwepo.

Sheria na Kanuni za Uchaguzi ni suala lisiloepukika kwa wana habari wanaotarajia kuripoti uchaguzi mwaka huu pamoja na ule wa 2020.

**ATHARI ZA MITANDAO**

Wanahabari safari hii wanalazimika kujipanga kutokana na ukweli kuwa blogi, wasap, twita, telegram, instagram, TV na redio za mtandao zitakuwa zinatangaza matokeo ya uchaguzi, kabla ya kuingia kwenye magazeti na vyombo vingine rasmi vya TV na redio.

Ni wakati wa kuwa makini na taarifa kimtandao ambazo inaweza kutokea zikaandaliwa kutoka nje ya nchi na kutishia hatma ya vyombo vya habari.

Mathalani, matokeo yanaweza kutangazwa kwenye mitandao kuwa mgombea wa chama fulani ameshinda kama ilivyotokea kwa Zimbabwe.

Sehemu kubwa ya taarifa za kimitandao ilieleza kuwa mgombea wa upinzani Nelson Chamisa, ameshinda na kwamba chama tawala kilichokuwa kinawakilishwa na Emerson Mnangagwa, kimeanguka.

Taarifa hizo ambazo kwa hakika hazikuwa na ukweli zilitikisa dunia, kwa kuwa Chamisa alikuwa mgombea mchanga asiyefahamika hata ndani ya viunga vya mji Mkuu wa Harare, aliaminishwa kuwa ameshinda.

Kwa wanahabari ili kuendelea kuwepo kwenye tasnia wanalazimika kuzifuatilia taarifa hizo kwa kina na kusikiliza upande wa pili.

"Sheria hii ya huduma za habari (Media Services Act) inawabana wanahabari na inawalazimisha kuwa makini zaidi kwa vile inampa rungu Msajili wa Magazeti ambaye pia ni Msemaji wa Serikali na ni Mkurugenzi Mtendaji wa Maelezo kwa kila mwaka kusajili upya magazeti kwa utashi wake.

Kila anayetajwa, kutuhumiwa au kuhusishwa na kashfa apewe nafasi ya kusikika na kutoa maoni yake.

Kanuni ya kupata maoni ya pande zote ikitumika huenda visa vya kukwaruzana na NEC, dola na wagombea vikapungua kwenye chaguzi zijazo.

Kwa wanahabari huu ndio wakati wa kuiangalia, kuizingatia na kutafakari upya Sheria ya Makosa ya Mitandao kwenye kuandika habari za uchaguzi.

Kutuma taarifa, picha, matokeo na habari za uchaguzi ambazo hazijathibitika kupitia mitandao, zinaweza kutishia hatima ya chombo na wanahabari watakaohusika.

Homa inapopanda kwa wanahabari wakati uchaguzi unapokaribia, umma usidhani kuwa uko nje ya mstari wa sheria, raia wengine nao wanaweza kubanwa.

Lakini ili kuondoa hofu hizo ni wakati wa wadau, taasisi na wagombea waanze kuwaelimisha Watanzania juu ya masuala ya uchaguzi, sheria na mambo muhimu kwa kuwa sheria hizi pamoja na kuwabana wanahabari hazitaawacha raia wengine salama.

Elimu ya uchaguzi inapotolewa ni muhimu umma ukaelezwa kuhusu sheria hizo na athari zake ambazo hazitawaacha Watanzania wengine linapokuja suala la jinai.

Wakati wa kutoa elimu hiyo wananchi wafunzwe kuhusu katiba na haki ya kupiga kura, kanuni na maadili ya uchaguzi, sheria za uchaguzi, Tume za Uchaguzi za NEC na ZEC kwa upande wa Zanzibar.

# China, Russia zapanua ushirikiano kukabili uhasama wa Marekani

**Na Anil Kija**

HATUA za utawala wa Rais Donald Trump wa Marekani dhidi ya China kwa upande mmoja na Russia kwa upande mwingine zimefanya nchi hizo kujenga kwa nguvu zaidi ushirikiano kati yao kuwa wa kimkakati zaidi na wa muda mrefu.

Hata hivyo, wachunguzi wa habari wanajiuliza ni kwa kiasi gani ushindani wa jadi kati ya nchi hizo mbili utafunikwa na hitaji la kushirikiana dhidi ya Marekani.

Wanajiuliza kama mwelekeo wa kiuchumi wa nchi hizo, ambao unaelekea soko la kimataifa, unaweza kubadilika kuelekea katika masoko au mitaji ya ndani ya nchi hizo.

Mwelekeo huu ulianishwa kwa nguvu wakati wa ziara ya hivi karibuni ya Rais Xi Jinping wa China nchini Russia, ambako kila aina ya dhihirisho la urafiki ilionekana katika mazungumzo yake na Rais Vladimir Putin.

Kiongozi huyo wa Russia alisema uhusiano kati ya nchi hizo mbili haujawa bora kama ulivyo sasa, mahusiano ambayo baadhi ya wachunguzi wa siasa za kimataifa wangependelea uchukue mkondo kuwa mhimili madhubuti dhidi ya dunia inayotawaliwa na matakwa ya Marekani.

Mchambuzi mmoja alishangaa kuwa uhusiano huo hautiliwi maanani katika vyombo vya habari vya nchi za Magharibi, akimaanisha kuwa ni kupuuzia hatari ya wazi.

Ziara ya Rais Jinping ilifuatana na ziara ya Rais Trump nchini Uingereza wakati wa sherehe za kumbukumbu ya miaka 75 ya kumalizika kwa Vita Vikuu vya Pili duniani, 1945 ambako kwa upande fulani Marekani na Uingereza zilikuwa washirika maalum.

Barani Ulaya kulikuwa zaidi na makundi ya ukombozi yenye silaha, kwani serikali zilizokuwapo zilikuwa za kifashisti au zimewekwa tu na majeshi ya Ujerumani baada ya kuteka maeneo yote kuacha Uingereza, au nchi zilizoshikwa na washirika wake kama Italia, Ureno na Hispania.


Ni zama za kale lakini wapo bado mababu walioshiriki katika vita hivyo na kina bibi waliotibu watu, wanaoenziwa.

Jambo ambalo bado lilikuwa linawatatanisha wachambuzi ni kiasi gani China na Russia zinaweza kujenga mahusiano ya kiuchumi ya kupunguza utegemezi wao kwa nchi za Magharibi na hasa Marekani.

Yaani kuwezesha ushawishi wa Marekani na uwezo wa kugeuza mkondo wa siasa au sera katika nchi nyingine kupungua.

Hakuna uhakika kuwa ziara ya Jinping nchini Russia ilitoa majawabu kwa suala hilo, au iliendeleza maeneo ya ushirikiano yaliyokuwapo, yakapewa nafasi zaidi, na si kubadili kimsingi mpangilio wa mahusiano hayo.

Mojawapo ni kupanuliwa kwa shughuli za kiteknolojia za kampuni ya simu Huawei ya China iliyofungiwa katika taasisi za kiserikali Marekani na kwingineko barani Ulaya. Itatoa leseni za simu za 5G inazotengeneza.



Rais Xi Jinping wa China (kulia), akiwa na Rais wa Russia Vladimir Putin. **PICHA: MTANDAO**

> Ziara ya Rais Jinping ilifuatana na ziara ya Rais Trump nchini Uingereza wakati wa sherehe za kumbukumbu ya miaka 75 ya kumalizika kwa Vita Vikuu vya Pili duniani, 1945 ambako kwa upande fulani Marekani na Uingereza zilikuwa washirika maalum.

Rais Jinping alikuwa muwazi kiasi cha kushangaza akizungumzia mahusiano yake na Rais Putin, aliiambia shirika la habari la Russia TASS kuwa ana uhusiano maalum na Rais Putin ambao ni wa hali ya juu ukilinganisha na marais wengine anaoshirikiana nao duniani.

Alisema ni rafiki yake mkubwa na anauthamini sana urafiki wao, jambo ambalo si la kawaida kwa kiongozi wa nchi nyingine kusema kuhusu anakotembelea, lakini inaelekea kuwa alikuwa anasema kweli.

Wakati Uingereza na Marekani zikisherehekea kumalizika kwa vita vikuu vya pili, China na Russia zilikuwa zinasherehekea miaka 70 ya mahusiano ya kibalozi, yaliyoanza Oktoba 1949 wakati China ilipokamilisha mapinduzi ya Kikomunisti, mfano wake bora ukiwa ni Urusi hiyo.

China na Russia zimeshirikiana katika masuala kadhaa ya kimataifa dhidi ya Marekani katika Baraza la Usalama la UN, kwa mfano kuhusu uvamizi wa Marekani, Uingereza na washirika wao nchini Iraq mwaka 2003 na hivi karibuni kuhusu vita vya Syria.

Pia kuna suala la mparaganyiko wa kisiasa nchini Venezuela ambako nchi za Magharibi zimemtambua Juan Guidao (mwenyekiti au Spika wa Bunge ambaye mahakama nchini humo imemvua wadhifa huo) kama rais halali wa Venezuela.

China na Russia zinamuunga mkono Rais Nicholas Maduro; jeshi liko nyuma yake.

Wakati viongozi wa Russia na China wanaongeza ushirikiano kujenga mhimili wa kushindana na Marekani na kuimarisha mifumo ya uchumi na hata siasa ambayo inakinzana na matakwa ya Marekani (kama siyo nchi nyingine za Magharibi) ustawi wa mkakati huo upo mashakani.

Moja ya mahitaji ya kujengeka kwake ni kuwapo kwa nchi nyingi duniani zinazochukua mkondo kama huo, wakati ambapo zilizopo siyo lazima ziwe na ushirikiano mzuri na mhimili huo mpya wa mahusiano ya kimataifa.

Saudi Arabia kwa mfano ni adui mkubwa wa Iran katika Mashariki ya Kati na mshirika wa Marekani, licha ya wabunge nchini Marekani kukerwa na mfumo wake wa utawala na kukiukwa kwa haki za binadamu, ila wanaangalia kando kuhusu vita yake ya Yemen.

Moja ya maeneo ambako uhusiano wa Russia na China unaendana kiasi fulani na mahitaji mapana kimataifa ni nafasi ya vyombo vya kimataifa na hasa Umoja wa Mataifa na mashirika yake katika kutatua matatizo duniani.

Hata Malkia Elisabeth II alieleza dhamira hiyo katika hotuba ya hafla ya uwepo wa Rais Trump ziarani Uingereza, ambaye ameonyesha kubeza au kupunguza nafasi ya vyombo hivyo katika mkakati wa sera za nje wa Marekani.

Pia kuna wasiwasi kuhusu uthabiti wa umoja wa kujilinda wa NATO chini ya Rais Trump kwani kuna migongano mingi na nchi wanachama, kwa mfano Ujerumani, na kwa njia tofauti hata Ufaransa.

Ambacho kinahitaji ufafanuzi au kunoa bongo zaidi katika mahusiano ya Russia na China ni jinsi nchi hizo zinavyoweza kuendeleza ajenda ya malengo ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa au mkakati mzima wa utandawazi ambao China imeujenga kupitia Mpango wa Ukanda na Barabara.

Ni mikakati ya ushirikiano binafsi kati ya China na nchi husika ambao hauhitaji kusimamiwa au kupitishwa na taasisi zozote za kimataifa, na wengi kati ya wanaoshiriki mpango hawafanyi hivyo kuunga mkono China dhidi ya Marekani ila kama sehemu ya kupanua wigo wa ushirikiano kibiashara.

Ni Russia ndiyo ina uwezo kuchota mkakati wa kupingana na Marekani kama ilivyo Iran, lakini kuna tatizo la uthabiti uchumi wa nchi hizo Marekani ikiweka vikwazo.

Udhaifu wa ushirikiano kati ya China na Russia kubadili chochote katika medani ya kimataifa unadhihirishwa na hali halisi kuwa kimsingi ni dola ambazo zinasimama upande wa uhuru wa nchi kuendesha mambo yao wenyewe, zisiingiliwe na Marekani au mataifa mengine.

Matokeo yake ni kuwa Marekani na washirika wake wanakuwa wa kwanza katika kuunga mkono harakati za demokrasia na mapinduzi yakijitokeza, kama ilivyo nchini Sudan hivi sasa, wakati China na Russia kwa jadi zitasimama na serikali za muda mrefu kutokana na mahusiano, siyo mabadiliko.

Wakati Rais Jinping anamaliza ziara yake huko Russia, wananchi wa Hong Kong walikuwa katika maandamano kupinga muswada wa sheria uliopelekwa mbele ya Baraza la Kutunga Sheria la jiji hilo ambalo Uingereza iliirudishia China mwaka 1997 kwa makubaliano maalum.

Ni kutaka watuhumiwa wa uhalifu kuhusiana na usalama wa taifa warudishwe Bara endapo wanakamatwa Hong Kong, ambako kuna viwango tofauti vya utawala wa sheria na haki za binadamu.

Umoja wa kimkakati wa Russia na China ni wa muda tu, kwani nchi zote hizo zinaelekea mabadiliko.



# Machinga washangaa ushuru wa h'mashauri

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wadogo jijini Mbeya wamedai licha ya kuwa na vitambulisho vilivyotolewa na Rais John Magufuli, lakini bado wanatozwa ushuru na Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Wakizungumza juzi kwenye mkutano na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, walisema uongozi wa Jiji la Mbeya unaendelea kuwatoza ushuru na kuwalazimisha kuingia mikataba ya kibiashara, wakati tayari wanavyo vitambulisho vya Sh. 20,000.

Mmoja wa wafanyabiashara hao kutoka Soko la Ikuti Kata ya Iyunga, Grace Mwasumbi, alimueleza Mwenyekiti huyo wa CCM kuwa wanaendelea kutozwa ushuru na kulazimishwa kuingia kwenye mikataba ya kibiashara na baadhi ya watumishi wa Jiji wakati tayari wanavyo vitambulisho ambavyo vinawaruhusu kufanya biashara zao bila kutozwa gharama zozote.

Grace alimuomba Nsomba kuingilia kati suala hilo kwa madai kuwa linawaumiza wajasiriamali ambao wana mitaji midogo ya kuendesha biashara zao.

Sister Mwembe, mjasiriamali wa Ilembo Kata ya Iwambi, alisema wanalazimika kufunga biashara zao ili kukwepa kulipa tozo hizo, na kwamba wakati mwingine hutishia kufunga wasipolipa.

Akizungumzia malalamiko ya wafanyabiashara hao, Mwenyekiti Nsomba alishangazwa na ujasiri wa watumishi hao kukaidi agizo la Rais Magufuli la kuendelea kuwatoza ushuru wajasiriamali ilhali wana vitambulisho, na kwamba chama hicho hakitawavumilia watendaji wanaoikwamisha serikali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema ni kosa kwa mtumishi kukaidi agizo la Rais, na kwamba anafanya uchunguzi kubaini watendaji waliohusika ili kuchukua hatua za kisheria.

# Hospitali yaomba serikali kuajiri wakalimani kusaidia wenye uziwi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani Kanda Mbeya, imeiomba Wizara ya Afya kuajiri wakalimani ambao watasaidia kutoa huduma ya ukalimani wa lugha ya alama kwa wenye ulemavu wa kusikia, ili kurahisisha huduma kwenye kundi hilo.

Hayo yalisema na Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, wakati wa hafla ya kutimiza mwaka mmoja tangu kuanza kutolewa kwa huduma ya ukalimani kwenye hospitali hiyo, ambayo ilihudhuriwa na viziwi sambamba na utoaji elimu kuhusu afya.

Dk. Mbwanji alisema waliamua kuanzisha huduma ya ukalimani hospitalini hapo baada ya kubaini changamoto zilizokuwa zikiwakabili wenye uziwi wanapohitaji huduma za matibabu.

Alisema uongozi wa hospitali na wadau wengine wakiwamo wenye uziwi walishirikishwa na kufikia muafaka wa kuanzisha huduma hiyo, na kuwa mpaka sasa wenye uziwi wanapata matibabu vizuri ukilinganisha na awali.

"Tangu kuanzishwa kwa huduma ya ukalimani hospitalini hapa jumla ya wenye uziwi ambao ni wagonjwa 420 sawa na wagonjwa 14 kila siku wamepatiwa matibabu kwa kutumia mkalimani ambapo kati yao wengine walifanyiwa upasuaji, huduma hii ni nzuri na muhimu sana katika kundi hili," alisema Dk. Mbwanji.

Aidha, alisema hospitali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imejipanga kuongeza kuajiri wakalimani wengine ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa wanaohitaji huduma, na kwamba hospitali hiyo ndio inayotegemewa kwa Nyanda za Juu Kusini.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye uziwi mkoani Mbeya, Tusajigwe Mwalwega, alipongeza Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya kwa kutoa huduma ya ukalimani, na kwamba imewasaidia kuwa huru kujieleza na kupata huduma sahihi.

Alisema awali walikuwa wanapata changamoto ya mawasiliano kati ya mgonjwa na daktari kwa sababu ya kutoelewana, lakini kwa sasa wanahudumiwa vizuri na hakuna foleni.

Aliiomba serikali kuajiri wakalimani na kwenye taasisi nyingine za umma ili kuwasaidia kupata huduma bila changamoto yoyote ya mawasiliano kama ilivyo kwa Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya.

Tusajigwe alisema tangu kuanza kutolewa kwa huduma ya ukalimani katika hospitali hiyo, kumewezesha wenye uziwi kutoka maeneo mbalimbali kupata huduma za afya kwa urahisi.




Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evord Mmanda (kulia), akipokea moja ya karatasi yenye herufi za maelekezo ya jinsi ya kujifunza lugha ya alama kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), tawi la Mtwara, Farida Selemani, baada ya kufungua mafunzo ya siku moja ya lugha ya alama yaliyoratibiwa na chama hicho, wilayani humo juzi. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# YWCA yawakumbuka wanaume wagane

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA


UMOJA wa Wanawake wa Kikristo (YWCA) katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wameshauri kuanzishwa kwa umoja wa wanaume wagane ili changamoto zao ziweze kutatuliwa kama ilivyo kwa wanawake wajane.

Hayo yalisemwa hivi karibuni wakati wa maadhimisho ya Kanda ya YWCA, ambayo hufanyika mara moja kila mwaka, ambapo walisema wamebaini kuwa wanaume waliofiwa na wenza wao wana changamoto nyingi ambazo hazijatafutiwa ufumbuzi, hivyo ukianzishwa umoja wao utasaidia kutatua matatizo yao.

Mwanachama wa umoja huo, Victoria Mwakatuma, aliiambia Nipashe kuwa mbali na kupaza sauti kwa wanaume ili changamoto zao zisikike kama zinavyosikika za wanawake wajane, wanatoa huduma mbalimbali ikiwamo elimu ya kujitambua na kujitathmini ambayo imesaidia wanawake wengi kuanzisha shughuli zao za kujiingizia kipato. "Umoja huu wa wanawake umekuwa na manufaa makubwa kwetu kwani umetuunganisha pamoja na kutufanya ndugu ambapo kila mmoja anabeba mzigo wa mwenzio yanapotokea matatizo, tumekuwa ni mfano wa kuigwa na kinamama wengine kwa sababu tunasaidiana na tumeanzisha miradi, tunashauri nao kinababa waanzishe umoja kama huu ili uwasaidie," alisema Victoria.

Mwenyekiti wa Kanda wa YWCA, Oliva Asukenye, alisema umoja wao umekuwa chachu ya maendeleo katika makanisa yao kwa kuwa wao ndio hubeba majukumu mengi ya kanisa ikiwamo kufanya maombi. Alisema ili kuongeza nguvu za kumtumikia Mungu katika nyumba za ibada, ipo haja ya kuanzisha umoja wa wanaume ili nao waweze kutatua changamoto zao.

Ofisa Elimu Kata ya Sisimba, Dickson Simkwembe, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwa niaba ya mdau wa maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela, aliwashauri kinamama hao kudumisha umoja na mshikamano.





# Rushwa serikali za mitaa yaanza kupungua

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

VITENDO vya kutoa na kupokea rushwa kwenye ngazi ya serikali za mitaa vimeanza kupungua baada ya wananchi kupatiwa uelewa na kuhoji masuala mbalimbali kwenye miradi ya maendeleo. Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja Mradi wa Utawala Bora na Kuzuia Rushwa unaojulikana kama 'Tuungane Kutetea Haki',

Maria Kayombo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuhitimishwa kwa mradi huo ambao ulitekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2017-2019. Mradi huo unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya na Shirika la Konrad Adenaur Stiftung (KAS) la Ujerumani kwa gharama ya Sh. bilioni 2.5.

Alifafanua kuwa kupitia mradi huo wananchi sasa wameanza kuhoji, kushiriki mikutano, kufuatilia miradi na rasilimali zao.

"Kutokana na ushiriki wa wananchi na uwazi kuwapo moja kwa moja mianya ya rushwa imeanza kupungua," alisema.

Kayombo alisema kupitia mradi huo wamekuwa wakishirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) hatua iliyosaidia wananchi kutoa taarifa za matukio ya rushwa. "Kabla ya mradi kulikuwa na malalamiko ya kushamiri kwa rushwa serikali za mitaa baada ya kubuniwa mradi huo, tulijielekeza kuwajengea uwezo mashirika ya hiari pamoja na wanajamii kuhusu kuhoji mapato na matumizi hususan mchakato wa kutathmini na kutekeleza miradi," alisema. Alisema wananchi 2,130 walichaguliwa kwenye maeneo ya mradi walihusika kikamilifu na walipewa elimu na kushiriki majadiliano kuhusu rushwa kati ya wananchi na viongozi wa serikali za mitaa.

"Mradi huu ulibuniwa na kutekelezwa na Mashirika ya KAS, Chama cha Walimu wa Uraia Tanzania (CETA) na Action for Democracy and Local Governance (ADLG), tumepata mafanikio makubwa na umefanyika kanda mbili kusini na kanda ya ziwa na ulikuwa kwenye mikoa saba ambayo ni Mara, Kagera, Simiyu, Geita, Lindi, Pwani na Ruvuma na kata 1065 zimefikiwa," alisema.

Katika hatua nyingine, Kayombo alisema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uhitimishaji wa mradi huo, jijini hapa.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG), Margaret Sitta (katikati), akizungumza na ujumbe kutoka Bunge la Rwanda pamoja na wajumbe wa umoja huo, katika kikao kilichofanyika jijini Dodoma jana. Kushoto ni Spika wa Bunge la Rwanda, Mukabalisa Donatille na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Huduma usafiri wa anga kuboreshwa

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, amesema serikali itaendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga ikiwamo kuongeza magari ya zimamoto kwenye viwanja vya ndege nchini ili kuendana na viwango vya kimataifa.

Kwandikwa alitoa kauli hiyo jana wakati wa kufungua mkutano wa 23 wa Baraza Kuu la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), uliofanyika jijini hapa.

Alisema katika kuhakikisha utoaji wa huduma ya usafiri wa anga kwenye viwanja vya ndege nchini inafikia viwango vya kimataifa, serikali imeendelea na kuchukua hatua za kuviboresha viwanja hivyo, ili kuendana na viwango vya kimataifa.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema jengo jipya la Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere la Terminal III lipo katika hatua za mwisho kukamilika na kwamba ni jitihada za serikali kuhakikisha viwanja hivyo vinaboreshwa.

Alisema kupitia bajeti ya mwaka 2019/20, serikali itaendelea kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kusaidia kutoa huduma katika viwanja vya ndege.

Kwandikwa alisema kupitia bajeti hiyo wataboresha na kujenga viwanja vya ndege katika baadhi ya maeneo ili kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi wa ndani na nje ya nchi.

Naye, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Serikali Kuu (Tughe), tawi la mamlaka hiyo, Nasibu Elias, alisema sekta ya anga inakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi hafifu.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni maslahi kwa watumishi na kuomba kuongezea ili kuwapa ari na motisha wafanyakazi katika utendaji.

"Mikutano mahali pa kazi ni muhimu maana ndio sehemu pekee ambapo wafanyakazi tunapata muda wa kupitia na kujadili changamoto zinazotukabili," alisema.

Mkurungenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa TAA, Renatus Msangila, alisema mkutano huo wa baraza utapitia na kujadili mpango wa Bajeti Kuu ya mwaka ujao wa fedha.

Alisema pia watajadili ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa majengo na viwanja vya ndege ili kusaidia kuboresha huduma za usafiri huo ambao unachangia kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi.

# Wajasiriamali wapewa somo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAJASIRIAMALI wametakiwa kutengeneza bidhaa zenye ubora ili kwenda sambamba na ushindani wa soko lilipo nchini na nje ya nchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kaimu Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), jijini Dodoma, Stephano Ndunguru, wakati akifunga mafunzo ya usindikaji vyakula yaliyoandaliwa na shirika hilo.

Ndunguru alisema katika biashara hakuna uchanga, kinachotakiwa ni wasindikaji kutengeneza bidhaa zilizo bora ambazo zitaleta ushindani

dhidi ya wajasiriamali pale watakapokuwa katika sehemu ya utafutaji soko.

Alifafanua zaidi ya kuwa ili kuendana na soko lililopo wajasiriamali wanatakiwa kufuata misingi iliyobora katika utengenezaji bidhaa zao, ikiwamo kuepuka kuchakachua kwa sababu kutasababisha bidhaa hizo kukaa kwa muda mrefu sokoni.

Ndunguru alisema ni vyema wakafuata misingi bora katika usindikaji ili kuzalisha bidhaa zenye ubora ambazo zitawaletea faida katika biashara za ujasiriamali wanazofanya.

Aliwataka kuweka jitihada katika kutafuta masoko ya bidhaa zao jambo ambalo litawasaidia kwa kiasi kikubwa kuuza kwa haraka hasa zitakapokuwa na soko.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Ofisa Uendelezaji Biashara kutoka Sido, jijini Dodoma, Crispin Kapinga, aliwataka wajasiriamali kujitofautisha na bidhaa za watu wengine katika soko ili waweze kupata wateja kwa haraka zaidi, ikiwamo kutowapoteza.

Alisema kinachotakiwa kwa wajasiriamali ni kuangalia katika soko ni bidhaa gani haipo na wao kuchangamkia fursa ya kwenda kuitengeneza.

Katika mafunzo hayo washiriki walijifunza namna bora ya kusindika bidhaa mbalimbali zikiwamo karanga, vitunguu swaumu, unga mchanganyiko, pamoja na namna ya kuingia sokoni ikiwamo kuhimili ushindani wa soko lililopo.





Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid (kushoto), akisalimiana na wageni wa Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Said Muhammed Dimwa, waliofika katika baraza hilo, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wajumbe wachachamaa kupuuzwa vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi, nusura wagomee bajeti ya Wizara ya Vijana, Sanaa na Michezo kwa maelezo kuwa ni kidogo isiyoweza kukabiliana na changamoto za vijana.

Kufuatia hali hiyo waliipitisha kwa mbinde baada ya wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi, kuhoji sababu za Idara ya Vijana kutengewa fedha kiduchu.

Baraza lilihoji sababu za Idara ya Vijana kutengewa shilingi bilioni moja kinyume na makadirio ya mwanzo yaliyoafiki kuwatengea bilioni tatu.

Mwakilishi wa Viti Maalumu Kaskazini Pemba ( Vijana), Viwe Khamis, alikasirishwa na kitendo cha vijana kutengewa fedha kidogo kinyume na matarajio yao, akisema fedha hizo hazitoshi katika kuwaendeleza vijana kuibua na kufanikisha miradi ya kiuchumi.

''Tumekubaliana vijana watengewe shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kazi za miradi ya kiuchumi, lakini tumesikitishwa kusikia kwamba bajeti yao ni shilingi bilioni moja tu . Kiasi hiki ni kidogo mno hakitoshi," alisema Khamis.

Alichachamaa kuwa vijana wamedharauliwa wakati ndiyo tegemeo la taifa katika kila jambo kuanzia kuendeleza uchumi, nguvu kazi, wapiga kura na watengeneza ajira.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alisema katika jimbo lake vipo vikundi vya wajasiriamali 25, lakini hakuna kikundi kilichonufaika na fedha za vijana katika miradi ya ujasiriamali.

Aliitaka wizara hiyo kuhakikisha fedha za mikopo za vikundi zinawafikia wajasiriamali moja kwa moja katika miradi ya kiuchumi.

# Ukatili kwa watoto wakithiri Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema ukatili dhidi ya watoto wa kike Zanzibar, ni jambo linaloongezeka kila siku.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari wanaohudhuria mafunzo kuhusu haki za mtoto, yaliyoandaliwa na jumuiya ya waandishi wa habari za maendeleo Zanzibar (Wahamaza) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF).

Alionya kuwa Zanzibar haitafikia malengo endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN) kama ukatili wa kijinsia utaongezeka na kuathiri wanawake.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria kali ikiwamo ya mwenendo wa makosa ya jinai na ushahidi, bado matukio hayo yamekuwa yakiendelea siku hadi siku yakifanywa zaidi na ndugu wa karibu wa watoto wanaodhulumiwa haki zao.

Aidha, waziri huyo aliwaomba wahariri na waandishi wa habari kusaidia mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia kwa jamii ya watoto ambao umekuwa ukirudisha nyuma maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ipo tayari kushirikiana na wahariri na vyombo vya habari nchini kuona kwamba ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake unatokomezwa moja kwa moja," alisema.

Akieleza kuhusu taarifa za utafiti zilizofanywa na UNICEF, alisema udhalilishaji wa watoto walio na umri wa miaka miwili unaongezeka kwa kasi kwani kiasi cha watoto bilioni, wanaodhalilishwa duniani kati ya miaka miwili hadi 17.

"Kwa upande wa Zanzibar hali inasikitisha kwani vitendo vingi vya udhalilishaji wa watoto vinafanywa na watu wa karibu na familia zao," alisema waziri huyo.

Mwakilishi wa UNICEF Zanzibar, Maha Damaj, alisema wapo tayari kuunga mkono mpango mkakati wa miaka mitano wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambao unatekelezwa na SMZ ambao lengo lake kubwa ni kumlinda mtoto.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanahabari za Maendeleo Zanzibar -Wahamaza, Salim Said Salim, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo ili kuwajengea uelewa wanahabari pasipo na usumbufu na kutambua kwa undani haki ambazo zinazostahiki kupatiwa mtoto.

# Mwenge watajwa kukuza mshikamano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imeeleza mbio za Mwenge wa Uhuru kuwa chanzo cha kuwaunganisha Watanzania kujiletea umoja na mshikamano pamoja na kuhamasisha miradi ya maendeleo.

Hayo yalisemwa na Kaimu Waziri wa wizara hiyo, Mahmoud Thabit Kombo, wakati akiwasilisha makadirio, mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisema mbio za Mwenge wa Uhuru zimerudisha hamasa ya mshikamano na wananchi kupenda nchi yao, huku ukiweka pembeni itikadi na tofauti za kisiasa nchini.

Alisema tangu mwenge huo kutembezwa katika mfumo mpya wa kuzishirikisha wizara za vijana za pande mbili za Muungano, mshikamano na umoja umeimarika kwa kiasi kikubwa.

Alisema Zanzibar ilishiriki kikamilifu katika mbio hizo kitaifa mwaka 2018 kuanzia uzinduzi wake huko Geita uliofanyika Aprili 2018.

Aliyataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Mbio za Mwenge wa Uhuru unaofanyika kwa pamoja kuwa ni kuzinduliwa kwa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na hospitali mijini na vijijini.

''Miradi mingi ya maendeleo ikiwamo kuwekwa mawe ya msingi hufanyika katika kipindi cha Mwenge wa Uhuru na hivyo kuleta hamasa za maendeleo, faraja kwa kuwa inalenga kuwanufaisha wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,'' alisema Kombo.

Aidha, alisema wizara inaendelea na kazi ya kuratibu mabaraza ya vijana nchini ambayo yameanza kuleta mabadiliko makubwa kwa kuwashirikisha vijana wengi kuibua miradi ya maendeleo.

Alisema jumla ya vijana 16,340 wameunganishwa na mabaraza ya vijana Unguja na Pemba kutoka idadi ya awali ya 13,064.

Aidha, Kombo alisema mabaraza ya vijana hayapo kisiasa kama inavyodhaniwa na wananchi wengi kwani baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiwakataza wananchi na wanachama wao kujiunga nayo.

"Haya mabaraza ya vijana hayapo kwa dhamira ya kisiasa kama wanavyodhani wananchi wengine pamoja na wanasiasa...Tunataka kuwaunganisha vijana kupiga hatua kwenye maendeleo na kupambana na umaskini kwa kuibua fursa za kibiashara na kuzifanyia kazi," alisema Kombo.

Waziri Kombo aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh. bilioni 9.6 kwa ajili ya kazi za kawaida na shughuli za maendeleo pamoja na utekelezaji wa programu za kuimarisha vijana.

# Serikali kukamilisha kanuni kudhibiti utoaji dawa

**Na Mashaka Mgeta**

SERIKALI inakamilisha mchakato wa kuunda kanuni ya usimamizi na udhibiti wa vyeti vya kutoa dawa ikiwa ni sehemu ya kuboresha sekta ya afya nchini.

Mfamasi kutoka Baraza la Famasi Tanzania, Timotheo Ngoda, alisema hayo alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa waandishi wa habari ulioandaliwa na Chama cha Wafamisi (PST) jijini Dar es Salaam juzi.

Mkutano huo ulikuwa mahususi kwa ajili kutangaza maadhimisho ya Siku ya Wafamasi inayoanza leo (Jumanne) nchi nzima na kufikia kilele chake Juni 16, mwaka huu.

Ngoda alisema serikali kupitia baraza hilo inatambua changamoto mbalimbali zinazoikabili tasnia ya famasia, miongoni mwake ni matumizi yasiyo sahihi na utoaji holela wa vyeti vya dawa.

"Kwa hali hiyo baraza letu lipo katika hatua za mwisho za uundaji wa kanuni ya kudhibiti maelezo ya dawa kuanzia kutoka kwa daktari hadi utoaji wake kwa mgonjwa," alisema.

Kwa mujibu wa Ngoda, miongoni mwa mambo mengine, kanuni hiyo itagusia kuwapo kwa taarifa zitakazojazwa na wahusika na kuelezea namna maelezo yanavyopaswa kutoka hadi kufanikisha upatikanaji wa dawa.

Rais wa PST, Issa Hango, alisema maadhimisho ya siku wa wafamasia itakuwa sehemu ya fursa kwa umma kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu tasnia hiyo na umuhimu wake kwa jamii.

Hango alisema maadhimisho hayo yenye kauli mbiu inayosema 'mfamasia wako ni zaidi ya utoaji dawa', itaadhimishwa jijini Dar es Salaam kwa uelimishaji jamii na kutoa huduma ya dawa ya minyoo bila malipo.

Alisema huduma hizo zitazotolewa kwa ushirikiano na washirika wao, Chama cha Wanafunzi Wafamasia (TAPSA) na Chama cha Wafamasia Wanawake (TAWPA) kwenye maeneo ya Kibo Complex-Mbezi, Mlimani City na viwanja vya Mwembe Yanga vilivyopo katika Manispaa ya Temeke.

Baraza la Famasia litaadhimisha katika kanda tano za mashariki (Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Temeke na Hospitali ya Taifa Muhimbili), kati (Hospitali ya Rufani ya Mkoa) na kaskazini (Kituo cha Afya Levolosi).

Sehemu nyingine ni kanda ya Nyanda za Juu Kusini ( viwanja vya Kabwe) na kanda ya Ziwa (viwanja vya Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando).

Hango alisema wananchi wanapaswa kujitokeza kwa wingi kushiriki maadhimisho hayo na kuyatumia kama fursa ya kupata elimu kuhusu tasnia ya famasia.

Kwa mujibu wa Hango, wafamasia wana umuhimu kutokana na ukweli kwamba wana dhamana ya kutafiti, kugundua, kutengeneza, kuhifadhi, kusafirisha na kutoa dawa kwa wagonjwa.



Wajasiriamali wakimsikiliza Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Jaffari Kunambi (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa semina ya siku tano ya ujasiriamali kwa wafanyakazi na wakazi wanaoizunguka Shule ya Misheni Bethel, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCT kuwawezesha wanawake kiuongozi

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

JUMUIYA ya Kikristo Tanzania (CCT) kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), imezindua mradi unaofahamika kwa jina la "Mwanamke jasiri" utakaosaidia kuinua uchumi wa wanawake na wasichana wa Mkoa wa Mara, ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha kuhusu siasa, uongozi na haki zao.

Akizungumza hivi karibuni mjini Musoma wakati wa uzinduzi wa mradi huo ambao ulioanza kutekelezwa tangu Januari Mosi, mwaka huu mkoani hapa, Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa mradi huo, Ambonisye Asumile, alisema mradi huo hautatoa mikopo ya aina yoyote isipokuwa utashughulika na utoaji wa elimu kupitia vikundi vya kuinuana kiuchumi ambavyo vinatambulika katika kila halmashauri husika.

Asumile alisema mradi huo una wasimamizi na wawezeshaji ngazi ya wilaya (DF) waliowekwa na CCT ambao watakuwa sehemu muhimu katika kuhakikisha wanashirikiana na vikundi pamoja na viongozi ngazi ya mkoa.

Alisisitiza kuwa mradi huo utakuwa sehemu muhimu ya kuongeza nguvu na kasi ya kuisaidia serikali katika kuyafikia maendeleo chanya hasa kwa wanawake na wasichana kwa ujumla.

"Mradi huu utawaunganisha wanawake walio katika vikundi ambavyo vitakuwa katika mradi wetu, na taasisi mbalimbali za fedha kupitia serikali, na kuwapa elimu ya kuzijua fursa mbalimbali za ujasiriamali, kiuchumi na kushiriki kutatua changamoto za masoko pamoja na mitaji ili kuwakwamua kiuchumi," alisema Asumile.

Aidha, Asumile aliongeza kuwa, mradi huo utawajengea uwezo wanawake na wasichana katika ushiriki wao kwenye ngazi ya uamuzi ikiwa ni pamoja na uhuru wa kushiriki katika nyanja mbalimbali, kunufaika na misaada ya kisheria itakayotolewa bure kwa njia ya elimu katika vikundi vyao.

Alisema jumuiya hiyo inaundwa na makanisa 12 ambayo mbali na kutoa huduma za kiroho, imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali kwa wananchi katika mikoa na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwanufaisha wananchi.

# Wakazi Ubungo wapatiwa mafunzo

**Na Gwamaka Alipipi**

ZAIDI ya wakazi 500 wa Ubungo jijini Dar es Salaam jana, walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kujiinua kiuchumi pamoja na kulisaidia taifa kufikia malengo ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mafunzo hayo yalitolewa na Shule ya Bethel Mission iliyopo katika wilaya hiyo na kufunguliwa na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Jaffar Kunambi.

Akizungumza na wananchi hao baada ya kufungua, Kunambi alisema mafunzo hayo ni muhimu kipindi hiki ambacho serikali inatekeleza sera ya viwanda.

"Mafunzo hayo yamekuja muda mwafaka hususani kipindi hiki ambacho taifa linazidi kupiga hatua katika maendeleo ya sekta ya viwanda ambayo pamoja na mambo mengine yatasaidia kuwainua wajasiriamali wa bidhaa mbalimbali," alisema Kunambi.

Kunambi aliipongeza taasisi ya 'Bethel Mission' kwa kuandaa mafunzo hayo, huku akiwataka wanamafunzo waliohudhuria kuyatumia ipasavyo kwa lengo la kujiletea mafanikio yao binafsi, familia zao na hata taifa kwa ujumla.

"Niupongeze uongozi wa Shule ya Bethel Mission School kwa kuandaa kongamano hili la siku tano kwa wajasiriamali, huu ni mfano mkubwa wa kuigwa na inaonyesha namna ya kuwasaidia wanajamii wanaoizunguka shule yenu na kutambua kuwa wao ni sehemu ya mafanikio ya shule yenu," alisema Kunambi.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Emmanuel Mshana, alisema mafunzo hayo ni ya siku tano na malengo yake makuu ni kuisaidia jamii inayowazunguka pamoja na wafanyakazi hatua itakayowaongezea kujikwamua kimaisha.

Alisema shule imeamua kudhamini programu hiyo ya ujasiriamali na kupitia mafunzo hayo, walengwa watanufaika kwa kupata faida mbalimbali zitakazowaongezea kipato katika familia.

Alisema kupitia mafunzo hayo yatawawezesha kuanzisha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali watakazofundishwa. Alisema mafunzo hayo yanatolewa na wataalamu mbalimbali waliobobea katika masuala ya ujasiriamali ikiwamo maeneo ya kilimo cha uyoga alichodai kuwa uzalishaji wake ni rahisi na una manufaa makubwa.

# Mamia maeneo ya kuua watu yagundulika Korea Kaskazini

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

SHIRIKA lisilo la kiserikali nchini Korea Kusini linasema kuwa limegundua maeneo 318 nchini Korea Kaskazini ambayo yanatumiwa na serikali kuua watu hadharani.

Shirika hilo limewahoji watu 610 waliotoroka Korea Kaskazini zaidi ya miaka minne iliyopita, limeorodhesha mauaji yaliyotekelezwa miongo kadhaa iliyopita, ambayo yalijumuisha makosa kama ya wizi wa ng'ombe na kutizama televisheni ya Korea Kusini.

Mauaji ya hadharani yalifanywa karibu na maeneo ya mtoni, viwanjani, sokoni, shuleni, na viwanja vya michezo, lilisema shirika hilo la kutetea haki.

Kundi la watu 1,000 au zaidi walikua wakijitokeza kushuhudia mauaji hayo, lilisema shirika hilo katika ripoti yake inayofahamika kama "Ramani ya hatma ya waliofariki", iliyotolewa jana.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa familia za waliohukumiwa kifo, wakiwamo watoto wakati mwingine zililazimishwa kushuhudia mauaji hayo.

Miili ya waliouawa haikuwahi kupewa familia zao wala kuoneshwa mahali ilipozikwa.

Kwa mujibu wa ushahidi, mtu mdogo zaidi kushuhudia mauaji hayo alikuwa na miaka saba.

Ilieleza kuwa mauaji mengine yalikuwa yakitekelezwa katika vituo vya kuzuilia watu kama vile jela na kambi za kufanya kazi, kwamba watu walioshitakiwa kwa uhalifu wa kisiasa wanalazimishwa kufanya kazi ngumu kama vile ya uchimbaji madini na kukata miti.

Mmoja wa watu waliokimbilia Korea kusini ambaye alizuiliwa katika kambi ya kazi mwaka 2000 alielezea jinsi wafungwa 80 walivyolazimishwa kushuhudia mauaji ya wanawake watatu walioshitakiwa kwa jaribio la kutorokea China.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa mauaji ni mbinu kuu inayotumiwa na utawala kuwatia hofu wananchi wanaojihusisha na vitendo vinavyodhaniwa kuhujumu serikali.

Ilieleza kuwa, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na watu waliotoroka, mauaji mara nyingi yalikua yakitekelezwa kupitia kikosi maalumu cha kuwapiga watu risasi.

Mauaji kama hayo mara nyingi yalihusisha maofisa watatu wanaopiga risasi mtu aliyehukumiwa kifo.

Baadhi ya watu waliohojiwa walisema kuwa watu waliopewa jukumu la mauaji walionekana kuwa walevi.

Mmoja alisema: "Hii ni kwa sababu kazi ya kuua ni ngumu sana na huathiri hisia ya mtekelezaji wa kitendo hicho".

Ethan Shin, mmoja wa waandalizi wa ripoti hiyo aliiambia Shirika la Habari la AFP kwamba: "Huenda idadi ya mauaji ya watu hadharani imeanza kupungua, lakini Pyongyang huenda pia inafanya hivyo kisiri inapojaribu kujionesha kama taifa la kawaida".

Maofisa wa ngazi ya juu wa Korea Kaskazini nao walikuwamo kwenye mauaji hayo, mwaka 2013, mjomba wa kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong-un aliuawa kwa kufanya kosa la uhaini.

Lakini ripoti hiyo imeshindwa kuthibitisha kutoka kwa mauaji hayo kwa sababu visa vya watu kudaiwa wameuawa na baadae kubainika kuwa uwongo vimewahi kutokea .

Mwaka 2013, Mwimbaji maarufu wa Korea Kaskazini Hyon Song-wol alidaiwa kuuawa hadharani, na hata Gazeti moja la Korea Kusini likaripoti kuwa aliuawa kwa kupigwa risasi huku likieleza kuwa alimiminiwa risasi huku waimbaji wa bendi yake wakishuhudia.

Lakini mwimbaji huyo alionekana mwaka 2018 akiwa miongoni mwa wajumbe wa Korea Kaskazini waliozuru Seoul kabla ya mashindano ya Olimpiki ya msimu wa baridi.

*BBC*

## Jela miezi sita ukikutwa ukimsaidia ombaomba

**KAMPALA, Uganda**

SERIKALI ya Uganda imetangaza kutekeleza sheria inayopiga marufuku utoaji wa msaada wa pesa au chakula kwa watoto ombaomba mitaani nchini humo, lengo kubwa likiwa ni kuwaondoa watoto hao barabarani.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, mtu yeyote anayetoa msaada wa pesa au chakula kwa watoto omba omba, atakuwa amefanya kosa la uhalifu na anaweza kufungwa miezi sita gerezani au kutozwa faini ya wastani ya Sh.41, 350.

Waziri msaidizi wa Vijana na Watoto Uganda, Nakiwala Kiyingi, alisema wizara hiyo kwa ushirikiano wa maofisa wa usalama, wameanza kutekeleza sheria iliyopitishwa na mamlaka ya Jiji la Kampala KCCA, mwezi uliopita.

Kiyingi alisema kosa la kusaidia watoto ombaomba watu wengi wanaliona kama ni kitendo cha ukarimu.

Alisema ameshapatiwa bilioni 3.4 zitakazotumika kuwapa makazi na chakula watoto hao ombaomba barabarani.

"Hakuna tena kumpa mtoto ombaomba pesa au hata ndizi. Ukifanya hivyo ni sawa na kuchangia kufanya kosa la uhalifu. Hawa watoto wanatumika kama biashara. Wanaomba kwa niaba ya watu wazima," alisema Kiyingi na kuongeza:


"Kwa kila kundi la watoto watano, kuna mtu mzima hapo karibu amejificha kukusanya pesa unazowapa hawa watoto. Tunajua mambo haya yote. Kwa hivyo, usitoe msaada wa chakula wala pesa kwa watoto walio barabarani, ni jukumu langu kufanikisha mahitaji yao kwa sababu nimepewa pesa na serikali,"

Mhadhiri wa masuala ya kijamii Chuo Kikuu cha Kyambogo, Younous Lubuuka, ambaye pia ni mtetezi wa haki za kiraia, alisema matumaini ya hatua ya serikali kufaulu ni madogo.

"Ni njia njema. Wale wanaoweza kuwaweka shuleni, wawaweke shuleni. Wa kupewa mafunzo ya kazi ya kimaisha waweze kujitegemea, nao wapewe. Ni sera nzuri, ni sheria nzuri lakini utekelezaji wake ndio tatizo. Naona ni jambo ambalo halitafaulu", alisema Lubuuka.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Watoto na Vijana ya Uganda, jumla ya watoto 15,000 wapo kwenye barabara za Uganda, wakitegemea ukarimu wa wapita njia kuwalisha, 2000 kati yao wakiwa jijini Kampala.

*VOA*



Wanajeshi wa Sudan wakiwa katika doria, baadhi ya wanajeshi wa nchi hiyo wamekamatwa kwa kosa la kuua raia. **PICHA: REUTERS**

## Wanajeshi wakamatwa kwa tuhuma za kuua raia

**KHARTOUM, Sudan**

BARAZA la kijeshi nchini Sudan limewasweka rumande wanajeshi kadhaa waliohusika na mauaji ya waandamanaji.

Wakati hali hiyo ikitokea, Marekani imetangaza kumtuma mjumbe wake wa ngazi ya juu kwenda mjini Khartoum.

Wanajeshi kadhaa wanashikiliwa rumande kufuatia kuuawa kwa idadi kubwa ya watu katika maandamano ya amani mjini Khartoum wiki iliyopita.

Jumatatu usiku Marekani ilitangaza kwamba mjumbe wake wa ngazi ya juu kuhusu Afrika, Tibor Nagy, ataelekea Sudan kukutana na makundi ya upinzani pamoja na baraza la kijeshi linaloshikilia madaraka ya nchi kwa sasa.

Lakini nchini Sudan baraza la kijeshi la mpito lilitoa taarifa hiyo kupitia Shirika la Habari la Sudan (Suna) likisema kuna ushahidi wa awali uliopatikana dhidi ya wanajeshi kadhaa kuhusiana na kuuliwa kwa waandamanaji 100 na kujeruhiwa kwa wengine zaidi ya 500 wiki iliyopita.

Wanajeshi hao imearifiwa kwa sasa wanashikiliwa rumande mjini Khartoum. Baraza la kijeshi pia limesisitiza kwamba halitochelewesha hatua ya kuwawajibisha wote waliokutwa na hatia kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Naibu Mwenyekiti wa Chama Cha Ummah kuhusu kitendo cha kuuawa kwa raia alisema: "Kilichotokea ni kitu kisichokubalika na kinachozua maswali mengi na tunakitizama kama njia ya kuvuruga mustakabali wa Sudan na umuhimu wa amani ambayo inahitajika kwa uthabiti, usawa na demokrasia nchini Sudan."

Hali imeendelea kuwa ya wasiwasi na mashaka katika Mji Mkuu wa Khartoum ambapo hadi jana iliarifiwa kwamba maduka mengi yalikuwa yamefungwa katika siku ya pili ya mgomo na maandamano ya nchi nzima yaliyoitishwa na makundi ya upinzani.

Mohammed Salem ni miongoni mwa waandamanaji na mkazi wa Khartoum aliyesema hakuna njia nyingine mbadala ya kulishinikiza Jeshi isipokuwa kuendelea na harakati za maandamano.

"Bila shaka ni kwamba harakati hizi za kuvunja sheria zinaiathiri nchi. Lakini ni kitu ambacho bado kinahitajika kuendelea kufanyika. Watu wamepata shida sana na ikiwa hawatofanya hivi basi harakati za mapinduzi zitakuwa zimepotea," alisema Salem.

Juhudi za kutafuta suluhisho wa mgogoro huo kati ya Jeshi na makundi ya upinzani zilizofanywa na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed aliyekutana na pande zote wiki iliyopita bado hazijaonesha mafanikio yoyote.

*DW*

# ACT kuwaendea kortini wakurugenzi kisa uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinatarajia kufungua kesi ya kikatiba chini ya hati ya dharura kuomba tafsiri ya kimahakama iwapo hukumu ya Mahakama Kuu kwenye kesi ya Chacha Wangwe inaathiri ushiriki wa Wakurugenzi wa Halmashauri kama wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Zitto alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza juu ya maamuzi ya kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho kilichofanyika juzi.

"Kwa uzito wa kipekee, Kamati Kuu imeendelea kuwapongeza, mwanaharakati, Chacha Wangwe na Wakili Fatuma Karume kwa kusimamia vema kesi ambayo Mahakama Kuu ya Tanzania ilibatilisha vifungu kwenye sheria ya uchaguzi ambavyo vilikuwa vinawapa nafasi wakurugenzi kuwa wasimamizi wa uchaguzi," alisema Zitto.

Aliongeza: "Chama chetu kitaendelea kuwaunga mkono katika kuhakikisha kuwa uamuzi wa Mahakama Kuu unaheshimiwa, pia Kamati Kuu imewaagiza wanasheria wa chama kufungua kesi ya kikatiba chini ya hati ya dharura kuomba tafsiri ya kimahakama iwapo hukumu ya Mahakama Kuu kwenye kesi ya Chacha Wangwe inaathiri ushiriki wa wakurugenzi wa halmashauri kama wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa."

Pia alisema chama hicho kimewaelekeza wanasheria wake kwa upande wa Zanzibar kufungua mashtaka ili kuondoa vifungu vipya vya sheria ya uchaguzi Zanzibar ambavyo ni hatari kwa uchaguzi huru na haki.

Zitto alisema kuwa chama hicho kitaendelea pia kushiriki katika kupigania tume huru ya uchaguzi pamoja na kushirikiana na vyama vingine vya upinzani katika kupigania demokrasia.



Mkurugenzi wa Biashara wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, Fimbo Butallah (kushoto), akikabidhi pakiti ya sukari kwa mmoja ya wafanyakazi wa kiwanda hicho, Bonoso Mlowe, wakati wa sherehe za kufunga msimu wa uzalishaji wa kiwanda hicho kwa mwaka 2018/2019, zilizofanyika kiwandani hapo mkoani Morogoro juzi, ambapo kiwanda hicho kilizalisha tani 134,116 za sukari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia kufungua mkutano kupambana na uhalifu

**Na Grace Semfuko, MAELEZO**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mkutano wa kimataifa wa taasisi zinazokabiliana na uhalifu unaovuka mipaka kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (ARINSA), utakaofanyika leo, Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Augustine Mahiga, alisema jana lengo la mkutano huo ni kuangalia mafanikio tangu kuanzishwa kwake, upungufu uliojitokeza pamoja na kupanga mikakati ya pamoja na kukabiliana na uhalifu mpya.

"Tunaadhimisha miaka kumi sasa, tunayo mafanikio makubwa, lakini pia tunazo changamoto kadhaa ambazo tunataka kuzifanyia kazi ili tuziondoe kabisa, kuanzishwa kwa ARINSA kunatokana na ukweli kwamba kwa sasa duniani kote imekubalika kuwa utaratibu uliozoeleka wa kutoa adhabu za vifungo kwa wahalifu sio njia madhubuti ya kuzuia uhalifu, badala yake ni kutaifisha mali zinazohusiana na uhalifu huo," alisema Waziri Mahiga.

Alisema ARINSA unaadhimisha miaka kumi tangu kuanzishwa kwake Machi 2009 na Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano huo.

Aidha, alisema nchi wanachama 16 zenye wajumbe zaidi ya 250 wakiwapo wawakilishi wa Taasisi za mashtaka na makosa ya jinai wanahudhuria mkutano huo wenye ajenda ya kushirikiana katika kuondoa uhalifu mkubwa unaovuka mipaka na kuhakikisha wahalifu hao hawanufaiki na shughuli hiyo kwa kurejesha mali zinazohusiana na uhalifu.

Rais wa ARINSA, Mkurugenzi wa Mashtaka chini (DPP), Biswalo Mganga, alisema Tanzania kama nchi mwenyeji wa mkutano huo imenufaika na umoja huo kutokana na kukabiliana na uhalifu ambao ulishika kasi.

Alisema katika mkutano huo pia wataitangaza Tanzania kwenye vivutio mbalimbali ili kukuza utalii wa ndani na kuongeza Pato la Taifa kwa fedha za kigeni zitokanazo na utalii.

## Shule yapata ukombozi madarasa, madawati

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Chali iliyopo kata ya Ndono, Wilaya ya Uyui mkoani Tabora, wamepata neema baada ya kupewa msaada wa madarasa na madawati 80.

Msaada huo uliotolewa na Kampini ya JTI Leaf lengo lake ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na vyumba vya kutosha vya madarasa.

Kampuni hiyo iliikabidhi shule hiyo madarasa matatu, madawati ma ofisi moja katika makabidhiano yaliyoshuhudiwa na Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Gift Msuya, ambaye alilifungua jengo hilo kwa kuweka jiwe la msingi na kusema kuwa kampuni ya JTI Leaf imewasaidia kutatua changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa inayozikabili shule nyingi za msingi.

"Serikali inatambua mchango wa kampuni ya kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo wanaifanya katika maeneo ambayo wananunua tumbaku," alisema.

Mkuu huyo wa Wilaya aliwataka wananchi waendelee kuchangia miradi ya maendeleo katika shule hiyo hasa kukamilisha maeneo yaliyobaki, na yeye akianza kwa kuahidi kutoa mifuko 20 ya saruji ifikapo mwisho wa mwezi huu.

"Ili kuondoa hali ya wanafunzi watakaoendelea kusomea katika madarasa ya zamani kuona wanabaguliwa ni vyema wananchi mkajitahidi nanyi kutafuta fedha kwa ajili ya fundi atakayefanya matengenezo ikiwamo kupaka rangi ili yafanane na madarasa haya mapya yaliyojengwa na kampuni hii," alisisitiza.

Mkurugenzi Mkuu wa JTI Leaf, John Gauna, alisema kampuni hiyo imekuwa ikifanya miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo ambayo wananunua zao la tumbaku ikiwamo miradi ya elimu, maji na afya na kuwataka wakulima wa tumbaku kuzingatia vigezo vyote vilivyowekwa ikiwamo sua la kutokomeza utumikishwaji wa watoto na utunzaji wa mazingira.

Alisema makabidhiano hayo ya madarasa yalienda sambamba na Siku ya Maadhimisho ya Kutokomeza Utumikishaji wa Watoto Duniani (WDACL) na Kauli Mbiu ya mwaka huu ni, 'Watoto hawatakiwi kufanya kazi mashambani, bali kufanyia kazi ndoto zao.'

Mwalimu mkuu Bwire Mbuya, aliishukuru kampuni ya JTI kwa kuwajengea jengo hilo kwa kuwa limeondoa upungufu wa vyumba vya madarasa.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NYUMBA /VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA DODOMA IRINGA RD KARIBU NA KITUO KIKUU CHA POLISI KIWANJA 1680sqm simu 0659 755 011

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,

2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## CHETI KIMEPOTEA



**ELISAMEHE REUBEN MARKO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0758/0041**kilichotolewa na KIJOTA SEKONDARI mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIL/RB/49323/2019.**

115269102

## KUPOTEA KWA VYETI



**Christopher G. Mrema** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatvyo: Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1330-0046** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007, katika shule ya Sekondari Presbyterian Seminary,cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1178-0523 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Arusha Modern. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **AR/RB/5533/2019**

115268402

## KUPOTEA KWA CHETI



**Saumu Bakari** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0516/011** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 1990, katika Shule ya Sekondari Mombo. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **CD/IR/RB/3489/2019**

115268002


## KUPOTEA KWA CHETI



**Mwajuma S. Abdalla** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.382/40** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 1983, katika Shule ya Sekondari Tumekuja. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **CD/IR/RB/3488/2019**

115268102

## KUPOTEA KWA CHETI



**Taifiki H. Daudi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba **S1468-0025** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016, katika shule ya Sekondari Chaume. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **TND/RB/1773/2019**

215267902

## VYETI VIMEPOTEA



**EPIPHANIA MAMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **H 503 29** kilichotolewa na ASSUMPTA SEKONDARI mwaka 1969. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **T 206/510F** kilichotolewa na KILAKALA SEKONDARI mwaka 1971. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No: **991088110577**

115269002

## GOROFA INAUZWA



**BOKO KAMWANGA STR LOW DENSITY AREA BLOC "C", PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SIMON HERIELY LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 547 DHB** TOYOTA MARK X. CHASSIS NAMBA **GRX1200028556.** ENGINE NAMBA **4GREAA8556.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/KIJ/RB/53016/2019.**

115268302

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **NJAMO TRADING CO.LTD** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye Namba **MC 534 BHL** Aina ya SANYA. CHASIS NAMBA **LKIPCKLISG1045315** ENGINE NAMBA **460417102.** Kwa atakaeiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu kwa KUMB. **MZ/TR/RB 463/2019.**

115269202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARI ABDALLAH SUED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T943 BBG** aina ya Toyota Corola, lenye chesisi namba **AE1105366892** na injini namba **5AH963182** linalomilikiwa na **OMARI ABDALAH SUED.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KAG/BUK/48075/2019.**

115269302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MZALENDO TRANSPORT Co. LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI AINA YA MISTUBISHI FUSO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.155 BTG** YENYE CHASIS NAMBA .FK418H 550187 NA ENGINE NAMBA **6D17693281.** AMEPOTEZA KADI YA GARI ILIYOKUWA NA NAMBA **7344270.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **IR/IR/RB/1837/2019.**

215268202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH ELIAS GODELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HILUX YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.450 AGD** YENYE CHASIS NAMBA **YN560008883 ,** ENGINE NAMBA **2Y0439969.** AMEPOTEZA KADI ILIYOKUWA NA NAMBA **6241389.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.TAARIFA YA POLISI: **IR/IR/RB/1921/2019.**

115269602

**PRIMARY COURTS ADMINISTRATION OF ESTATE**

**FORM NA. 11 EST 2**

**CITATION**


**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MABIRA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA 11/2019**

**Ombi la kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya marehemu Charles John Amani**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**
Kuwa na uhusiano na marehemu
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyu.

Wanaalikwa kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/06/2019 kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani unaweza kukaguliwa Tarehe ........................



115269502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **HASSANI ALLY RUGA** wa **TANGA,** mtu mzima, mwenye akili zangu timamu bila kushawishiwa na mtu yeyote kwa hiari yangu mwenyewe ninaapa na kuthibitisha haya yafuatao:-

1. **KWAMBA mimi HASSANI ALLY RUGA** ni mmiliki wa kiwanja **Plot No.7 BLOCK "J" eneo la MABAWA** jijini Tanga.
2. **KWAMBA** kwa bahati mbaya hati ya kumiliki kiwanja hicho imepotea nimefanya juhudi ya kuitafuta lakini sikufanikiwa kuipata nimefika kituo cha polisi Mabawa na kupewa loss report yenye namba **NG/RB/218/2018** ya tarehe 16/02/2018.
3. **KWAMBA** naiomba Ofisi yako itambue nilikuwa na hati ya kiwanja lakini imepotea, kwa hiyo ninaomba kupatiwa hati nyingine kwa jina hili hili **HASSANI ALLY RUGA.**

**UTHIBITISHO.**
Nathibitisha kuwa yote niliyotamka ni ya kweli kweli tupu kwa kadri nijuavyo sheria za viapo.



215267802

KWA MATANGAZO MADOGO MADOGO TUPIGIE

***0767 223311***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

***Tupigie 0767 223 311***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# OBLAK SASA AJIANDAA KUTUA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

KIPA wa Atletico Madrid, Jan Oblak, anajiandaa kuhamia katika klabu yake ya zamani ya utotoni Manchester United, Sky Sports imeripoti.

Oblak mwenye umri wa miaka 26, anaonekana kuwa ndiye mrithi sahihi wa golikipa wa sasa wa Man United, David de Gea ambaye anatajwa kwamba anataka kuondoka.

Man United inakabiliwa na hali halisi ya kumpoteza mlinda mlango wao wa muda mrefu De Gea kipindi hiki cha majira ya joto.

Mkataba wa raia huyo wa Hispania unafikia ukingoni mwaka 2020 na hajaonyesha dalili zozote za kusaini mkataba mpya na 'Mashetani Wekundu' hao.

De Gea amekuwa ni mchezaji mahiri na kiungo muhimu katika Klabu ya Man United katika enzi na baada ya Sir Alex Ferguson, lakini alikabiliwa na misukosuko katika msimu wa 2018/19.

Lakini licha ya makosa aliyoyafanya, bado hadhi yake ni kubwa na kuna tetesi kuwa timu ya Klabu ya Paris Saint-Germain ya Ufaransa iko mstari wa mbele miongoni mwa timu ambazo zimeazimia kusaini naye mkataba.

Na sasa Oblak ndio anaonekana kuwa mbadala wake chini ya Kocha Ole Gunnar Solskjaer, ambaye kwa sasa ana kibarua kikubwa msimu huu cha kukijenga kikosi cha United.

Tayari raia huyo wa Norway amekwishaanza kazi, huku Daniel James akiwa tayari amesaini mkataba na kikosi hicho kutoka Swansea kinatarajiwa kuidhinishwa rasmi wiki hii.

Suala la umri wa Oblak wa miaka 26, linaweza kuwa kichocheo cha Man United kuamua kumchukua na wanaweza kumpa mkataba mrefu.

Oblak alisaini mkataba na Atletico mwaka huu ambao utamuweka hapo hadi mwaka 2023, na kuna kipengele kinachomuwezesha kuuvunja kwa thamani ya euro milioni 120, kwa mujibu wa Gazeti la Mirror.






# BARCA YAONGEZA KASI YA KUMNASA DE LIGT

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA ipo tayari kutoa ofa yao ya mwisho wiki hii kwa ajili ya kumsajili beki wa kati wa Ajax, Matthijs de Ligt, kwa kuanza tena mazungumzo na wakala wake, Mino Raiola, kwa mujibu wa ESPN FC.

Ingawa Barca iliripotiwa kwamba imefikia makubaliano na De Ligt Machi mwaka huu, lakini inaonyesha ofa yao ilikuwa ndogo ikilinganishwa na ile ya Paris Saint-Germain, ambayo nayo imeingia kwenye mbio za kutaka kumsajili.

Juventus, Liverpool na Manchester United pia zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili De Ligt, lakini chanzo kimoja kimeiambia ESPN FC kwamba, miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich imejiondoka kwenye mbio hizo.

Barca imekataa kuongeza ofa yao baada ya De Ligt na Raiola kuongeza mahitaji mengine na mazungumzo yalisimama kwa muda.

Lakini sasa Barcelona imeripotiwa kutaka kuanza mazungumzo na wakala wake, Raiola wiki hii kwa sababu wanahofia PSG inaweza kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi.

Hata hivyo, hakukuwa na taarifa zaidi kama Barca wataongeza ofa na wanataka kukomaa na ile ya mwanzo.

Hadi sasa, Barca imekataa kumlipa zaidi De Ligt kuliko mchezaji mwenzake wa Ajax, Frenkie de Jong, ambaye anajiunga na timu hiyo mwezi ujao.

Barca tayari ilikuwa na makubaliano na Ajax kwamba wanatakiwa kumshawishi De Ligt kuhamia pale Camp Nou kwa ada ya uhamisho ya euro mlioni 80.

# AS Roma yamtangaza mrithi wa Di Francesco

**ROME, Italia**

KLABU ya AS Roma imemtangaza kocha wa zamani wa Shakhtar Donetsk, Paulo Fonseca kuwa kocha wake mpya na kumpa mkataba wa miaka miwili.

Roma ilimfukuza Eusebio Di Francesco baada ya kutolewa hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Porto, huku Claudio Ranieri akiiongoza kipindi cha msimu kilichobaki na kuiwezesha kumaliza nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Hata hivyo, Roma sasa imemtangaza Fonseca kwamba ndiye atakuwa kocha wao kwa kipindi cha miaka miwili, huku taarifa yao ikisema: "AS Roma ina furaha kuutambulisha uma kwamba, Paulo Fonseca atakuwa kocha mpya wa klabu.

"Kocha huyo mwenye umri wa miaka 46, amekubali kusaini mkataba wa awali wa miaka miwili na 'Giallorossi' kuelekea msimu mpya.

"Katika mkataba huo kuna kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi hadi 2022."

Akizungumza kuhusu tangazo hilo, Rais wa Klabu hiyo, James Pallotta alibainisha: "Tunafuraha kumkaribisha Paulo Fonseca kwenye klabu yetu. Paulo ni kijana na mwenye ari ya kupata mafanikio makubwa."

Kocha huyo aliyeanza kuinoa Braga na Porto kabla ya kwenda kutumia muda wake nchini Ukraine, alisema: "Najisikia furaha kubwa kuteuliwa kocha wa AS Roma na ninaushukuru uongozi wa klabu kwa nafasi waliyonipa."



## HABARI MICHEZO




Kiungo wa Manchester United, Paul Pogba ( watatu kulia), akipozi katika picha na beki wa kati wa Chelsea, Kurt Zouma (wa pili kulia), pamoja na marafiki zao wakati walipokwenda kuhiji Mecca kipindi cha mwezi wa Ramadhan. **PICHA: DAILY MAIL**

# POGBA: NIMEBADILIKA BAADA YA KUHIJI MECCA

**PARIS, Ufaransa**

Paul Pogba amesema kwamba alikuwa 'akijiuliza maswali mengi' kabla ya kugeukia Uislamu na kuwa na 'amani zaidi ndani' yake.

Nyota huyo wa Manchester United, ambaye mwezi uliopita alikwenda kuhiji Mecca na kukaa huko kwa kipindi chote cha mwezi wa Ramadhan, hakuwa Muslimu licha ya mama yake kuwa muumini wa dini hiyo.

Lakini baada ya kupitia kipindi kigumu katika maisha yake, Pogba ameamua kutafuta dini nyingine na kuwafuata marafiki zake wengi kwa kujifunza Uislamu.

Kiungo huyo ambaye amebaki kuwa windo kuu la Real Madrid katika usajili wa majira haya ya joto, amesifu uamuzi wake kwa kumsaidia kuwa mtu mwema.

Alipoulizwa kuwa Muislamu alimaanisha, Pogba alisema: 'Ni kila kitu. Hiyo ndiyo inanifanya ninashukuru kila kitu.

'Imenifanya kubadilika, kutambua mambo katika maisha. Nadhani, labda, inanifanya kuwa na amani zaidi ndani.

'Ilikuwa mabadiliko mazuri katika maisha yangu kwa sababu sikuzaliwa nikiwa Muislamu, hata kama mama yangu alikuwa dini hii. Nilikuwa tu kama hivyo, kuheshimu kila mmoja."

## MARCELO ANATAKA KUBAKI REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

BEKI wa kushoto wa Real Madrid, Marcelo hana mpango wa kuondoka katika klabu hiyo na malengo yake ni kupigania namba, licha ya kusubiriwa kwa ujio wa beki Ferland Mendy, ESPN FC imeripoti.

Marcelo ambaye ameshinda mataji 20 yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2007, kwa sasa beki huyo mwenye umri wa miaka 31, alikuwa na msimu mbaya wa 2018-19, huku nafasi yake mara nyingi ikichezwa na Sergio Reguilon.

Ingawa kurudi kwa Zinedine Zidane Machi mwaka huu kulionekana kama ndio muda wa Marcelo kurudishwa kwenye kikosi cha kwanza, lakini kocha huyo raia wa Ufaransa ameonyesha nia kubwa kwa kumsajili beki wa Lyon, Mendy kwa euro milioni 55, ambapo usajili wake unakamilika wiki hii.

Hata hivyo, rafiki wa karibu wa Marcelo ameiambia ESPN FC kwamba, kusajiliwa kwa Mendy hakujabadili chochote kwa nahodha huyo msaidizi wa Madrid, na sasa anajipanga kuhakikisha anakuwa chaguo la kwanza msimu wa 2019-20.

Kulikuwa na uvumi kwamba, Marcelo angemfuata mchezaji mwenzake wa zamani, Cristiano Ronaldo kwenda Juventus, huku Gazeti la Marca likidai kwamba anaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

Marcelo hayupo na timu ya Taifa ya Brazil inayojiandaa na michuano ya Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, na sasa anatumia muda huo kujifua zaidi kuelekea kipindi cha maandalizi ya msimu mpya kitakapoanza mwanzoni mwa Julai.

Usajili wa Mendy kutoka Lyon ulitarajiwa kukamilika baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kumaliza majukumu na timu ya taifa wiki hii.

## Coutinho afunguka kilichommaliza Barca




**SAO PAULO, Brazil**

MCHEZAJI Philippe Coutinho amebainisha kwamba, kiwango chake pale Barcelona msimu huu hakikuwa kizuri wakati mabingwa hao wa Hispania wakipanga kumuuza.

Coutinho mwenye umri wa miaka 26, alikuwa na mwanzo mzuri baada ya kujiunga na Barca kwa ada ya euro milioni 160 wakati akitokea Liverpool, Januari mwaka 2018.

Lakini katika msimu wake wa pili mambo yameonekana kwenda tofauti na sasa yeye mwenyewe amesema msimu huu ulikuwa mbaya kwake.

"Sikuwa na msimu bora," alisema mchezaji huyo akiwaambia waandishi wa habari wakati akiwa na timu yake ya Taifa ya Brazil inayojiandaa na michuano ya Copa America.

"Ilikuwa ni chini tofauti na nilivyotarajia mwenyewe na jinsi mashabiki walivyotarajia kutoka kwangu.

"Lakini unaweza kurudia kujiamini kwako kwa kufanya kazi kwa bidii, na ndio kitu ambacho nakifanya kwa sasa."

Baada ya Barcelona kupigwa kipigo cha mbwa mwizi na Liverpool na kutolewa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, miamba hao wa Catalunya sasa wanapanga kumuuza Coutinho.

Brazil ambayo ndiyo mwenyeji wa michuano ya Copa America itaanza kampeni yake dhidi ya Bolivia mjini Sao Paulo Jumamosi na pia wapo kundi moja na Venezuela na Peru.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS AMCHAMBUA HAZARD REAL MADRID

●●●Nina furaha, nadhani ni usajili mkubwa, ni mmoja wa wachezaji wa kiwango cha juu duniani...

**MADRID, Hispania**

Sergio Ramos ameweka wazi kuwa kuwasili kwa Eden Hazard hapo Real Madrid kunaweza kuanzisha zama mpya kwa klabu hiyo, wakati pia akisisitiza tetesi za hivi karibuni kuhusu mustakabali wake hakukuathiri tabia yake.

Hazard amekamilisha uhamisho wake kutoka Chelsea kwenda Madrid Ijumaa katika dili ambalo linaweza kuwa limegharimu euro milioni 140 na Ramos ameainisha kuwa anaona nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anaweza kuisaidia Madrid katika kutoa changamoto kwenye La Liga msimu wa 2019-20.

Kikosi hicho cha Zinedine Zidane kilipoteza mechi tatu kati ya nne za mwisho za La Liga katika msimu wa 2018-19 wakati kikimaliza nafasi ya tatu, pointi 19 nyuma ya mabingwa Barcelona, lakini mashabiki wa Madrid watakuwa na matumaini ya kusajiliwa kwa nyota kama Hazard hatimaye kutaziba pengo la Cristiano Ronaldo wakati alipoondoka Santiago Bernabeu kabla ya msimu kuanza.

Ramos alielezea kuridhika kwake wakati wa kuwasili kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, akiwaambia waandishi wa habari: "Nina furaha, nadhani ni usajili mkubwa, ni mmoja wa wachezaji wa kiwango cha juu duniani.

"Ni vizuri kuimarisha kikosi kwa aina hiyo ya wachezaji ambao wanaweza kufafanua zama."

Ramos pia alielezea uamuzi wake wa kujitokeza katika mkutano na waandishi wa habari ambapo alitangaza matamanio yake ya kubaki Madrid hadi atakapostaafu, akisema alitaka kuhitimisha taarifa za vyombo vya habari zilizomhusisha na uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu ya China ['Chinese Super League'].

Beki huyo mwenye umri wa miaka 33, kwa sasa bado yupo kwenye majukumu ya timu ya Taifa ya Hispania na alifunga wakati wakishinda 4-1 kwenye ushindi wa mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Visiwa vya Faroe Ijumaa na kisha Jumatatu akarudi tena nyavuni, safari hii ikiwa ni kwa mkwaju wa penalti wakiichapa Sweden 3-0 katika kinyang'anyiro hicho.

"Ni mwenye furaha sehemu nilipo. Ni mwenye furaha sana hapa Madrid na kukutana na timu ya taifa si ahueni.

"Ni kitu unachokichukulia ufahari. Ni mwenye furaha sana kwa zote timu ya taifa na Madrid.

"Nimecheza kila mchezo kama ni mwisho wangu."

## KWA UFUPI

**OBLAK AIVUTIA PUMZI UNITED**
KIPA wa Atletico Madrid, Jan Oblak, 26, anataka kuondoka majira haya ya joto na inaelezwa Mslovenia huyo anataka kutua Manchester United kuliko Paris St-Germain. ***(ESPN)***

**SARRI AUWEKA USIKU CHELSEA**
CHELSEA inatarajia Maurizio Sarri atatangazwa kuwa kocha wa Juventus ndani ya saaa 48 zijazo, na orodha ya wanaowania nafasi hiyo hapo Stamford Bridge ni pamoja na kocha Derby, Frank Lampard, kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, kocha msaidizi wa England, Steve Holland, kocha wa Ajax, Erik ten Hag, kocha wa Wolves, Nuno Espirito Santo na kocha wa Watford, Javi Gracia. ***(Express)***

**UNITED YAIGOMEA REAL MADRID**
Manchester United imeiambia Real Madrid kwamba kiungo Paul Pogba, 26, hauzwi huku ikikataa kueleza dau inalohitaji ili kumwachia Mfaransa huyo. ***(AS)***

**POGBA KUUZA WATANO JUVE**
Juventus inavutiwa kumsajili kwa mara nyingine Pogba, lakini mabingwa hao wa Serie A watapaswa kuuza wachezaji watano ili kuwa tayari kumudu kumnunua kiungo huyo wa Manchester United. ***(Mail)***

**BARCA HAIPOI KWA DE LIGT**
Barcelona ipo tayari wiki hii kutoa msukumo wa mwisho wa kumsajili beki wa kati wa Ajax na Uholanzi, Matthijs de Ligt, 19, kwa kufungua tena mazungumzo na wakala wake, Mino Raiola. ***(ESPN)***

**ANDERSEN, PRAET WAITESA ARSENAL**
ARSENAL imetoa ofa ya pauni milioni 43 kwa beki wa kati Mdenmark, Joachim Andersen, 23, na kiungo Mbelgiji Dennis Praet, 25, ambazo zimekataliwa na klabu yao Sampdoria, ambayo inataka pauni milioni 49 kwa wote wawili. ***(Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

**KOVACIC ANUKIA JUMLA CHELSEA**
Chelsea ina mawazo ya pili kuhusu kusajili kiungo Mcroatia Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 25, kwa mkataba wa kudumu kutoka Real Madrid. ***(Evening Standard)***

**BUTLAND ANUKIA ASTON VILLA**
WAPANDA Ligi Kuu wapya, Aston Villa wanaandaa pauni milioni 20 kwa ajili ya kumsajili kipa Muingereza Jack Butland, 26, kutoka Stoke City. ***(Sun)***

**MENDY KIMEELEWEKA MADRID**
KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, wakati wa mkutano na waandishi wa habari amefunguka kuwa beki wa kushoto wa Lyon, Ferland Mendy, 24, atajiunga na Real Madrid majira haya ya joto. ***(Marca)***

**WAN-BISSAKA AITESA UNITED**
Manchester United imekuwa ikishawishika kurudi tena kwa beki kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka - licha ya kutoa ofa ya awali ambayo ilikataliwa. ***(Evening Standard)***

**SEMEDO KUACHANA NA BARCA**
BEKI wa kulia, Mreno Nelson Semedo, 25, anaweza kuondoka Barcelona majira haya ya joto na Atletico Madrid inavutiwa naye, lakini miamba hiyo ya Catalunya inataka euro milioni 45 hadi 50 ili kumwachia. ***(Marca)***

**UNITED KUMRUDIA TENA ROSE**
Manchester United inaweza kujaribiwa tena kurejea kuvutiwa kwao na beki wa pembeni wa Tottenham, Danny Rose, 28, baada ya mlinzi huyo kusema anaweza kuondoka Spurs majira haya ya joto. ***(Manchester Evening News)***

**KRUSE APOTEZEWA LIVERPOOL**
Liverpool imetupilia mbali mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Werder Bremen, Mjerumani Max Kruse, 31. ***(Liverpool Echo)***

**DELAP AKARIBIA KUTUA CITY**
Manchester City inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Derby County, Liam Delap, 16, ambaye ni mtoto wa kiungo wa zamani wa Stoke, Rory Delap. ***(Derby Telegraph)***

# BENKI YA EXIM YATANGAZA WA5 WAKUISHANGILIA STARS AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

Benki ya Exim imetangaza washindi wake watano watakaoungana na Watanzania wengine kwenda kuishangilia timu ya Taifa 'Taifa Stars' katika mashindano ya fainali za Kombe la Mataifa ya Africa (Afcon) 2019 nchini Misri.

Katika kampeni hiyo maalum iyofahamika kama "Deposit & Win - Twende Tukaliamshe Misri" ilikuwa inatoa fursa kwa wateja wa benki hiyo kulipiwa gharama zote za safari na malazi, ili waweze kushuhudia mechi za Taifa Stars katika mashindano hayo yanayotarajiwa kuanza Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu.

Washindi waliotangazwa jana ni Musa Mohamed kutoka Mtwara, Athumani Hassani (Manyara), Deogratius Kessy (Arusha), Msimu Ngaruka (Dar es Salaam) pamoja na Justine Tembo wa Arusha ambao wamepatikana kupitia droo kubwa ya kampeni hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mapema jana chini ya uangalizi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT).

Kwa mantiki hiyo, washindi hao watano wataanza kuishuhudia Stars ikicheza mechi yake ya kwanza ya Kundi C dhidi ya Segenal Juni 23, halafu dhidi ya Kenya Juni 27 na kisha itakapoivaa Algeria Julai Mosi, mwaka huu.

Akizungumza baada ya kupatikana kwa washindi hao Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa benki hiyo, Andrew Lyimo, alisema washindi hao watapata fursa ya kuungana na Taifa Stars katika mashindano ya Afcon nchini Misri, huku wakiwa wamelipiwa gharama zote za safari ikiwamo visa, tiketi ya ndege, gharama za tiketi ya kushuhudia mechi hizo pamoja na fedha za kujikimu.

Kwa mujibu wa Lyimo ili kushiriki katika kampeni hiyo, wateja wapya walipaswa kufungua akaunti ya akiba na kuhakikisha kila mwezi ina kiasi kisichopungua Sh. 500,000 au zaidi au kufungua akaunti ya current/biashara ikiwa na wastani wa kila mwezi wa Sh. milioni 10 au hifadhi ya amana maalum (Fixed deposit) yenye thamani isiyopungua Sh. milioni tano.

"Kwa wateja ambao tayari wana akaunti ya Benki ya Exim walichotakiwa kufanya ni kuongeza akiba kwa kiasi cha Sh. 500,000 au zaidi kwa akaunti za akiba au kuongeza kiasi cha Sh. milioni 10 kwenye akaunti zao za Current/biashara au kuwa na hifadhi ya amana maalum (Fixed deposit) yenye thamani isiyopungua Sh. milioni tano," alibainisha.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu, alisema kampeni hiyo inatoa nafasi kwa washindi hao kuweza kushuhudia Taifa Stars ikitimiza ndoto zake za kushiriki katika mashindano ya Afcon baada ya miaka 39 kupita.

Kafu alisema kampeni hiyo ni sehemu ya mkakati wa kibenki katika kutafuta kesho bora kwa wateja wake na jamii kwa ujumla ambapo pamoja na mambo mengine benki hiyo imekuwa ikiunga mkono agenda za kitaifa ikiwsmo suala zima la michezo.




Meneja Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Abdulrahman Nkondo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati akitangaza washindi wa kampeni maalum ya benki hiyo inayofahamika kama "Deposit & Win – Twende Tukaliamshe Misri" watakaoungana na Watanzania wengine kwenda kuishangilia timu ya Taifa 'Taifa Stars' katika mashindano ya fainali za Kombe la Mataifa ya Africa (Afcon) 2019 nchini Misri. Washindi hao walipatikana kupitia droo kubwa ya kampeni hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Wengine pichani ni Msimamizi Mkuu wa Matawi Wateja wa Rejareja wa benki hiyo, Mwinyimkuu Ngaliama (Kulia) pamoja na Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Abdallah Hemedy. **MPIGAPICHA WETU**

## Dereva SportPesa Langalanga ang'ara

**Montreal, Canada**

Dereva wa mbio za Langalanga (Fomular One) wa timu ya SportPesa Racing Point, Lance Stroll, amepata pointi mbili katika mashindano yaliyofanyika mjini Montreal, Canada hayo yakiwa ni mafanikio ya kwanza kwa dereva huyo kwenye michuano hiyo.

Stroll alisema kuwa amepata mafanikio hayo baada ya gari lake kufanya vizuri pamoja na kupata ushindani mkubwa kutoka kwa madereva wengine.

"Gari langu limefanya vizuri sana na najisikia fahari kupata pointi hapa Montreal. Kuongoza mashindano haya haikuwa kazi rahisi na hasa baada ya kupata matatizo kwenye injini. Lakini tuliendelea kusukuma ama kupata pointi," alisema Stroll.

Alisema alianza mashindano vizuri na malengo yao yalikuwa kufika mbali pamoja na changamoto mbalimbali.

"Tulipofika katikati, tulikuwa katika wakati mzuri wa kumfikia Carlos Sainz na kufikia nafasi ya tisa, yalikuwa mashindano mazuri sana kwetu, nilipenda kila dakika niliyokuwa nashindana. Kwa kweli ilikuwa wiki nzuri ya mashindano na hasa baada ya kupata sapoti kubwa ya mashabiki, sitayasahau mashindano haya," alisema.

Kwa upande wa Sergio Perez, alisema haikuwa siku nzuri kwake bali kwa timu na hasa baada ya kupata pointi mbili kupitia kwa Lance.

Afisa Mtendaji Mkuu wa timu ya SportPesa Racing Point, Otmar Szafnauer alisema wamefarijika sana kwa Lance kupata pointi akiwa uwanja wa nyumbani.

# Yanga wapigiwa mbiu ya kuchangishana

**Na Mwandishi Wetu**

WANACHAMA na mashabiki wa Yanga wamesisitizwa kujitokeza kwa wingi katika harambee ya kuchangia klabu yao ambayo inatarajiwa kufanyika Jumamosi kwenye Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema jana kuwa wanahitaji kuona mwitikio mkubwa katika harambee hiyo ili waweze kutimiza malengo ya kukusanya fedha kwa ajili ya kuwasajili wachezaji wenye ubora watakaoitumikia timu yao katika msimu ujao.

Mwakalebela alisema mchakato wa kusajili wachezaji kwa ajili ya msimu ujao haujakamilika, na kinachokwamisha ni kukosekana kwa fedha klabuni hapo.

"Tunahitaji kupata fedha ili tusajili wachezaji wazuri ambao watatumika kwa ushindani klabu yetu, hatutaki kuona msimu ujao tunapoteza mwelekeo, tunawaomba Wana-Yanga kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini kujitokeza kwa wingi au kuichangia klabu kwa njia zilizoelekezwa," alisema Mwakalebela.

**Aliongeza kuwa, en dapo wataimarisha ushirikiano, anaamini malengo ya kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao pamoja na mataji mengine yatatimia.**

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa, Anthony Mavunde, alisema wanawashukuru wadau wote wanaoendelea kuichangia Yanga pamoja na wasanii wa muziki na bongo movie wanavyoendelea kuhamasisha ili watu wafike kwenye harambee hiyo.

"Mbali na kufanya harambee hii kubwa kuliko, pia hapo baadaye tutajipanga kupitia wasanii hawa wafanye tamasha maalumu la kuichangia klabu," Mavunde alisema. Alikitaja kiingilio cha chini katika tamasha hilo litakalofanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni kuwa ni Sh. 50,000.

Baada ya uongozi mpya wa klabu hiyo kuingia madarakani ulitangaza kumkabidhi Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, kiasi cha Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya ambao wanawahitaji katika msimu ujao.

# Ruvuma Queens waanza kwa mauaji

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

MABINGWA wa soka wa mkoa wa Ruvuma kwa wanawake, Ruvuma Queens wameanza vema kampeni ya kusaka tiketi ya kupanda daraja baada ya kuwafurumusha wenzao wa Allans Queens mabao 10-0 katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Filbert Bayi mjini hapa.

Hadi zinakwenda mapumziko, Ruvuma Queens ilikuwa mbele kwa mabao 7-0, lakini Allans Queens ya Mpwapwa Dodoma ikionekana kutokata tamaa na matokeo hayo. Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Chama cha Soka cha Wanawake Mkoa wa Dodoma, Bahati Matola, alisema timu yake inaundwa na wachezaji wengi wachanga, lakini anaamini watashuka wakiwa tofauti katika mechi ya pili.

Matola alisema timu yake ililazimika kuanza kujenga vipaji vipya baada ya wachezaji wake nyota kusajiliwa na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi nyingine za ligi hiyo inayoshirikisha timu saba zitachezwa kesho ni kwa Migoli Queens ya Iringa kuwakaribisha TSC kutoka jijini Mwanza wakati Mapinduzi Queens ya Tanga itaumana na Mburahati Queens ya Dar es Salaam.

Michezo

Jumatano Juni 12, 2019

Nipashe



Ramos amchambua Hazard Real Madrid

HABARI UK 30



Mabeki wa Hispania, Sergio Ramos (kulia) na Inigo Martinez (katikati), wakipambana kumiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Sweden kwenye mechi ya Kundi F kuwania kufuzu Uefa Euro 2020 iliyopigwa katika Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi na Hispania kushinda 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# BOCCO AZUA HOFU SIMBA USAJILI SAUZI

## Ni baada ya Polokwane City ya Afrika Kusini kusema wameshamalizana, uongozi Msimbazi waja juu wasema...

**Na Somoe Ng'itu**

FILAMU na maigizo kuhusu usajili wa wachezaji wa Tanzania umeendelea kuchukua nafasi yake kuelekea msimu mpya baada ya kuwapo na taarifa tofauti kuhusu usajili wa mshambuliaji na nahodha wa mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba, John Bocco.

Taarifa zilizoonekana juzi sambamba na picha katika mitandao ya kijamii, zilionyesha Bocco akisaini mkataba mpya wa miaka miwili wa kuitumikia Simba, lakini jana ofisa mmoja wa Polokwane City ya Afrika Kusini ameweka wazi kwamba mshambuliaji huyo ni mali yao.

Bocco ambaye hakuwa na timu yake katika mchezo wa mwisho wa kufunga pazia dhidi ya Mtibwa Sugar uliochezwa Morogoro, ilielezwa kwamba ni mgonjwa, alionekana akisaini mkataba mpya mbele ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohammed "MO" Dewji.

Kiongozi huyo wa Polokwane alisema kuwa Bocco alisaini mkataba wa kuitumikia klabu hiyo akiwa kama mchezaji huru baada ya kuelezwa amemaliza mkataba na Simba.

Aliongeza kuwa Polokwane City hawatakaa kuzungumza chochote na Simba kwa kuwa walimsainisha kwa sababu hakuwa na mkataba na klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori alinukuliwa jana akisema kuwa wana taarifa kuwa Porokwane FC walimsajili Bocco Aprili 9, mwaka huu, wakati akiwa bado na mkataba na Simba, huku akiendelea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika Mei 28, mwaka huu.

"Unajua mchezaji anaweza kuongea na klabu na kukubaliana miezi sita kabla ya kumalizika kwa mkataba, lakini ni lazima klabu yake ijulishwe hata kama wakijibiwa au la, hawa jamaa walimsainisha bila kututaarifu wakati mchezaji ana mkataba na sisi, lakini waliposikia tumemuongeza mkataba ndiyo wakaja ofisini kusema wanamhitaji, wakati huo tayari sisi tuna taarifa zao kuwa wamemsainisha kabla." alinukuliwa Magori.

Magori alisema kuwa timu hiyo ndiyo ina makosa na kama inaona ina haki basi iende kushtaki Shirikisho la Soka duniani (Fifa).

"Bocco ni mchezaji wetu tumemuongeza mkataba wa miaka miwili, hao wanaosema wamemsajili ni batili," alisema.

Bocco alijiunga na Simba akitokea kwa mabingwa wa Kombe la FA, Azam FC na msimu uliomalizika ameisaidia timu yake kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa pili mfululizo.

Kabla ya kusaini Polokwane City ambayo mkataba wake unatakiwa kuanza Julai Mosi, mwaka huu, Bocco alikuwa anahusishwa na tetesi nyingine za kurejea Azam FC.

Katika tuzo za Mo mwaka jana, Bocco alitangazwa kuwa Mchezaji Bora wa klabu hiyo, tuzo ambayo msimu huu imechukuliwa na mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere.

## Taifa Stars yaongezewa mbinu Afcon

**Na Mwandishi Wetu**

HATUBAKI nyuma! Katika kuhakikisha kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kinakuwa imara na kamili kuwakabili wapinzani wao Misri, wachezaji wa timu hiyo jana walijifunza mbinu za ushindi kupitia njia ya video.

Misri inatarajiwa kuwakaribisha Taifa Stars katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa kesho kuanzia saa 3 : 00 kwa saa za Tanzania jijini Alexandria.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Taifa Stars, Danny Msangi, alisema Kocha Emmanuel Amunike aliamua kutumia njia hiyo ili kubaini idara zenye nguvu na zilizo na udhaifu katika kikosi cha Misri.

Msangi alisema mazoezi ambayo wameshafanya yamewaimarisha na kila mchezaji anaonekana yuko tayari kuanza mapambano katika mechi mbili za kirafiki watakazocheza nchini humo.

"Kesho (leo) tunasafiri kuelekea Alexandria kwa ajili ya mchezo wetu wa kwanza wa kirafiki, kiujumla kambi inaendelea vema, wachezaji wako vizuri na mwalimu anaendelea kuwapa mbinu tofauti tofauti, kama jana (juzi) alitoa mafunzo kupitia video na hii alitaka kuangalia sehemu imara na dhaifu katika kikosi cha Misri ili kusaka matokeo bora," alisema Msangi. Meneja huyo aliongeza kuwa Stars imeweka kambi katika eneo bora na wachezaji wanapata vifaa vyote muhimu vya mazoezi vinavyotakiwa na benchi la ufundi.

"Tunaamini tutapata kile tunachotarajia, maandalizi yetu ni bora na wachezaji wanaocheza kwanza wanahitaji kuweka historia katika mashindano haya, pia hawataki kuonekana walibahatisha kufika hapa," Msangi aliongeza.

Baada ya mchezo wa kesho, Taifa Stars itashuka tena dimbani Jumapili kucheza mechi nyingine ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Zimbabwe.

Inaelezwa kuwa, baada ya mechi hiyo dhidi ya Zimbabwe, Amunike atataja wachezaji wake 23 ambao ndio watapeperusha rasmi bendera ya Tanzania katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 ambazo zitaanza Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >